**USAWIRI WA MANDHARI KATIKA *EMBE TAMU* (NJOGU, 2003), *SIKU YA WAJINGA* (MOMANYI, 2005) NA *NJIAPANDA* (AMANA, 2008)**

**AN EXAMINATION OF SETTINGS IN *EMBE TAMU* (NJOGU, 2003), *SIKU YA WAJINGA* (MOMANYI, 2005) AND *NJIAPANDA* (AMANA, 2008)**

**TASNIFU**

**YA**

**MUTISYA COSMAS MBITHI**

**C50/CE/27926/2013**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA ILI KUTIMIZA BAADHI YA MAHITAJI YA KUTUZWA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA IDARA YA KISWAHILI, CHUO KIKUU CHA KENYATTA.**

**2021**

# UNGAMO

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kikuu kingine.

**MTAFITI**

| | |
|---|---|
| ................................... | [illegible]/3/2022 |
| SAHIHI | TAREHE |

MUTISYA COSMAS MBITHI

Tasnifu hii imewasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Kenyatta.

**WASIMAMIZI**

| | |
|---|---|
| ................................... | 10.3.2022 |
| SAHIHI | TAREHE |

DKT. PAMELA M. Y. NGUGI

IDARA YA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA KENYATTA

| | |
|---|---|
| ................................... | 10/3/2022 |
| SAHIHI | TAREHE |

PROF. CATHERINE NDUNGO

IDARA YA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA KENYATTA

## SHUKRANI

Ningependa kutoa shukrani za dhati kwa Mungu kwa kuniwezesha kufikia kiwango hiki cha elimu. Vilevile, nawashukuru wasimamizi wangu Dkt. Pamela Ngugi na Prof. Catherine Ndungo sina cha kuwalipa Mungu awalinde na aendelee kuwabariki. Maelekezo yenu yalinifaa sana na mikononi penu nilijihisi salama.

Pia, nakishukuru Chuo Kikuu cha Kenyatta na hasa idara ya Kiswahili. Nawashukuru; Prof. Mbaabu, Dkt. Mwihaki, Dkt. Onyango, Dkt. Chacha, Dkt. Wafula, Dkt. Osore, Dkt. Arege, Dkt. Beth na Dkt. Muriithi. Mlinifaa nyote.

Asanteni sana wana "Kiswahili Defence Forces" daima sitasahau mchango wenu kama kikundi tulichofanya kazi pamoja katika shughuli za usomi. Isitoshe nawashukuru wasomi wezangu kwa ushikiriano wenu katika masomo.

Aidha, ningependa kumshukuru babu yangu, Fr. Thomas Kyalo Kibathi kwa kujitolea kwa hali na mali kunilipia karo yangu kuanzia shule ya msingi hadi kiwango hiki mola akujalie maisha marefu.

Kipendacho roho ni dawa, asante sana mpenzi wangu Ann Cosmas kwa mawaidha na msukumo wako kuhakikisha kuwa nimeendelea na masomo. Kwa mama mzazi Mutheu wa Mutisya na watoto wangu Michelle na Shannel pongezi kwa kuvumilia nilipokuwa mbali nanyi.

Kwa kaka zangu Abed Ngei na Thomas Mwaka shukrani za dhati ni mola tu anayeweza kuwalipa.

Mwisho ningependa kumpongeza mwalimu mkuu wa shule ya upili ya Kaliakakya, Bwana Christopher Kiaro kwa kunipa mandhari ya kikazi mazuri yaliyoniwezesha kuendeleza masomo bila tatizo. Wema hauozi mkubwa barikiwa.

## TABARUKU

Na tabarukia kazi hii kwa mpenzi wangu wa roho Anne Ndinda Cosmas na watoto wangu Michelle Mutheu Cosmas na Shannel Mwende Cosmas pamoja na mama mzazi Mutheu wa Mutisya.

## IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza usawiri wa mandhari katika fasihi andishi ya watoto. Mandhari yaweza kuwa mahali, wakati au muda ambao matendo ya kifasihi hufanyika. Malengo yalikuwa; kubainisha aina za mandhari yanayosawiriwa kuwasilisha maudhui katika miktadha ya fasihi andishi ya watoto katika riwaya hizi; *Embe Tamu* (Njogu, 2003), *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005) na *Njiapanda* (Amana, 2008). Vilevile, ulichunguza jinsi mandhari yalichangia sifa za wahusika na mwisho kufafanua matumizi ya lugha katika kusawiri mandhari. Nadharia changamano zilitumika katika utafiti huu. Kwanza, nadharia ya finominolojia iliyoasisiwa na Husserl (1900 - 1901) na kuendelezwa baadaye na Heidegger, Sartre, Merleau (2012), Dordrecht na Boston (1997) na Smith na Thomasson (2005) miongoni mwa wengine. Nadharia hii huchunguza miundo ya uzoefu au ufahamu wa mandhari na jinsi watu wanavyoona vitu au kuvihisi katika mandhari na maana vitu vilivyo nayo kulingana na uzoefu wa mtu na ufahamu wake kuvihusu. Nadharia hii ilitumika kuchunguza aina ya mandhari kwa kuzingatia dhana tofauti katika mandhari na kuyahusisha na miktadha husika ya fasihi andishi ya watoto. Aidha, nadharia ya kimtindo iliyoasisiwa na Leech (1969) ilitumika. Nadharia ya kimtindo hushikilia kuwa lugha hufanikisha kazi ya sanaa katika uzuaji na ubunifu wa kifasihi kwani lugha husaidia kutoa ujumbe wa msanii au mtunzi kwa wasomaji au wasikilizaji. Nadharia hii ilitumika kutathmini matumizi ya lugha katika kusawiri mandhari katika fasihi andishi ya watoto. Ngara (1982), anaonyesha kwamba sehemu mbalimbali kama vile maudhui, mandhari na hata wahusika haviwezi kuwasilishwa bila kutumia lugha. Naye Wamitila (2003), anasema kuwa mtindo humwezesha mwandishi kuwasilisha ujumbe wake na kuonyesha sifa mahususi za mwandishi zilizojitokeza. Mihimili ya nadharia ya finominolojia na kimtindo ilitumika ili kuongoza utafiti na kutimiza malengo ya utafiti. Ukusanyaji data ulikuwa wa maktabani; kusoma vitabu na tasnifu mbalimbali zenye data iliyomnufaisha mtafiti katika kazi yake. Utafiti ulitumia vitabu ambavyo viliteuliwa kimaksudi vilivyolenga watoto ambao ni wa darasa la tano hadi nane kwa kuwa waliyafahamu mandhari halisi na yaliyowapendeza. Data iliyopatikana ilichanganuliwa na matokeo kuwasilishwa kupitia maandishi ya kinathari na maelezo kutolewa. Waandishi wa fasihi watanufaika na mchango wa kazi hii kwani utawaongoza kusawiri mandhari ambayo yatawavutia watoto na kuwasaidia kukua pamoja na kuwapasha ujumbe. Isitoshe, utafiti huu utawafaidi wakuza mitaala kwani wataweza kuteua vitabu ambavyo vitawafaa watoto na mwisho, utafaidi jamii kwa jumla kwani unaweka wazi mandhari ambayo yatawafaa watoto na hivyo kuendeleza jamii toka kizazi kimoja hadi kingine.

## ABSTRACT

This study investigated how settings in written *children's literature* are portrayed. Setting is the place, time or period in which events of literature occur or happen. The study aimed at investigating the types of settings that are portrayed to influence themes in different contexts of written children literature.The examined books were; *Embe Tamu* (Njogu, 2003), *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005) and *Njiapanda* (Amana, 2008). In addition, the study set out to investigate the influence of setting in character traits of actors in written children literature. Lastly, the study described the use of language in portraying settings in children literature. The study used a combination of theories: firstly, it employed the Phenomenology theory by Husserl (1900 – 1901). Phenomenology theory is the philosophical tradition launched in the first half of the 20$^{th}$ century by Edmund Husserl (1900 – 1901), Heidegger, Sartre, Merleau (2012), Dordrecht na Boston (1997) and Smith na Thomasson (2005) and others. This theory studies structures of experience or consciousness that is appearance of things, or things as they appear in our experiences or the ways we experience things thus the meaning which things have in our experience. This theory was used to investigate different types of settings that are portrayed in different contexts of written children literature. In addition, the methodological theory by Leech (1969) was used. The theory insists on the impact of language use in literature works as language is used to pass information. The theory was applied to describe the use of language in portraying settings in written children literature. Ngara (1982), language is an important aspect in developing any literature work. In addition, Wamitila (2003) says that methodology enables the writer to pass message. The principles of these theories were applied in the study to help in attaining the set objectives. The library was used in data collection by going through different books and thesis that have information relevant to the study. Children literature books that had been selected deliberately for children in class five to class eight were used. Data was analysed in accordance with the set objectives and the results were presented in a prose form and elaborations given. The study is of great importance; firstly, to children literature writers because it guides them when portraying different settings that are attractive to children and enable them to grow through acquiring the message in the literature works. Curriculum developers will benefit because it will help them in choosing appropriate books for the children. Lastly, it helps the society at large as the study describes the types of settings that are supposed to be portrayed for children to enable them grow socially and morally from one generation to the other.

## UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU

**Fasihi ya watoto**: Kwa mujibu wa kazi hii, fasihi ya watoto ni ile ambayo iliwalenga watoto walio kati ya miaka kumi hadi kumi na tano ambao wanapatikana darasa la tano hadi darasa la nane kama hadhira.

**Mandhari**: Mandhari ni mahali, wakati au muda ambao matendo katika kazi ya fasihi hufanyika.

**Usawiri**: Hii ni picha ambayo inachorewa msomaji na mwandishi wa kazi ya fasihi kuhusu mahali, wakati, mtu au kitu fulani kupitia kwa maandishi au picha.

**Wahusika**: Viumbe wote au kitu chochote ambacho kilipewa hadhi na mwandishi kutekeleza jukumu lolote katika kazi ya fasihi.

**Watoto:** Katika mkutadha huu, watoto ni wale walio kati ya darasa la tano hadi nane.

## YALIYOMO

UNGAMO ........ ii
SHUKRANI ........ iii
IKISIRI ........ v
ABSTRACT ........ vi
UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU ........ vii
YALIYOMO ........ viii
SURA YA KWANZA ........ 1
UTANGULIZI ........ 1
1.0 Usuli wa Mada ........ 1
1.1 Suala la Utafiti ........ 4
1.2 Malengo ya Utafiti ........ 4
1.3 Maswali ya Utafiti ........ 5
1.4 Sababu za Kuchagua Mada ........ 5
1.5 Upeo na Mipaka ........ 6
1.6 Yaliyoandikwa kuhusu Mada ........ 6
1.7 Misingi ya Nadharia ........ 12
1.7.1 Nadharia ya Finominolojia ........ 12
1.7.2 Mihimili ya Nadharia ya Finominolojia ........ 15
1.7.3 Nadharia ya Kimtindo ........ 15
1.7.4 Mihimili ya Nadharia ya Kimtindo ........ 16
1.8 Mbinu za Utafiti ........ 17
1.8.1 Mtindo wa Utafiti ........ 17
1.8.2 Mahali pa Utafiti ........ 17
1.8.3 Uteuzi wa Sampuli ........ 17
1.8.4 Njia za Ukusanyaji Data ........ 17
1.8.5 Uchanganuzi wa Data ........ 18
1.8.6 Uwasilishaji wa Matokeo ........ 18
1.9 Maadili ya Utafiti ........ 19
SURA YA PILI ........ 20

USAWIRI WA AINA ZA MANDHARI KUWASILISHA MAUDHUI KATIKA FASIHI ANDISHI YA WATOTO ..... 20
2.0 Utangulizi ..... 20
2.1 Mandhari katika *Embe Tamu* (Njogu, 2003) ..... 21
2.1.1 Muhtasari wa hadithi ya *Embe Tamu* (Njogu, 2003) ..... 21
2.1.2 Mandhari ya ghala ..... 22
2.1.3 Mandhari ya sokoni ..... 22
2.1.4 Mandhari ya usafiri ..... 23
2.1.5 Mandhari ya ufugaji ..... 24
2.1.6 Mandhari ya mvua ..... 24
2.1.7 Mandhari ya ukuaji wa mimea ..... 25
2.1.8 Mandhari ya uharibifu wa mazingira ..... 25
2.1.9 Mandhari ya mjini ..... 26
2.2 Mandhari katika *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005) ..... 26
2.2.1 Muhtasari wa hadithi ya *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005) ..... 27
2.2.2 Mandhari ya nyumbani ..... 27
2.2.3 Mandhari ya shuleni ..... 28
2.2.4 Mandhari ya darasani ..... 30
2.2.5 Mandhari ya michezo ..... 32
2.2.6 Mandhari ya makaburini ..... 32
2.2.7 Mandhari ya hospitali ..... 33
2.3 Mandhari katika *Njiapanda* (Amana, 2008) ..... 33
2.3.1 Muhtasari wa hadithi ya *Njiapanda* (Amana, 2008) ..... 33
2.3.2 Mandhari ya barabarani ..... 34
2.3.3 Mandhari ya kidhahania ..... 35
2.3.4 Mandhari ya shuleni ..... 35
2.3.5 Mandhari ya hospitali ..... 36
2.4 Hitimisho ..... 37
SIFA ZA WAHUSIKA KUTOKANA NA MANDHARI ..... 39
3.0 Utangulizi ..... 39
3.1 Sifa za wahusika kutokana na mandhari katika *Embe Tamu* (Njogu, 2003) ..... 40

3.1.1 Sifa za Chandu na familia yake ... 40
3.1.2 Sifa za wafanyibiashara na Chandu ... 41
3.1.3 Sifa za Chandu na Bwaga ... 42
3.1.4 Sifa za mchungaji na ng'ombe ... 43
3.1.5 Sifa za mvua na mbegu ... 43
3.1.6 Sifa za wapita njia, beberu na mwembe ... 44
3.1.7 Sifa za mwembe, wapita njia na mtema kuni ... 46
3.1.8 Sifa za mwembe na Chandu. ... 47
3.2 Sifa za wahusika kutokana na mandhari katika *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005). ... 48
3.2.1 Sifa za Zena, Sadiki, Zito na wazazi wao ... 48
3.2.2 Sifa za Sadiki, Zena, Zito na walimu wao ... 50
3.2.3 Sifa za mwalimu Petro, Rukia pamoja na Sadiki, Zena na Zito ... 52
3.2.4 Sifa za wachezaji na wanafunzi ... 54
3.2.5 Sifa za mwalimu Rukia na wanafunzi ... 55
3.2.6 Sifa za mwalimu Petro na wanafunzi ... 55
3.3 Sifa za wahusika kutokana na mandhari katika *Njiapanda* ... 56
3.3.1 Sifa za Waislamu,Wakristo, mama msaidizi na dereva ... 57
3.3.2 Sifa za Bikizee na Kijana ... 58
3.3.3 Sifa za vijana, walimu na Kiumbe ... 59
3.3.4 Sifa za mama msaidizi, mpokezi, Lulu, madaktari na Bob ... 60
3.4 Hitimisho ... 63
SURA YA NNE ... 64
MATUMIZI YA LUGHA KATIKA USAWIRI WA MANDHARI ... 64
4.0 Utangulizi ... 64
4.1 Matumizi ya lugha katika usawiri wa mandhari katika *Embe Tamu* (Njogu, 2003), *Siku za Wajinga* (Momanyi, 2005) na *Njiapanda* (Amana, 2008). ... 65
4.1.1 Usimulizi ... 65
4.1.2 Taswira ... 69
4.1.3 Chuku ... 73
4.1.4 Tashbihi ... 73
4.1.5 Tashihisi ... 74

4.1.6 Mbinu rejeshi ........................................ 75
4.1.7 Mazungumzo baina ya wahusika ........................................ 75
4.1.8 Methali ........................................ 78
4.1.9 Sadfa ........................................ 78
4.1.10 Ritifaa ........................................ 79
4.1.11 Majazi ........................................ 82
4.2 Hitimisho ........................................ 82
SURA YA TANO ........................................ 83
HITIMISHO, MUHTASARI NAMAPENDEKEZO ........................................ 83
5.0 Utangulizi. ........................................ 83
5.1 Muhtasari ........................................ 83
5.2 Matokeo ya Utafiti ........................................ 84
5.3 Umuhimu wa Matokeo ya Utafiti ........................................ 88
5.4 Changamoto za Utafiti ........................................ 89
5.5 Mapendekezo ........................................ 89
MAREJELEO ........................................ 90

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Usuli wa Mada

Dhana ya mandhari imeelezwa na waandishi mbalimbali. Mbatiah (2001) anasema kuwa, mandhari ni mahali popote ambapo tukio la hadithi hutokea. Anaeleza kuwa mandhari ya hadithi yaweza kuwa ya nyumbani, njiani au mahali kwingineo. Kwa mujibu wa Wamitila (2003), mandhari hutumiwa kueleza sehemu ambako tendo fulani katika hadithi hutendeka. Anasema kuwa, mandhari yana nafasi na umuhimu mkubwa katika hadithi na ni lazima msomaji ajitahidi kuangalia kama kuna uhusiano kati ya mandhari na vipengele vingine vya utunzi kama; wahusika, dhamira, maudhui na lugha. Anasisitiza kuwa, mandhari yaweza kuwa ya kijamii, kitamaduni, kisiasa na kihistoria. Mandhari ni mahali au makazi maalum yaliyojengwa na mtunzi mnamotukia matukio mbalimbali ya kazi ya fasihi (Njogu na Chimerah, 2008).

Njogu na Chimerah (2008) pia wanaeleza mandhari kama mahali ya wahusika pamwe na matukio na inahusu mahali wanamokaa wahusika na kuingiliana katika kazi ya fasihi.Kwa mujibu wa Sweetlands (2017), kuna aina kadhaa za mandhari kama vile; mandhari ya kuongezeka, mandhari muhimu na mandhari halisi.  Mandhari ya kuongezeka ni ya kufikirika na huvutia msomaji lakini hayana umuhimu mkubwa kwa hadithi. Hadithi yenyewe yaweza kutolewa au kusimuliwa katika mandhari yoyote yale. Kinyume na mandhari ya kuongezeka, mandhari muhimu huwa na ushawishi kwa wahusika, matendo na maudhui katika hadithi. Mandhari haya huwa muhimu katika hadithi yenyewe kwa kuwa haingefanyika katika mandhari mengine yale na huelezewa kimahali na kiwakati. Mwisho, mandhari halisi humruhusu msomaji kuangazia nyakati zozote na maeneo tofauti ili kukuza uelewa mzuri wa watu, maeneo na hata nyakati nyingine (Erickson, 2018).

Mandhari huwa na umuhimu mkubwa katika kazi ya fasihi kwanza, mandhari hufanya kazi ya kuchochea ambapo husaidia wahusika kusuluhisha migogoro ambayo imesababishwa na mandhari kwa kuhusisha migogoro yenyewe na mandhari halisi katika jamii. Vilevile, mandhari hufanya kazi ya kuangazia wahusika ili waweze kujisaka na kujielewa (Sweetlands, 2017). Isitoshe, mandhari hutenda kazi kama ishara ya mtu, mahali, hali au tendo fulani ambalo huwa na maana fulani katika hadithi.

Elmeel na Elmeel (1996) wanasema kuwa, mandhari ya maeneo mahususi ya kijiografia husaidia wasomaji kuelewa mandhari yao. Vilevile, mandhari yasiyofahamika husaidia kuelewa mandhari mapya. Wanaendelea kusema kuwa, mandhari huchangia matendo katika hadithi, ploti na wahusika. Wanadai kuwa, uelewa mzuri wa mandhari huchangia sana katika usawiri wa mandhari hayo kwa kuwa matendo ya wahusika na mtiririko au msuko wa hadithi huambatana na mahali na wakati wa hadithi.

Hunt (2006) anasema kuwa, mandhari hutofautiana kutoka hadithi moja hadi nyingine kwa kuwa waandishi tofauti hutumia mandhari kwa malengo tofauti katika kazi zao. Vilevile, anasema kuwa, waandishi husawiri mandhari kwa kutumia hisia, kutazama na kusikiliza miongoni mwa njia nyinginezo. Waandishi wanapaswa kuwa na ufahamu wa mavazi, vyakula, makazi na lugha kuambatana na tamaduni kadha wa kadha ili kuweza kutoa maelezo kuhusu kipindi au wakati na hata mahali ambapo hadithi inasimuliwa (Bakize, 2014).

Michoro hutumiwa na waandishi kusawiri mandhari na wengine hutumia maelezo ili kuweza kufumbata kazi zao katika mandhari ili zieleweke vizuri na msomaji. Mwandishi anapaswa kusawiri mandhari yenye uhalisia na hata kama ni ya kufikirika tu hana budi kuyafanya yaonekane halisi na msomaji kwa kutumia michoro na maneno ili kujenga toni ya hadithi na hisia atakazopata (Fang, 1996).

Oyoo (2003) anasema kuwa, umri ni muhimu katika uteuzi wa mandhari katika fasihi ya watoto. Anasema kuwa, watoto kati ya miaka nne hadi tano, husawiriwa mandhari ya kidhahania au kifantasia ili kuleta mvuto wa kipekee kwa watoto. Watoto kati ya miaka sita hadi nane husawiriwa mandhari ya shuleni na nyumbani. Anaendelea kusema kuwa, watoto kati ya miaka tisa na kumi husawiriwa mandhari changamano hadi pale wanapohitimu umri wa miaka kumi na tatu hadi kumi na tano ambapo mandhari halisi wanayoyafahamu na kuwapendeza husawiriwa.

Santora (2005) naye anasema kuwa, fasihi ni chombo muhimu cha kusaidia watoto kuelewa mandhari yao ya nyumbani, jamii na hata dunia kwa jumla. Anasisitiza kuwa, mandhari katika fasihi ya watoto yanapaswa kuwakilisha mandhari tofauti tofauti na ambayo yanaeleweka na watoto kutoka jamii pana na wala si kikundi fulani cha watoto.

Waandishi wa fasihi andishi ya watoto wanapoandika huwafurahisha na kuwafahamisha watoto, vilevile huwaathiri kukua kijamii na kimaadili. Mwandishi anapoteua mandhari fulani huhakikisha hadithi yake inaambatana na ukweli fulani wa mahali au wakati husika.

Mandhari yaliyojulikana na yaliyosawiriwa vizuri na mwandishi husaidia kujenga taswira kwa msomaji na kusaidia kujenga msukumo chanya kwa msomaji ili aweze kuisoma kazi yenyewe. Mwandishi alivyosawiri kazi yake huwa na athari kubwa sana kwa msomaji kwa sababu vipengele kadha wa kadha vya fasihi kama vile; mandhari, maudhui, wahusika miongoni mwa vingine huingiliana ili kufanikisha kazi yenyewe.

Utafiti huu ulibainisha usawiri wa aina mbalimbali za mandhari kuwasilisha ujumbe katika vitabu teule ambavyo ni; *Embe Tamu* (Njogu, 2003), *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005) na *Njiapanda* (Amana, 2008). Vilevile, utafiti ulichunguza jinsi mandhari yaliyosawiriwa na waandishi wa vitabu teule yalivyochangia sifa za wahusika ambao watoto hujinasibisha nao

wanaposoma vitabu vyenyewe, na mwisho, kufafanua matumizi ya lugha katika usawiri wa mandhari.

## 1.1 Suala la Utafiti

Mandhari anayochorewa mtoto kuhusu hali, mtu au hata eneo fulani la kijiografia katika hadithi hukolea akilini mwake. Hali hii huathiri mtazamo wake wa hali na vitu katika mandhari yaliyomzunguka. Ufahamu wa vitu vinavyomzunguka mtoto na jinsi anavyoviona na kuvihisi katika mandhari, humwezesha kuelewa maana ya vitu hivyo. Ufahamu huu wa mandhari hutokana na uzoefu na ufahamu wake kuhusu vitu alivyotagusana navyo katika mandhari halisi au aliyochorewa katika fasihi andishi ya watoto. Kazi ya fasihi yapaswa kusawiri mandhari ambayo yanaleta uhalisia na hata kama ni ya kufikirika, ifanywe ionekane na msomaji kama halisi. Hii ni kwa kuwa, watoto hujinasibisha na mandhari wanayosawiriwa katika kazi ya fasihi. Hali hii uwawezesha kuyafahamu na kuyaelewa mandhari yanayowazunguka.

Kwa hivyo, palikuwa na haja ya kuchunguza jinsi waandishi teule wa kazi za fasihi andishi ya watoto walivyosawiri aina mbalimbali za mandhari kuwasilisha maudhui na athari za mandhari hayo kwa sifa za wahusika katika hadithi pamoja na matumizi ya lugha katika kusawiri mandhari katika kazi zao.

## 1.2 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga:

a) Kubainisha aina ya mandhari yaliyosawiriwa kuwasilisha maudhui katika; *Embe Tamu* (Njogu, 2003), *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005) na *Njiapanda* (Amana, 2008).

b) Kuchunguza jinsi mandhari yalivyochangia sifa za wahusika katika; *Embe Tamu* (Njogu, 2003), *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005) na *Njiapanda* (Amana, 2008).

c) Kufafanua matumizi ya lugha katika kusawiri mandhari katika; *Embe Tamu* (Njogu, 2003), *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005) na *Njiapanda* (Amana, 2008).

## 1.3 Maswali ya Utafiti

Maswali yafuatayo yaliongoza utafiti:

a) Ni aina zipi za mandhari yaliyosawiriwa kuwasilisha maudhui katika *Embe Tamu* (Njogu, 2003), *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005) na *Njiapanda* (Amana, 2008)?

b) Mandhari yalichangia vipi sifa za wahusika katika; *Embe Tamu* (Njogu, 2003), *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005) na *Njiapanda* (Amana, 2008)?

c) Lugha ilitumiwa vipi katika kusawiri mandhari katika; *Embe Tamu* (Njogu, 2003), *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005) na *Njiapanda* (Amana, 2008)?

## 1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Mada ilichaguliwa kutokana na mtazamo kuwa mandhari aliyochorewa msomaji huwa na ushawishi mkubwa katika upokezi wa ujumbe katika kazi anayosoma. Hii ni kwa sababu mandhari huwasilisha maudhui na hivyo mtafiti alidhamiria kuchunguza mandhari mbalimbali yaliyosawiriwa na waandishi katika miktadha ya fasihi andishi ya watoto.

Isitoshe, mada hii ilichaguliwa kutokana na utafiti wa awali wa Karuga (2005), aliyeangazia suala la mandhari kama kigezo cha tathmini ya vitabu vya fasihi ya watoto. Kwa sababu hii, mtafiti alidhamiria kuchunguza iwapo waandishi wa vitabu vilivyoteuliwa walisawiri mandhari yaliyoafiki kigezo hiki cha fasihi ya watoto na kuwasaidia kukua kimaadili na kijamii.

Zaidi ya hayo, mada hii ilichaguliwa kutokana na utambuzi kuwa mabadiliko ya jamii huathiri usawiri wa mandhari na waandishi waliokulia katika mandhari tofauti na walioishi katika vipindi tofauti vya kihistoria kama vile; *Embe Tamu* (Njogu, 2003), *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005)

na *Njiapanda* (Amana, 2008) ambavyo viliteuliwa kimakusudi kwa misingi ya malengo ya utafiti.

Aidha, mada hii ilichaguliwa kutokana na maoni ya mtafiti kuwa watoto kama viumbe wanaokua hupenda kujinasibisha na mandhari yaliyowazunguka na vilevile wahusika waliosawiriwa katika kazi za fasihi walizosoma. Utafiti huu unadhamiria kuchunguza jinsi mandhari waliyosawiri waandishi wa vitabu vilivyoteuliwa yalichangia sifa bainifu za wahusika.

**1.5 Upeo na Mipaka**

Utafiti huu ulichunguza usawiri wa mandhari katika fasihi andishi ya watoto. Ulishughulikia utanzu wa riwaya tatu za watoto ambazo ni; *Embe Tamu* (Njogu, 2003), *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005) na *Njiapanda* (Amana, 2008).

Utafiti huu ulijikita katika kipengele cha mandhari hasa usawiri wa aina mbalimbali za mandhari ili kuwasilisha maudhui katika fasihi andishi ya watoto. Vilevile, utafiti ulijihusisha na uhusiano wa mandhari na sifa za wahusika na mwisho, kubainisha matumizi ya lugha katika usawiri wa mandhari. Utafiti huu umetumia nadharia changamano; nadharia ya finominolojia na nadharia ya kimtindo.

**1.6 Yaliyoandikwa kuhusu Mada**

Akishughulikia nafasi ya fasihi andishi ya watoto nchini Kenya, Mwanzi (1982) anaonyesha kuwa, fasihi simulizi inasifika sana kuliko fasihi andishi. Vilevile, anaonyesha umuhimu wa kuchorea wasomaji picha mbalimbali kwa kutumia lugha, michoro na mandhari mbalimbali ili wavutiwe na kazi wanayosoma. Anasisitiza kuwa, kila mwandishi wa fasihi andishi ya watoto huandika ili kuchochea watoto kutazama jamii kwa mwelekeo fulani. Anasema kuwa, pana haja ya kuhakiki vitabu vya watoto kabla ya kuwachagulia wavisome. Licha ya kuwa, Mwanzi hajatoa vigezo vya kuhakiki vitabu vya watoto ili viwavutie, utafiti huu wa sasa unaendeleza

maoni yake kwa kuchunguza aina ya mandhari ambayo waandishi wa vitabu teule wanasawiri na uhusiano wa mandhari hayo na vipengele vingine vya fasihi kama vile; wahusika na matumizi ya lugha ili kuunda kazi inayowavutia watoto na kuwasaidia kuelewa kazi yenyewe.

Utafiti wa Akoleit (1990), ulichunguza mvuto na upokezi wa fasihi andishi ya watoto katika kazi ya Barbara Kimenye. Anasema kuwa, fasihi andishi ya watoto inapaswa kumfunza mtoto maadili muhimu. Anasisitiza kuwa, mtoto asomaye kazi ya fasihi ndiye anapaswa kuwa mhakiki wa kwanza wa kazi yenyewe. Anaongezea kuwa, kazi nzuri ya fasihi ya watoto ni ile ambayo umbo lake na yaliyomo yanafaana na kukamilishana ili kuunda kazi yenye mvuto kwa msomaji. Japo Akoleit anaangazia suala la mvuto na upokezi ambapo hajajihusisha na vipengele vingine kama vile; maudhui, mandhari na hata matumizi ya lugha ambavyo ni vipengele muhimu katika kujenga umbo na yaliyomo katika kazi ya fasihi. Utafiti wa sasa uliendeleza kazi hii kwa kuchunguza usawiri wa mandhari mbalimbali katika vitabu teule na kuangazia uhusiano wa mandhari hayo na vipengele vingine kama vile; wahusika na matumizi ya lugha ili kuleta mvuto na upokezi mzuri wa fasihi andishi ya watoto.

Ngari (1990), alifanya utafiti kuhusu maigizo ya kienyeji ya watoto nchini Kenya: nafasi ya kuyatumia katika ufundishaji. Ameangazia vipengele kama vile; utambaji wa ngano, utegaji wa vitendawili na uchezaji wa michezo mbalimbali ya watoto. Utafiti huu haukuangazia usawiri wa mandhari yaliyopatikana katika ukuzaji wa vipengele hivi na hivyo utafiti huu unadhamiria kulijaza pengo hili kwa kuangalia usawiri wa mandhari katika fasihi andishi ya watoto.

Kahenya (1992), akishughulikia maudhui na umuhimu wa vibonzo katika fasihi andishi ya watoto nchini Kenya, anasema kuwa, vibonzo huwavutia watoto kwa kuwa vibonzo huundwa kwa kutumia picha na rangi ambazo huwavutia watoto wenyewe na kuwapa burudani. Anasisitiza kuwa, kwa kutumia kibonzo kama bingwa kunawasaidia watoto kuwa na kielelezo na

kujinasibisha na bingwa huyo. Ijapokuwa Kahenya alionyesha umuhimu wa vibonzo katika kuendeleza maudhui katika kazi ya fasihi hajajihusisha na usawiri wa mandhari ambapo vibonzo kama wahusika wanapatikana. Utafiti wa sasa unaendeleza utafiti huu kwa kuchunguza usawiri wa mandhari katika vitabu teule na kuangazia uhusiano wa mandhari yenyewe na vipengele vingine vya fasihi andishi kama vile; wahusika na matumizi ya lugha.

Karuga (2005), alishughulikia, “uhakiki na upokezi wa fasihi ya Kiswahili katika shule za msingi nchini Kenya.” Anaangazia suala la mandhari kama kigezo cha kutathimini vitabu vya fasihi ya watoto, tofauti na utafiti wa sasa ambapo ulichunguza usawiri wa mandhari yenyewe na uhusiano wa mandhari hayo na vipengele vingine vya fasihi. Utafiti wake utatoa mwongozo wa kuilewe dhana ya mandhari.

Akishughulikia usimilishwaji, Muthubi (2005), anasema kuwa, kazi ambazo zimeilenga hadhira ya watoto zimesimilishwa ili kuifaa hadhira ya watoto katika mandhari tofauti tofauti. Hata hivyo, Muthubi anadai kuwa, nyingi za kazi zilizosimilishwa hazijazingatia mahitaji ya watoto ambao ndio wasomaji wa kazi zenyewe. Anasisitiza kuwa,wasimilishaji wa fasihi andishi ya watoto hawazingatii vipengele kama; lugha na matumizi yake, wahusika, michoro, miongoni mwa vipengele vingine.

Utafiti huu japo uliangazia usimilishwaji wa vitabu vya fasihi, haujashughulikia mandhari ya fasihi andishi ya watoto na kushughulikia tatizo analokubali yeye mwenyewe kuwa vitabu vilivyosimilishwa havijazingatia mahitaji ya watoto. Utafiti wa sasa ulichunguza usawiri wa mandhari katika fasihi ya watoto na kujaribu kutoa mwongozo kwa waandishi waliosimilisha kazi za fasihi wakilenga hadhira ya watoto wasawiri mandhari yanayowasaidia watoto kukua kijamii na kimaadili na kusaidia watoto kupokea ujumbe kutoka kwa kazi zenyewe.

Utafiti wa Kairu (2005), kuhusu uhalisia na mtindo wa Ken Walibora katika fasihi ya watoto, umeangazia kipengele cha mandhari hasa usawiri na uhalisia wa mandhari. Ameonyesha mandhari ambayo Walibora ameunda katika kazi zake tofauti. Vilevile, ameonyesha matumizi ya lugha ya Ken Walibora. Utafiti huu japo unatoa mwanga kwa utafiti wa sasa ulitofautiana sana kwa kuwa alishughulikia mwandishi mmoja wa fasihi andishi ya watoto ilhali utafiti huu ulishughulikia waandishi tofauti wa fasihi andishi ya watoto wenye mitindo tofauti ya uandishi kama vile; *Embe Tamu* (Njogu, 2003), *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005) na *Njiapanda* (Amana, 2008).

Karanja (2008), akishughulikia usawiri wa masuala ibuka katika hadithi za fasihi ya watoto, suala la mandhari limejitokeza kama suala ibuka katika jamii. Hali hii inajitokeza katika ukataji miti na uchafuzi wa mandhari katika mitaa ya mabanda miongoni mwa masuala mengine. Katika kazi yake, amejihusisha na suala la mandhari kama suala ibuka katika jamii wala si mandhari ya fasihi andishi ya watoto. Tofauti na kazi ya Karanja, utafiti huu ulichunguza masuala haya ibuka endapo yapo katika vitabu vilivyoteuliwa, yalitokea katika mandhari ya aina gani na mandhari haya yalisawiriwa vipi na waandishi na yalikuwa na athari zipi kwa wahusika ambao watoto walijinasibisha nao.

Kulingana na Ruthiiri (2012), vigezo kadha wa kadha hutumiwa kuongoza uteuzi wa vitabu vya fasihi ya watoto kama vile; maudhui, wahusika, ploti, mtindo, lugha na mandhari. Akiangazia ufaafu wa vitabu vya kusoma kwa madarasa ya tano na sita katika shule za msingi, anadai kuwa, mandhari yanayofahamika na watoto huwapendeza. Japo ameshughulikia aina kadhaa za mandhari, hajajihusisha na usawiri wake. Utafiti wa sasa unaendeleza kazi ya Ruthiiri (2012) kwa kuchunguza usawiri wa aina mbalimbali za mandhari katika vitabu vilivyoteuliwa na kuangazia uhusiano wa mandhari yenyewe na vipengele vingine kama lugha na wahusika.

Muusya (2012), ameshughulikia mandhari katika hadithi fupi. Japo kazi hii imeshughulikia mandhari, ni tofauti na utafiti wa sasa kwa kuwa utafiti huu unachunguza usawiri wa mandhari katika fasihi andishi ya watoto na wala si hadithi fupi kwani tanzu hizi ni tofauti na mandhari yake ni tofauti. Muusya (2012) anasisitiza kuwa, mandhari katika hadithi fupi huwa moja na haibadiliki. Utafiti wa sasa ulichunguza aina mbalimbali za mandhari wanayosawiri waandishi na jinsi mandhari anayosawiri mwandishi yanahusiana na vipengele vingine vya fasihi kama vile; wahusika na matumizi ya lugha katika vitabu vilivyoteuliwa yaani; *Embe Tamu* (Njogu, 2003), *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005) na *Njiapanda* (Amana, 2008).

Njue (2015), ameshughulikia tathmini ya hadithi za watoto katika mtandao ambapo alichunguza muundo na mtindo wa hadithi za watoto katika mitandao kinyume na utafiti wa sasa ambapo unaendeleza dhamira yake kwa kuchunguza usawiri wa mandhari katika fasihi andishi ya watoto. Utafiti wa Omuya (2017), kuhusu usimilishwaji wa Biblia kama fasihi ya watoto ambapo alilinganisha matini chasili na matini lengwa ili kuelewa kwa undani marekebisho yaliyofanyiwa matini chasili wakati wa kusimilishwa. Utafiti huu japo umetathmini usimilishwaji wa matini chasili haujajihusisha na usawiri wa mandhari katika kazi hiyo hivyo, utafiti wa sasa unaendeleza azimio hilo na kuchunguza usawiri wa mandhari ili kutoa uelewa mzuri wa kazi zilizosimilishwa.

Odhiambo (2018), amefanya utafiti kuhusu ngano za kifantasia miongoni mwa watoto lakini hakujihusisha na usawiri wa mandhari katika ngano hizo. Utafiti wa sasa umechunguza usawiri wa mandhari katika fasihi andishi ya watoto na kutoa mwongozo kwa utafiti zaidi kuhusu ngano za kifantasia ambapo utafiti zaidi kuhusu usawiri wa mandhari katika ngano za kifantasia waweza kufanywa.

Ngugi (2018), akishughulikia maudhui na mtindo katika ushairi wa watoto uliotungwa kwa lugha ya Kiswahili na kusema kuwa, maudhui na mtindo ni vipengele muhimu katika kazi ya sanaa ambavyo hutegemeana, hujengana na kuathiriana katika kuikamilisha kazi inayohusika. Japo ameshughulikia maudhui na mtindo, hajajihusisha na usawiri wa mandhari. Utafiti wa sasa ulichunguza usawiri wa mandhari yenyewe na uhusiano wa mandhari hayo na vipengele vingine vya fasihi. Utafiti wake utatoa mwongozo wa kuelewa dhana za maudhui na mtindo.

Gatere (2019), amechunguza usawiri wa familia ya kisasa katika fasihi ya watoto nchini Kenya ambapo anakiri kuwa, dhana ya familia ni changamano.Alilenga kubaini ni kwa kiasi gani uchangamano wa kifamilia unaakisika katika hadithi za watoto kwani anasisitiza kuwa, usawiri wa familia ni kiungo muhimu katika uwasilishaji wa maudhui ya kimaadili kwa watoto. Japo amejihusisha na usawiri wa asasi ya kifamilia hajajihusisha na usawiri wa mandhari ambapo familia ya kisasa inapatikana hivyo, utafiti wa sasa unaendeleza azimio hilo kwa kuchunguza usawiri wa mandhari katika fasihi andishi ya watoto.

Akishughulikia dhima za hurafa katika fasihi ya watoto, Ngiti (2019), anadhamiria kubainisha dhima, maudhui na mbinu katika fasihi andishi ya watoto. Alilenga kuthibitisha utendakazi wa hurafa kwa watoto. Japo alishughulikia dhima za hurafa, hajajihusisha na usawiri wa mandhari katika hurafa na utafiti wa sasa utatoa mwanga kwa utafiti wa baadaye kuhusu hurafa kwa kuchunguza usawiri wa mandhari katika fasihi andishi ya watoto.

Mwendwa (2020), ameangazia usimilisho wa vielelezo katika hadithi za watoto na namna vinavyochangia katika uwasilishaji wa ujumbe. Anadai kuwa, mtindo wa lugha, ploti ya hadithi, usawiri wa wahusika na mandhari ya hadithi za watoto hutegemea jinsi ambavyo mwandishi alitumia vielelezo ili kuwasilisha ujumbe. Utafiti wa sasa umeendeleza maoni yake kwa

kuchunguza usawiri wa mandhari na uhusiano wa mandhari hayo na vipengele vingine kama vile; wahusika na matumizi ya lugha.

Masuala kadha wa kadha kuhusu fasihi ya watoto yalishughulikiwa na Mwanzi (1982), Akoilet (1990), Kahenya (1992), Karuga (2005), Muthubi (2005), Kairu (2005), Karanja (2008), Ruthiiri (2012), Muusya (2012), Njue (2015), Omuya (2017), Odhiambo (2018), Gatere (2019), Ngiti (2019) na Mwendwa (2020). Masuala haya ni kama vile; mitindo, upokezi, maigizo, usimilisho, ufundishaji wa fasihi ya watoto miongoni mwa mengine. Suala la usawiri wa mandhari katika fasihi andishi ya watoto halijashughulikiwa. Utafiti huu uliangazia suala lenyewe ili kujaza pengo hilo.

## 1.7 Misingi ya Nadharia

Utafiti huu umeongozwa na nadharia changamano, hususan, nadharia ya finominolojia iliyoanzishwa na Husserl (1900) na kuendelezwa baadaye na Heidegger, Sartre, Merleau, Dordrecht na Boston, Smith na Thomasson (2005) miongoni mwa wengine na nadharia ya uhakiki wa kimtindo iliyoasisiwa na Leech (1969).

Nadharia hizi zimeufaa utafiti huu kwa kuwa mihimili iliongoza kufikia malengo ya utafiti. Nadharia ya finominolojia na Husserl (1900) imesaidia kuchunguza aina ya mandhari yaliyosawiriwa katika miktadha tofauti ya fasihi andishi ya watoto na kuchunguza namna mandhari huchangia sifa za wahusika katika fasihi andishi ya watoto. Nadharia ya kimtindo ya Leech (1969) imesaidia kubainisha matumizi ya lugha katika kusawiri mandhari ili kuwasilisha maudhui katika fasihi andishi ya watoto.

### 1.7.1 Nadharia ya Finominolojia

Kwa mujibu wa Merleau (2012), finominolojia iliasisiwa katika nusu ya kwanza ya karne ya ishirini – 1900-1950. Kulingana na Moran (2000), finominolojia ni tawi la falsafa

linalochunguza miundo ya uzoefu au ufahamu wa mandhari ya jinsi tunavyoona vitu au kuvihisi katika mandhari na maana ya vitu hivyo kulingana na uzoefu na ufahamu wa mtu kuvihusu.

Finominolojia ni tofauti na matawi mengine ya falsafa japo inahusiana na kukamilishana na matawi haya mengine (Mohanty, 2011). Kwa mfano, tawi linalochunguza kuwepo kwa vitu katika mandhari, tawi linalochunguza ufahamu wa vitu na tawi linalochunguza uzuri na ubaya wa matendo. Kulingana na Smith na Thomasson (2005), matawi haya japo tofauti, yanahusiana kwa njia moja au nyingine na tawi la finominolojia kwa kuwa yanasaidia kuunda mkusanyiko mpana wa ufahamu wa mandhari na nikupitia uhusiano huu ambapo tumeweza kuyaelewa mandhari vizuri.

Husserl (1989), akichunguza umantiki, aliangazia ufahamu wa vitu katika mazingira na akasisitiza kuwa maana ya vitu katika dunia hupatikana kupitia hali tofauti za uzoefu wa mtu kuhusu vitu hivyo. Vilevile, alisema kuwa, maana hupatikana kupitia kutenda shughuli mbalimbali za kijamii, kwa kuona, kusikia, kufikiria na hata kuigiza hali tofauti tofauti katika maisha ya kila siku. Alisisitiza kuwa kila binadamu huwa na ufahamu fulani wa hali halisi ya mazingira yanayomzunguka na hali hii humsaidia kuelewa na kupata maana ya vitu katika ulimwengu.

Akiendeleza kazi ya Husserl, Heidegger (1982), aliangazia finominolojia kwa mtazamo tofauti ambapo alisitiza kuwa binadamu na matendo yao huwa katika dunia kila wakati. Anadai kuwa, binadamu haelewi maana ya vitu na mazingira yanayomzunguka kwa kuangazia sehemu fulani ya mazingira hayo bali hupata maana ya vitu kwa kuangalia uhusiano uliopo baina ya binadamu na mazingira yanayowazunguka na jinsi vitu vilivyo katika mazingira hayo tofauti na Husserl aliyesisitiza uzoefu wa binadamu kuyaelewa mazingira.

Naye Moran (2000), aliongezea kuwa vitu vyote katika ulimwengu hupata maana kutokana na jinsi vinavyoonekana na binadamu, uzoefu wa binadamu kuvihusu katika hali halisi ya mazingira. Anasisitiza kuwa, maana halisi ya vitu katika mazingira haipatikani kutokana na ufahamu na uzoefu wa mtu kuvihusu bali pia hupatikana kwa kutafsiri, kuelezea aina tofauti ya vitu kulingana na uzoefu wa mtu kuhusu vitu katika mazingira yanayomzunguka. Kulingana na Moran (2000), akiendeleza kazi ya Satre anasisitiza kuwa, uzoefu wa binadamu kuhusu mazingira yanayomzunguka na shughuli zake za kijamii ni muhimu sana katika kuelewa mazingira na maana ya vitu katika mazingira hayo.

Katika kuasisiwa kwake, tawi hili la falsafa lilitumia mbinu za kitamaduni katika uchunguzi wake wa vitu vilivyoko katika mandhari anavyotagusana navyo binadamu katika maisha ya kila siku. Mnamo karne ya ishirini, Husserl (1900) na wengine waliangazia finominolojia kwa mtazamo wa kisayansi yaani kama falsafa ya akili ambapo walitoa maana ya vitu katika mandhari kutoka kwa mtazamo finyu wa tunachoona na tunachosikia miongoni mwa mengine. Kwa kutumia mtazamo wa kisayansi, waliangazia maana ya vitu kwa mujibu wa uzoefu na ufahamu wa mtu kuhusu vitu katika mandhari. Kwa mfano, manufaa ya vifaa tofauti tofauti, mpito wa wakati, matukio na kadhalika (Merleau, 2012). Kwa kuwa uzoefu wa binadamu umempa ufahamu wa mambo mengi katika akili yake zaidi ya anachoona na kusikia, finominolojia ni pana na hufikia kiwango kikubwa katika kutoa maana ya vitu katika mandhari.

Kulingana na Smith (2013) kila binadamu huwa na uzoefu na ufahamu wa dhana tofauti tofauti katika mandhari kupitia kuona, kufikiria, kuhisia, kutenda, shughuli za kijamii miongoni mwa mengine. Uzoefu huu na ufahamu huu huwa na sifa za kipekee kwa kuwa tunazihisi, tunaishi nazo na kuzitumia katika shughuli tofauti za kijamii. Finominolojia huunda mkusanyiko mpana wa ufahamu wa mandhari yanayomzunguka binadamu yaani jinsi anavyojiona na kuona vitu

katika mandhari yake na anavyotumia vitu katika mandhari kufanya au kutenda matendo tofauti tofauti pamoja na kuingiliana na wanajamii katika shughuli mbalimbali za kijamii (Merleau, 2012).

### 1.7.2 Mihimili ya Nadharia ya Finominolojia

Mihimili ya nadharia ya finominolojia ni pamoja na:

1. Kuchunguza aina ya mandhari kwa kuzingatia dhana tofauti katika mandhari na kuyahusisha na miktadha husika.
2. Uhusika na uchanganuzi wa ufahamu wa mandhari yanayomzunguka binadamu na jinsi maana ya vitu katika mandhari inavyopatikana kutokana na uzoefu na ufahamu wa mandhari husika.
3. Kuchunguza vitu na hali katika mandhari asilia.

Utafiti huu ulitumia mhimili uliohusisha kuchunguza aina ya mandhari kwa kuzingatia dhana tofauti katika mandhari na kuyahusisha na miktadha husika. Vilevile, mhimili uliohusika na uchanganuzi wa ufahamu wa mandhari yaliyomzunguka binadamu na jinsi maana ya vitu katika mandhari ilivyopatikana kutokana na uzoefu na ufahamu wa mandhari husika ulitumika. Mihimili hii imetumika kuchunguza aina ya mandhari yaliyosawiriwa katika miktadha ya fasihi andishi ya watoto hasa vitabu vilivyoteuliwa vya fasihi andishi ya watoto na kubainisha mchango wa mandhari katika sifa za wahusika.

### 1.7.3 Nadharia ya Kimtindo

Miongoni mwa waasisi maarufu wa nadharia hii ni Leech (1969). Leech anasema kuwa, mtindo hurejelea jinsi lugha inavyotumiwa katika miktadha mbalimbali na kwa malengo tofauti. Anaongezea kuwa, athari ya kazi yoyote ya fashi kwa msomaji hutegemea mtindo wa mwandishi

ambaye hutumia lugha kwa njia mbalimbali pamoja na vipengele tofauti vya kimtindo ili kumwadhiri msomaji kihisia na kimawazo.

Naye Ngara (1982) anaonyesha kwamba, sehemu mbalimbali kama vile maudhui na hata wahusika haviwezi kuwasilishwa bila kutumia lugha. Akiendeleza nadharia ya kimtindo Wamitila (2003) anasema kuwa, mtindo humwezesha mwandishi kuwasilisha ujumbe wake kupitia kwa mtindo ambapo jinsi kazi ilivyoundwa huelezewa. Anaongezea kuwa, mtindo huonyesha sifa mahususi za mwandishi zinazojitokeza katika kazi zake. Wamitila anadai kuwa umtindo humwezesha kuchunguza jinsi lugha ilivyotumiwa katika uchanganuzi.

Wanamtindo husisitiza majukumu ya lugha katika upokeziwa ujumbe uliokusudiwa. Nadharia ya kimtindo husisitiza uwiano kati ya ujumbe na lugha. Ina msingi katika dhana kwamba lugha huchangia ufanisi wa kazi ya sanaa kwa namna ambayo hutumiwa katika uzuaji na ubunifu wa kifasihi.

**1.7.4 Mihimili ya Nadharia ya Kimtindo**

i. Wanamtindo husisitiza kuwa lugha hutumika kuwezesha upokezi wa ujumbe uliokusudiwa.
ii. Uwiano kati ya ujumbe na lugha. Lugha husaidia mwandishi kuwasilisha dhana mbalimbali katika sanaa.
iii. Sehemu za kazi ya sanaa kama; maudhui na nyinginezo huwasilishwa kupitia kwa lugha.

Utafiti huu umetumia mhimili uliosisitiza kuwa kazi ya sanaa huwa na sehemu kama ploti, dhamira, maudhui, mandhari na wahusika lakini bila lugha, vipengele hivi haviwezi kuwasilishwa kikamilifu. Hivyo basi mhimili huu umetumika kubainisha matumizi ya lugha katika kusawiri mandhari hasa katika vitabu vya fashi andishi ya watoto vilivyoteuliwa.

### 1.8 Mbinu za Utafiti

Sehemu hii imeshughulikia; mtindo wa utafiti, mahali pa utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo yenyewe.

#### 1.8.1 Mtindo wa Utafiti

Mugenda na Mugenda (1999), wanasema kuwa mtindo wa kimaelezo hutumika kuchunguza hali ya mambo jinsi yalivyo. Mtindo huu ulisaidia kukusanya data kuhusu mada. Kupitia mtindo wa kimaelezo, maelezo kuhusu usawiri wa mandhari katika fasihi andishi ya watoto yalitolewa.

#### 1.8.2 Mahali pa Utafiti

Utafiti huu ulifanyiwa maktabani na mtandaoni ambapo usomaji wa kina wa vitabu, makala, majarida na marejeleo mengine mengi kuhusu mada ulifanywa. Usomi huu wa maktabani ulifaa kwani ulisaidia kupata data faafu kuhusu mada ya utafiti na vilevile kabainisha pengo la utafiti. Aidha, vitabu vilivyoteuliwa yaani; *Embe Tamu* (Njogu, 2003), *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005) na *Njiapanda* (Amana, 2008) vilisomwa na kuchanganuliwa kwa kina ili kupata data iliyofaa utafiti.

#### 1.8.3 Uteuzi wa Sampuli

Sampuli lengwa katika utafiti huu ilikuwa vitabu vifuatavyo vya fasihi andishi ya watoto; *Embe Tamu* (Njogu, 2003), *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005) na *Njiapanda* (Amana, 2008). Mbinu ya usampulishaji iliyotumiwa ni mbinu ya kimaksudi ambapo sampuli lengwa iliteuliwa kutokana na uchunguzi wa mtafiti kupitia usomaji wa kina kwa misingi ya malengo ya utafiti ili mtafiti aweze kuafiki malengo yake.

#### 1.8.4 Njia za Ukusanyaji Data

Data ilikusanywa kwa kusoma kwa kina vitabu vilivyoteuliwa ambavyo ni; *Embe Tamu* (Njogu, 2003), *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005) na *Njiapanda* (Amana, 2008). Kusoma kwa

kuzingatia; aina ya mandhari yaliyosawiriwa kuwasilisha maudhui katika vitabu teule, kuzingatia mchango wa mandhari kwa sifa za wahusika katika vitabu teule na matumizi ya lugha katika kusawiri mandhari katika vitabu teule. Data pia ilikusanywa kwa kusoma vitabu vingine vya ziada pamoja na marejeleo mengine yaliyohusu mada ya utafiti na kuongozwa na malengo ya utafiti pamoja na mihimili ya nadharia husika ambazo ni; nadharia ya finominolojia na nadharia ya kimtindo.

### 1.8.5 Uchanganuzi wa Data

Data kuhusu aina ya mandhari ilichanganuliwa kwa kueleza aina mbalimbali za mandhari yaliyosawiriwa katika vitabu teule yaani; *Embe Tamu* (Njogu, 2003), *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005) na *Njiapanda* (Amana, 2008). Aidha uhusiano kati ya mandhari na sifa za wahusika ulichunguzwa na mwisho kubainisha matumizi ya lugha katika kusawiri mandhari katika vitabu teule.

### 1.8.6 Uwasilishaji wa Matokeo

Matokeo yaliyopatikana yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo. Maelezo haya yalizingatia aina ya mandhari yaliyosawiriwa katika vitabu tuele pamoja na uhusiano wa mandhari hayo na sifa za wahusika na kubainisha matumizi ya lugha katika kusawiri mandhari mbalimbali katika vitabu teule. Uwasilishaji wa data umeongozwa na malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia husika.

Sura ya kwanza ilishughulikia utangulizi uliohusu maswala ya kikaida kwa mujibu wa mahitaji ya idara ya Kiswahili, chuo kikuu cha Kenyatta, kama vile; suala la utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, misingi ya nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada miongoni mwa kaida nyinginezo.

Sura ya pili ilishughulikia usawiri wa aina mbalimbali za mandhari katika fasihi andishi ya watoto. Utafiti ulibainisha aina za mandhari zilizosawiriwa na waandishi wa vitabu teule vya

fasihi andishi ya watoto ili kuafikia mojawapo ya malengo ya utafiti huu. Pia, ulionyesha vile ambavyo kila mandhari yaliosawiriwa yalivyowasilisha maudhui. Sura ya tatu ilishughulikia sifa za wahusika kutokana na kila aina ya mandhari yaliosawiriwa katika vitabu viteule.

Sura ya nne ilishughulikia jinsi ambavyo matumizi ya lugha yalijitokeza katika mandhari yaliosawiriwa. Waandishi wa vitabu teule walitumia mbinu za lugha na tamathali za usemi tofauti.

Sura ya tano ilishughulikia muhtasari wa utafiti, matokeo ya utafiti, mapendekezo ya utafiti miongoni mwa mengineyo.

**1.9 Maadili ya Utafiti**

Mligo (2012), anasema kuwa, wizi wa kitaaluma ni kinyume na maadili ya uandishi. Anasema kuwa, wizi wa kitaaluma huhusisha wizi wa maneno, mawazo au vifungu vya maneno kutoka kwa watafiti au watu wengine bila kuonyesha ni ya nani na chanzo chake. Mtafiti aliepuka haya kwa kutambua mchango wa waandishi wengine na vyanzo vyote vya mawazo yao kwa kufanya unukuzi sahihi wa maandishi yao.

# SURA YA PILI

# USAWIRI WA AINA ZA MANDHARI KUWASILISHA MAUDHUI KATIKA FASIHI ANDISHI YA WATOTO

## 2.0 Utangulizi

Sura hii ilishughulikia usawiri wa aina mbalimbali ya mandhari katika fasihi andishi ya watoto. Nadharia ya finominolojia ya Husserl (1900), ilisaidia kubainisha aina ya mandhari yaliyosawiriwa katika miktadha tofauti ya fasihi andishi na kubainisha mchango wa mandhari katika kuwasilisha ujumbe. Smith (2013) anasema kuwa, kila binadamu huwa na uzoefu na ufahamu wa dhana tofauti tofauti katika mandhari kupitia kuona, kufikiria, kuhisi, kutenda shughuli za kijamii miongoni mwa mengine. Uzoefu na ufahamu huu huwa na sifa za kipekee kwa kuwa binadamu anazihisi, anaishi nazo na kuzitumia katika shughuli tofauti za kijamii. Nadharia hii inajihusisha na uchunguzi wa aina ya mandhari kwa kuzingatia dhana tofauti katika mandhari na kuyahusisha na miktadha husika.

Aina ya mandhari anayosawiri mwandishi katika miktadha mbalimbali husaidia kuelewa dhana mbalimbali katika mandhari husika. Hata hivyo katika kufahamu mandhari, msomaji hupata kupokea ujumbe uliokusudiwa na mwandishi.

Mandhari huwa na umuhimu mkubwa katika kazi yoyote ya fasihi. Hii ni kwa sababu Njogu na Chimerah (2008) wanaeleza kuwa, mandhari yanahusu wahusika pamwe na matukio pamoja na mahali wanamokaa wahusika na kuingiliana katika kazi ya fasihi. Mandhari ya maeneo mahususi ya kijiografia husaidia wasomaji kuelewa mandhari yao (Elmeel na Elmeel, 1996). Vilevile, mandhari yasiyofahamika husaidia kuelewa mandhari mapya. Mandhari katika fasihi andishi ya watoto huwa mengi sana na ambayo hudokezwa tu na huwa sahili. Kudokezwa huku ni muhimu kwa sababu huweza vilevile kudokeza maudhui katika hadithi husika.

Sura hii ilijikita katika kubainisha aina za mandhari zilizosawiriwa kuwasilisha maudhui na waandishi wa vitabu teule vya fasihi andishi ya watoto.Vitabu teule vilivyotumika katika uchunguzi ni pamoja na; *Embe Tamu* (Njogu, 2003), *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005) na *Njiapanda* (Amana, 2008). Vitabu hivi viliteuliwa kimakusudi kama sampuli ili kutumiwa katika kuafikia malengo ya utafiti. Kila kitabu kilitolewa muhtasari wa matukio yaliotukia katika hadithi nzima.

### 2.1 Mandhari katika *Embe Tamu* (Njogu, 2003)

Kwa mujibu wa orodha ya vitabu vya ziada na Tume ya Kukuza Mitaala Nchini Kenya (Ministry of Education Science and Technology, 2015), *Embe Tamu* ni kitabu cha ziada kinachonuiwa kuendeleza msingi wa kusoma na kukuza uwezo wa kusoma wa wanafunzi wa darasa la tano katika shule za msingi. Kitabu hiki kiliandikwa na Kimani Njogu mwaka wa 2003. Kitabu hiki kilitumiwa kuchunguza usawiri wa aina mbalimbali za mandhari.

#### 2.1.1 Muhtasari wa hadithi ya *Embe Tamu* (Njogu, 2003)

Mwandishi anasimulia asili ya tunda la embe ambapo anaonyesha jinsi mmea wa mwembe unavyotokea kutokana na mbegu la embe. Anaonyesha safari ya mwembe kumea kuanzia tunda lenyewe likiwa limehifadhiwa ghalani likiwa tayari kupelekwa sokoni. Mwandishi anatumia mhusika Chandu anayepeleka maembe sokoni na kwa bahati mbaya anaangusha embe moja linaloliwa na mhusika mwingine aitwaye Bwaga. Baada ya kula tunda, Bwaga anatupa mbegu ardhini. Mwandishi anasawiri mandhari haya ili kuonyesha chanzo cha mmea wa mwembe ambapo anasawiri mfugaji anayeongoza ng’ombe wanaosaidia kuizika ile mbegu ardhini. Mwandishi anafungua ukurasa mpya wa mmea wa mwembe ambapo anaonyesha changamoto zinazokumba mwembe unapokua kama vile; kuliwa na beberu, kuvamiwa na nyigu, kukatwa na kuchomwa makaa. Hata hivyo, mwandishi anaonyesha jinsi mwembe unavyostahimili madhila

haya yote na mwishowe kufikia kukomaa na kutoa embe tamu linaloliwa na mhusika yule yule wa mwanzoni Chandu aliyeanzisha safari ya embe la mwanzo lililotoa mbegu iliyoota mwembe. Sasa Chandu ni mzee na anajikinga hadhari za jua chini ya mwembe huo. Mwandishi amesawiri mpito wa wakati kupitia asili ya mmea wa mwembe kusawiri aina mbalimbali za mandhari na kuwasilisha maudhui kadha wa kadha.

### 2.1.2 Mandhari ya ghala

Kwa mujibu wa Smith (2013), maana ya vitu hupatikana kupitia kutenda shughuli mbalimbali za kijamii. Anasisitiza kuwa, binadamu huwa na ufahamu fulani wa hali halisi ya mazingira yanayomzunguka na hali hii humsaidia kuelewa na kupata maana ya vitu katika ulimwengu. Hadithi inapoanza tunaambiwa kuwa Chandu alikuwa karibu na ghala. Hili ni ghala lililokuwa nyumbani kwao, walipokuwa wanahifadhi mavuno yao. Tunaelezewa kwamba kulikuwa na kikapu kilichokuwa kimejaa maembe yaliyokuwa tayari kupelekwa sokoni. Ilikuwa zamu ya Chandu kwa sababu nduguze watatu walikuwa wamemtangulia kwenda sokoni wiki tatu zilizopita (uk. 2).

Mlikuwa pia na magunia yaliyojaa mavuno. Magunia haya yamejaa maembe ambayo ni kama mabichi na magunia mengine yamefunikwa. (uk. 1).

Kwa kuwa maana ya vitu hupatikana kupitia kutenda shughuli mbalimbali za kijamii (Moran, 2000). Mandhari ya ghala kwa kina Chandu yamesawiriwa na mwandishi kuwasilisha maudhui ya ukulima. Wao ni wakulima kwa sababu wametunza mimea ya miembe hadi ikanawiri na kuwapa mavuno ya kutosha katika msimu huo wa maembe.

### 2.1.3 Mandhari ya sokoni

Chandu anaelezea kuwa siku yenyewe ilikuwa ya gulio; siku maalum ya soko (uk.2). Soko lenyewe hufanywa kwenye kiwanja wazi ambapo watu hufanya biashara mbalimbali. Mwandishi

anasema kuwa, siku hiyo bidhaa huwa nyingi tofauti tofauti ambazo huuzwa kwa bei nafuu na rahisi. Kule sokoni kuna uuzaji wa nguo, nafaka, nyanya, kabeji, ndizi na bidhaa nyinginezo (uk. 3).

Kuwapo na siku ya gulio kunasawiri mandhari ya sokoni. Mandhari haya yanawasilisha maudhui ya biashara. Biashara zinazotekelezwa kwenye soko hili zinaonyesha kitega uchumi cha wanabiashara katika kuendeleza maisha yao. Soko lenyewe hutekelezwa kwenye uwanja wazi ili kuonyesha soko huria ambapo watu wana uhuru wa kuuza bidhaa zao watakavyo mradi wameelewana na wateja.

### 2.1.4 Mandhari ya usafiri

Heidegger (1982) anasema kuwa, binadamu huelewa mandhari kwa kuangalia uhusiano uliopo baina ya binadamu na mandhari yanayomzunguka. Katika usawiri wa mandhari ya usafiri, mwandishi anasema kuwa, soko lilikuwa mbali mno ndiyo maana Chandu aliamka mapema. Alikuwa amebeba kikapu cha maembe kichwani kama inavyoonyeshwa kwenye (uk. 4).

Chandu anatembea kwa kasi kuelekea sokoni. Kasi yake ilimfanya ajikwae. Kujikwaa huku kulisababisha kikapu kuegemea upande mmoja na kuangusha embe moja. Chandu hakufahamu kuwa embe moja lilianguka. Mwandishi anasawiri mhusika Bwaga aliyekuwa nyuma ya Chandu akielekea sokoni kuuza Bata. Bwaga anatumiwa na mwandishi kuendeleza safari ya asili ya mwembe ambapo baada ya kuokota embe, anashawishika na kulila embe hilo na kutupa mbegu ardhini.

Mwandishi amesawiri mandhari ya usafiri kuwasilisha maudhui ya umaskini kupitia safari ya Chandu kutembeakwa miguu hadi sokoni; angetumia gari au baiskeli kusafirisha maembe hadi sokoni kwa kuwa soko lilikuwa mbali. Hali hii inasaidia kuonyesha uhusiano wa wahusika;

Chandu na Bwaga na asili ya mwembe kwani binadamu huelewa mandhari kwa kuangalia uhusiano uliopo baina ya binadamu na mandhari yanayomzunguka (Heidegger, 1982).

### 2.1.5 Mandhari ya ufugaji

Mandhari haya yanaashiria ufugaji wa mifugo haswa ng'ombe. Mchungaji anawaongoza ng'ombe kuelekea malishoni huku akiwa ameshika fimbo kwenye mkono wa kushoto na redio kwenye bega la kulia.

Uzoefu wa binadamu kuhusu mandhari yanayomzunguka na shughuli zake za kijamii ni muhimu sana katika kuelewa mandhari na maana ya vitu na hali katika mandhari hayo (Smith na Thomasson, 2005).Ili kusaidia msomaji kuelewa mandhari anayosawiri, mwandishi anasema kuwa, mchungaji na ng'ombe wake waliikanyanga mbegu ya embe iliyotupwa na mhusika Bwaga na kuizika ardhini. Jambo hili linasawiri maudhui ya upanzi kwani, kitendo cha ng'ombe kuzika mbegu ardhini hata bila fahamu, kina umuhimu mkubwa kwa kuwa kinasaidia kupanda mbegu ya embe. Kitendo hiki kinadokeza maudhui ya sayansi kwani miti humea hata bila kupandwa lakini wanyama huchangia kukua kwa miti katika mandhari.

Vilevile, mchungaji anasikiliza redio huku ameiwekelea begani mkono wa kulia. Redio katika mandhari ya ufugaji imetumiwa kuendeleza maudhui ya sayansi na teknolojia kwani kupitia njia mbalimbali za mawasiliano kama vile matumizi ya redio mawasiliano yamerahisishwa na kuwezesha watu wengi kupata habari muhimu popote pale walipo.

### 2.1.6 Mandhari ya mvua

Mwandishi anasema kuwa, mvua ilinyesha mfululizo. Hali hii ilisababisha maji mengi ambayo yalisomba mchanga, changarawe, vijiti, majani, karatasi na kila aina ya uchafu na kuusafirisha sehemu nyingine. Mvua nyingi iliyonyesha ilisababisha mmomonyoko wa ardhi kwa kuwa rutuba iliyokuwa ardhini ilisombwa na kupelekwa kwingine. Maji haya ya mvua yalisafisha

mazingira na kuupa udongo uliokauka uhai. Maji yalipenya ndani ya mchanga na kukutana na mbegu ya embe (uk. 8). Mandhari ya mvua yamesawiriwa kuwasilisha maudhui ya mabadiliko ya hali ya anga na mazingira kwa ujumla ambapo mbegu ilikuwa mche.

### 2.1.7 Mandhari ya ukuaji wa mimea

Finominolojia hujihusisha na kuchunguza vitu na hali katika mandhari hasilia (Merleau, 2012). Katika muktadha huu, mwandishi anasema kuwa, beberu alikula majani yote ya mche. Aidha, baada ya muda, ule mche uliobaki kishina unachipua majani mengine. Vipepeo wanatua pale na baada ya kutaga mayai wanaenda zao. Mayai yale yanaagua na kuwa viwavi ambao wanayala yale majani takriban nusu ya mwembe huo. Baadaye ndege waliotua mtini wanawadona na kuwala. Kitendo hiki kinasaidia kuondoa mojawapo wa changamoto za ukuaji wa mimea.

Mandhari ya ukuaji yanaonyesha changamoto ambazo mche unapitia. Aidha, mwembe una matumaini ya kuchipua majani tena na tena. Hali hii inatuonyesha kuwa katika maisha kuna changamoto si haba. Mandhari haya yamesawiriwa kuendeleza maudhui ya ukulima na kubainisha changamoto za ukulima.

### 2.1.8 Mandhari ya uharibifu wa mazingira

Wapita njia wanauchoma mzinga wa nyingu na kuwaangamiza kwa sababu walikuwa wanawasumbua wapita njia. Hata hivyo, tawi moja la mwembe liliangamia. Mwandishi anasema kuwa, majani meusi yalianguka chini. Vilevile, kuna ndege aliyekuwa na tunda mdomoni. Mbegu ya tunda hilo lilianguka kwenye jani. Kimelea kikaanza kumea na kuchoma ganda la mwembe huo.

Katika msimu huo wa masika, radi, umeme na ngurumo zilishambulia msitu, milima na mabonde (uk. 17). Umeme ulipiga sehemu kubwa ya mwembe na kuangamiza kimelea kabisa. Palitokea mtema kuni akakata matawi na shina la mwembe.

Mandhari haya yanaonyesha jinsi shughuli za binadamu zinavyoathiri mazingira na kuyaharibu. Binadamu wanachoma mzinga wa nyigu – tendo ambalo linaangamiza nyingu na tawi moja la mwembe. Vilevile, mtema kuni anakata mwembe ili kupata kuni za kupikia. Japo ananufaika hatunzi mazingira kwa kupanda miche mingine.

### 2.1.9 Mandhari ya mjini

Kuna majengo ya ghorofa ambayo yanadhihirisha kuwa lile ni jiji. Vilevile, kuna mabasi na magari mengine yanayoonyesha mandhari mapya ya usafiri na kupitisha maudhui ya maendeleo ya kiteknolojia. Mandhari haya yamesawiriwa kuonyesha mpito wa wakati na mabadiliko ya soko hili.

Mzee Chandu alipoketi chini ya mwembe akibarizi, mwembe unamtambua "hakika huyu ndiye Chandu!" (uk. 22). Chandu naye baada ya kuangushiwa embe na mwembe anasema kuwa, siku hiyo ilikuwa ni Alhamisi ya miaka mingi kupita na yenye kuzunguka kama mduara (uk. 23). Mandhari haya yanaonyesha maudhui ya maendeleo na mabadiliko. Chandu anapata kuona mabadiliko na maendeleo katika eneo hili. Masoko makuu kadhaa yalikuwa yamefunguliwa katika mji wao alipokuwa kijana mdogo na sasa amezeeka.

Mwandishi wa *Embe Tamu* amesawiri aina mbalimbali za mandhari kama vile mandhari ya; sokoni, usafiri, ufugaji, miongoni mwa mengineyo. Mandhari haya yamesawiriwa kuwasilisha maudhui kama vile; sayansi na teknolojia, kazi na biashara, ukulima na changamoto za ukulima na maudhui mengineyo.

## 2.2 Mandhari katika *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005)

*Siku ya Wajinga* ni mojawapo wa vitabu teule vya kutumika katika utafiti. Kiliandikwa na Clara Momanyi mwaka wa 2005. Kitabu hiki kilitumiwa kuchunguza aina za mandhari yaliyosawiriwa na mwandishi ili kusaidia kutimiza malengo ya utafiti.

### 2.2.1 Muhtasari wa hadithi ya *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005)

Zito anasoma katika shule ya msingi ya Kambini. Darasani Zito anasumbua walimu kwa ujinga wake. Anadanganya wanafunzi kuwa wametumwa kuokota mawe katika mtambo wa reli ambapo gari la moshi lilipita. Alipoulizwa alisema ilikuwa siku ya wajinga! Utundu wake na kutenda matendo ya kijinga yanamfanya kuhamishiwa shule ya kurekebishia tabia iliyoitwa Hamio ambapo anapeleka ujeuri na ujinga wake. Mwishowe, anabadili tabia na kuacha tabia ya ujinga na kurejea shule ya msingi ya Kambini na kumalizia masomo yake. Mwandishi anatumia safari ya kubadilika kitabia kwa mhusika Zito kusawiri aina mbalimbali za mandhari ili kuwasilisha maudhui mbalimbali.

### 2.2.2 Mandhari ya nyumbani

Sura ya "Zito" ina mandhari ya nyumbani. Hapa ndipo tunapatana na Sadiki; ambaye ni mvulana na Zena; dadake Sadiki. Hawa wawili walikuwa pacha ambao walishirikiana kwa kila jambo. Smith (2013) anasema kuwa, vitu vyote katika ulimwengu hupata maana kutokana na jinsi vinavyoonekana na binadamu. Pale nyumbani Sadiki akisafisha vyombo naye Zena anafagia nyumba yao. Wazazi wao waliwafundisha kupalilia mimea, kuvuna, kukama ng'ombe na kuwachunga malishoni pamoja na kufua nguo. Sadiki na Zena wako pale jikoni wakifanya kazi tofauti. Jiko hili ni la kisasa kama linavyoonyeshwa kwenye uk. 8.

Mandhari haya yanaonyesha kuwa familia hii ilienzi kilimo na ufungaji wa mifungo na kusaidia kuwasilisha maudhui ya kilimo na ufugaji. Jiko na vyombo pale jikoni vinaonyesha kuwa familia hii ina uwezo wa kiwango cha wastani kiuchumi. Hali inayosaidia kusawiri maudhui ya utabaka.

Finominolojia huunda mkusanyiko mpana wa mandhari yanayomzunguka binadamu (Merleau, 2012). Zito alipofika nyumbani, anaagizwa na mamake amkamate jogoo ili atengeneze kitoweo siku hiyo. Zito anaamua kumkimbiza na kupita nyumba za majirani walioshangazwa na mbio

hizo za binadamu na kuku. Kauli hii inatusawiria mandhari ya nyumbani kwa Zito na ya nyumbani kwa mzee Lombo ambaye ni jirani wa akina Zito.

Babake Zito alirauka kila siku kupeleka mifugo malishoni na mamake kwenda shambani na kuwakama mifugo wao wakirudi jioni. Naye Zito alikuwa anawafungia mifugo. Siku moja Zito anatimua mbio na fahali mmoja huku akiwa amemkamata mkia. Watu wanastaajabishwa na jambo hili walililiona kama sinema.

Kasi ya fahali huyu zinamzidi Zito na anaanguka chini. Alipata majeraha usoni na kuzirahi. Marafiki wa Zito waliwafahamisha wazazi wake. Mtu mmoja alirarua shati la Zito na kumfunga kichwani ili kuzuia damu kuchiriza.

Mandhari haya ya nyumbani yanatuonyesha maudhui ya kazi. Wazazi wa Zito walifanya kazi kwa bidii, ndiyo maana kila asubuhi walirauka kutekeleza wajibu wao. Vilevile, mandhari haya yanasawiri maudhui ya utovu wa nidhamu na utundu kwa kuwa vituko vyote vya Zito vinaashiria utundu wake.

### 2.2.3 Mandhari ya shuleni

Kwa mujibu wa Mohanty (2011), maana ya vitu na hali katika dunia hupatikana kupitia hali tofauti za uzoefu wa mtu kuhusu vitu hivyo na kutenda shughuli mbalimbali za kijamii. Sadiki, Zena na Zito wanasomea katika shule ya msingi ya Kambini na walikuwa darasa la saba (uk. 7). Mwandishi anasema kuwa, Sadiki na Zena walifanya mazoezi ya Hesabu, Kiingereza, Sayansi na masomo mengineyo, kuonyesha uzoefu na ufahamu wao kuhusu masomo hayo na pia kuonyesha wanatia bidii katika masomo.

Mandhari ya shuleni pia yanaonyeshwa wakati Zito anapopekua nyaraka na karatasi za mwalimu Petro. Wakati huo wanafunzi wote wako uwanjani kutazama mchezo wa kandanda. Alinakili majibu yote ya zoezi walilopewa na mwalimu Petro.

Mandhari haya yanakuza maudhui ya wizi na ulaghai. Mandhari haya pia yanaonyesha madhara ya wizi na ulaghai kwa kuwa Zito anaadhibiwa kwa kupewa adhabu ya kufyeka nyasi zote zilizokuwa kwenye uwanja wa mpira.

Mandhari haya ya shuleni yametumiwa kuwasilisha maudhui ya kielimu. Pia yanaonyesha kazi ambazo wale wanazingatia masomo watafanya yaani; udaktari, ualimu, wakili na kadhalika. Maelezo haya yanasaidia kuwasilisha maudhui ya utaaluma.

Vilevile, kuna mandhari ya shuleni katika shule ya Hamio. Hapa wanafunzi wote waliishi kwenye bweni chini ya ulinzi mkali. Zaidi ya hayo, kulikuwa na ratiba iliyoonyesha kazi ambazo kila mwanafunzi angetekeleza kwa juma zima (uk. 51).

Mwandishi amesawiri mandhari ya shuleni kuendeleza na kukuza maudhui ya elimu na umuhimu wa kuzingatia nidhamu na kutii sheria katika shule na maisha kwa jumla.

Kila binadamu huwa na ufahamu wa dhana tofauti tofauti katika mandhari kupitia kuona, kufikiria, kuhisi na kutenda shughuli za jamii (Smith, 2013). Sura ya saba ya riwaya hii ni "Maisha Mapya". Sura hii inasimuliwa katika mandhari pana ya shuleni. Kuna mandhari ya shule ya Hamio. Zito anadhihirisha mabadiliko ya kifaurongo yaani mabadiliko yasiyo ya kweli. Mwandishi anasema kuwa, Zito alikuwa na mpango wa kutoroka shuleni. Zito anatoroka kwa kuruka ua wa shule na hatimaye kukamatwa na mlinzi. Zito anafikishwa mbele ya walimu waliompa mawaidha. Alishauriwa kuwa, akitaka maisha mema atie bidii masomoni na ajiepushe na utundu kwani ameshuhudia madhara ya utovu wa nidhamu katika maisha.

Mandhari haya ya Shule ya Hamio yanatuonyesha maudhui ya mabadiliko. Zito anabadilika na kufuata masharti ya walimu na kuwaomba mawaidha. Mwandishi anasema kuwa;

> "Baada ya muda usio mrefu, Zito alikuwa kijana tofauti kabisa. Alikuwa hodari katika kila kazi aliyofundishwa, hasa useremala. Aliranda mbao na kutengeneza vifaa

vilivyowafurahisha walimu wake. Mwishoni mwa mwaka wa pili katika shule hii, alipewa cheti cha kufuzu kwa nidhamu bora" (uk. 61).

Kuna mandhari ya shule ya Kambini. Hapa Zito anarudi tena darasa la saba ambapo wenzake walikuwa wamepiga hatua na kujiunga na kidato cha kwanza. Maandishi aliyoandika dawatini yake yalimhuzunisha na kuamua kuyafuta na kuandika, 'ukitaka cha mvunguni, sharti uiname'. Mandhari haya yanatuonyesha maudhui ya majuto. Zito anajutia vitendo vyake vya kijinga hapo awali. Vivyo hivyo, kuna maudhui ya mabadiliko ndio maana Zito anayafuta maandishi yaliyoandikwa kwa dawati na kuandika mengine mapya. Zito anamwambia mwalimu Petro kuwa, atafanya bidii na kuondoa kabisa siku ya wajinga akilini mwake. Mwalimu Petro anampongeza kwa azimio hilo nzuri.

### 2.2.4 Mandhari ya darasani

Mwandishi anasema kuwa, Zito alichukia somo la Hesabu zaidi kuliko masomo yale mengine kama tunavyoona katika sura ya pili. Mwalimu wa Hesabu, Petro alikuwa akizunguka darasani akiwaonyesha jinsi ya kufanya Hesabu. Katika mandhari ya darasani kuna dawati, viti na wanafunzi. Kwa kuwa mwalimu hakuwa darasani, Zito anazunguka humo akiwaonyesha wanafunzi wenzake alama alizopata. Mandhari haya yametumika kuendeleza maudhui ya elimu.

Kwa mujibu wa Mohanty (2011), ufahamu wa mandhari yanayomzunguka binadamu na maana ya vitu katika mandhari hayo hutokana na uzoefu na ufahamu wa mandhari husika. Mandhari ya darasani yanaonyesha kuwa, walimu wana uzoefu wa mandhari yanayowazunguka kwani wanatumia mitindo mbalimbali ili kuhahikisha kuwa wanafunzi wao wanaelewa kile wanachowafundisha. Mtindo wa mwalimu Petro uliwachangamsha wanafunzi wengi na kuchangia kumpenda na hata kulipenda somo lake.

Mandhari ya darasani yametumiwa na mwandishi kutoa maudhui ya ubaguzi wa kijinsia ambapo Zito licha ya kuwa haelewi hesabu anakataa katakata kuonyeshwa na Zena ambaye ni msichana. Anasema kuwa, kuonyeshwa hesabu na msichana ni madharau makubwa (uk. 13). Mandhari haya yametumika kudhihirisha taasubi ya kiume katika jamii hii. Aidha, Zito anapopata sufuri na sufuri hiyo kutomelewa masikio, macho, pua na midomo wanafunzi wengine walimcheka. Sadiki hambagui Zito kwa misingi ya kuwa ni mjinga. Kauli hii imetumika kuendeleza maudhui ya ubaguzi.

'Sauti ya Chura' ndiyo anwani ya sura ya tatu. Sura hii ina mandhari ya darasani. Mwalimu Rukia ambaye wanafunzi walimwita mwalimu Nanhino kwa sababu ya kuzoea kuwaita wanafunzi wake nanhino, nanhuyu au nanhii (uk. 20), aliwaongoza wanafunzi kuimba nyimbo ili kutambua na kukuza vipawa vyao vya uimbaji. Sauti ya mwalimu huyu ilikuwa nzuri kama kinanda. Wanafunzi wengine walijaribu kuiga sauti hiyo bila mafanikio. Mwalimu Rukia alikuwa akiwafundisha wanafunzi wa darasa la saba wimbo mpya ulioitwa '*Safari ya Bamba'* (uk. 22).

Mandhari haya ya darasani yanaonyesha maudhui ya ukuzaji talanta na ufundishaji. Mwalimu Rukia anatumia muda mwingi ili kuwafundisha wanafunzi wimbo mpya. Hatimaye, anabaini kuwa Zito ndiye aliyekuwa na sauti kama ya chura.

Vilevile, mwalimu wa somo la Kiswahili, Bwana Mfaki (Mwalimu mkuu), anawafunza wanafunzi kwa kuwapa nafasi ya kutunga hadithi zao na kuwasimulia wengine darasani. Ilikuwa zamu ya Zito kusimulia hadithi yake 'Akili ni Mali' (uk. 24). Zito alisoma hadithi yake kutoka kwa karatasi kuonyesha maudhui ya ukuzaji talanta kwa wanafunzi kupitia ubunifu wa utunzi.

### 2.2.5 Mandhari ya michezo

Timu ya shule ya Kambini ilikuwa ikifanya mazoezi na timu jirani katika mchezo wa kandanda. Wanafunzi wote walienda uwanjani kushuhudia mchezo huo. Vilevile, shule ya Kambini ilisifika sana kwa mchezo huo kwasababu ilikuwa imenyakua kikombe cha kandanda wilayani (uk. 30). Mwandishi anatuchorea mandhari haya kutuonyesha umuhimu wa michezo kwa vijana. Vilevile, michezo ya wilaya ya kandanda baina ya shule za msingi ilifanyika katika shule ya Mkomani iliyokuwa umbali wa kilomita sita kutoka shule ya Kambini. Wanafunzi wakitoka michezoni hawakufuata njia halisi, walifuata njia ya mkato iliyopita kando ya mto (uk. 30).

Mandhari haya ya michezo yanaonyesha kuwa kulikuwa na ushabiki mkubwa wa mpira wa kandanda ndio maana wanafunzi wote wa shule ya Kambini na mashabiki wengine walienda kushuhudia michezo hiyo. Tunabaini kuwa timu ya kandanda ya shule ya Kambini ilikuwa hodari kwa sababu iliweza kuimbuka bingwa katika wilaya hiyo. Mandhari haya yanasaidia kuwasilisha maudhui ya michezo na kusisitiza umuhimu wa michezo kwa vijana kwani vijana wanapocheza huweza kuburudika na kuendeleza vipawa vyao.

### 2.2.6 Mandhari ya makaburini

Binadamu haelewi maana ya vitu na mazingira yanayomzunguka kwa kuangazia sehemu fulani ya mazingira bali hupata maana ya vitu kwa kuangalia uhusiano uliopo baina ya binadamu na mazingira yanayomzunguka na jinsi vitu vilivyo katika mazingira hayo (Heidegger, 1982). Mwandishi anasema;

> “Kando ya mto huu kulikuwa na makaburi yaliyojengwa na misalaba nyeupe iliyong’aa wakati wa jua la kichwa. Kwa mbali misalaba hiyo ilioneka kama watu walionyoosha mikono yao wakisali” (uk. 30 - 31).

Mwandishi amesawiri mandhari ya makaburini ili kuwasilisha maudhui ya vifo kwani pana uhusiano wa maisha ya binadamu na vifo kwa sababu binadamu huishi na mwishowe anafariki. Mwandishi anatumia mandhari hayo kuonyesha kuwa baada ya kufariki binadamu huzikwa makaburini.

### 2.2.7 Mandhari ya hospitali

Wazazi wa Zito na watu wengine walisaidiana kumpeleka Zito hospitalini kwani alikuwa ameumia sana baada ya kuanguka alipokuwa akimkimbiza fahali. Zito alikuwa amezirahi hadi siku ya pili. Mwalimu Petro na wanafunzi wengine walimtembelea pale hospitalini (uk. 39).

Mandhari ya hospitali yanatuonyesha maudhui ya ushirikiano kwa kuwa watu wengine waliwasaidia wazazi wa Zito kumbeba hadi hospitalini.

Riwaya ya *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005) imesawiri aina mbalimbali za mandhari kama vile; nyumbani, shuleni, makaburini na aina nyingine nyingi. Aina hizi za mandhari zimechangia kuwasilisha maudhui kama vile; elimu, michezo na mengine mengi.

## 2.3 Mandhari katika *Njiapanda* (Amana, 2008)

*Njiapanda* ni kitabu kinacholenga wanafunzi wa darasa la nane katika shule za msingi ili kuendeleza na kukuza uwezo wao wa kusoma. Kitabu hiki kiliandikwa na Boukheit Amana mwaka wa 2008. Kitabu hiki kilitumiwa kuchunguza usawiri wa aina mbalimbali za mandhari na kusaidia kutimiza baadhi ya malengo ya utafiti.

### 2.3.1 Muhtasari wa hadithi ya *Njiapanda* (Amana, 2008)

Mwandishi katika *Njiapanda* amesawiri mandhari ya kidhahania kwa wingi ili kuwasilisha ujumbe wake. Hadithi inapoanza anasawiri wasafiri wa dini mbili; Waislamu na Wakristo wanaoenda katika shughuli za mazishi. Wanaoenda kuzikwa mmoja ni kijana na yule mwingine ni mama mzee. Pale wanapokutania, msichana mjamzito anaanguka katikati ya barabara na

kukatiza usafiri. Mwandishi anatumia fursa hii kuanzisha dayalojia kati ya maiti hawa wawili na kijusi. Kijana marehemu anasimulia kilichomsababishia maafa naye mama mzee anajaribu kumwonya kijusi asiige tabia za marehemu kijana, kwani huenda zikamletea maafa afikapo ulimwenguni. Baadaye, mwandishi anasawiri mandhari ya ulezi ambapo anaanzisha mazungumzo baina ya msichana mjamzito ambaye anaelezea kijusi asili yake yaani baba yake na ukoo wake. Mwishowe, mwandishi anakamilisha masimulizi kwa kuonyesha jinsi maafisa wa kimatibabu wanavyojitahidi kuokoa maisha ya msichana mjamzito na kijusi. Mwandishi amesawiri mandhari mbalimbali ili kuwasilisha ujumbe wake.

### 2.3.2 Mandhari ya barabarani

Smith (2013) anasema kuwa, kila binadamu huwa na uzoefu na ufahamu wa dhana tofauti tofauti katika mandhari. Uzoefu na ufahamu huu wa mandhari humsaidia binadamu kutenda shughuli tofauti za kijamii. Hadithi inapoanza tunakutana na mandhari ya barabara ya *Grand Coalition*. Barabara hii ni njiapanda. Pale barabarani kulikuwa na Waislamu waliobeba jeneza na msafara wa magari ya Wakristo waliokuwa pia wanaomboleza mmoja wao wakienda mazishi. Kuna vijana Waislamu waliobeba jeneza huku wakifuatwa na wazee. Hali hii inaonyesha kuwa wana uzoefu na ufahamu wa dhana ya mazishi kama shughuli ya kijamii.

Upande wa pili wa barabara kulikuwa na msafara wa magari yaliyoangikwa tepe nyekundu. Kuna gari moja refu jeusi lililobeba jeneza (uk. 2).

Mwandishi anatuonyesha itikadi na imani za dini mbili tofauti. Waislamu na Wakristo walikuwa wanaomboleza na kupeleka wapendwa wao kwenda mazishini kulingana na desturi zao. Mandhari haya yanaashiria maudhui ya vifo.

Mlikuwa pia na msongamano wa watu waliosuburi wapite. Miongoni mwao ni mwanamke mjamzito.Vilevile, kulikuwa na taa zilizoashiria zamu ya gari kupita. Taa nyekundu zilipoashiria

magari yakasimama nawapita njia nao wakaanza kupita. Mwanamke mjamzito ndiye alikuwa mbele, ghafla akaanguka chini katikati ya barabara na kuzirai.

Wapita njia katika mandhari ya barabara ya *Grand Coalition* wametumiwa na mwandishi kuwasilisha maudhui ya usafiri. Kuwepo kwa taa barabarani zilizoongoza wapita njia na magari kunadokeza maudhui ya maendeleo ya sayansi na teknolojia ambapo taa zilipisha zamu ya watu au gari kupita bila kuhusisha binadamu.

### 2.3.3 Mandhari ya kidhahania

Mwanamke mjamzito anapozirahi, anaanza mazungumzo baina yake na kijusi kilichokuwa ndani ya kizazi chake wakati alipokuwa amelazwa kwenya kiti cha nyuma cha abiria. Mwanamke mjamzito alitaka kujua ni kwa nini kijusi chake kiliwafanya wasimame saa nzima pale njiapanda. Kijusi kinamweleza kilikuwa kinazungumza na wale maiti wawili waliokuwa wanapelekwa kuzikwa.

Mazungumzo haya ya kijusi, Bikizee (maiti ya Muislamu na mwanamke mzee) na Kijana (maiti ya Mkristo na ni mwanaume wa makamo) yanasawiri mandhari ya kidhahania. Mwandishi anatumia mandhari haya kuwasilisha maudhui ya ushauri nasaha kwa kuweka wahusika hawa katika mazungumzo ya kufikirika tu ili waweze kutangamana kimawazo na kutoa ushauri nasaha kwa kijusi kuhusu maisha ya duniani ambayo hatima yake ni mauti.

### 2.3.4 Mandhari ya shuleni

Kitendo cha wanafunzi kusababisha machafuko shuleni na kuchoma mabweni, madarasa, nyumba ya mwalimu mkuu na gari lake kinatumiwa na mwandishi kusawiri mandhari ya shuleni. Tukio hili ndilo linalosababisha maafa ya kijana huyu. Kijana anasema kuwa,“katika hali ya kuchoma, mlipuko wa bomu la petroli ya chupa ukanifikia na kuniunguza vibaya sana mwili mzima mpaka nikafia humo mimi pia” (uk. 7).

Kijana anasema kuwa, sababu zifuatazo ndizo zilizowachochea kusababisha michafuko na migomo shuleni; mtihani wa mwigo kuwa mgumu ilhali silabasi haijakamilishwa, uongozi wa kiimla shuleni, ukosefu wa demokrasia, ukosefu wa heshima, wanafunzi wawe na simu ya mkononi, DVD ndani ya basi za shule, tofauti za kizazi na kipindi cha maisha, wanyanyasaji, masomo yasiyojenga mustakabali wa wanafunzi kwa kutoa njia mwafaka za kukabiliana na mabadiliko ya sayansi, teknolojia, siasa na ukosefu wa kazi. Jambo hili linasababisha kukata tamaa kwa vijana na mwisho uchochezi wa walimu na wafanyikazi wa shule kwa sababu wanahisi kudhulumiwa. Mandhari haya yanasawiriwa kuwasilisha maudhui ya migomo shuleni na madhara ya migomo hiyo.

**2.3.5 Mandhari ya hospitali**

Finominolojia ni pana na hufikia kiwango cha kutoa maana ya vitu na hali katika mandhari kwa kuwa uzoefu wa binadamu humpa ufahamu wa mambo mengi katika akili yake zaidi ya anachoona na kusikia (Merleau, 2012).

Mwanamke mjamzito yuko kwenye machela ya magudurumu akipelekwa katika chumba cha dharura. Mama msaidizi anabaki na mpokezi akitoa stakabadhi ambazo zitawezesha kumtambulisha mgonjwa. Vilevile, anatafuta jamaa zake kwenye simu ya mwanamke mjamzito. Katika chumba cha dharura msichana mjamzito amewekewa mipira ya gesi ya oksijeni puani na kuwekewa dripu mkono mmoja. Mandhari ya hospitali yanachangia kuwasilisha maudhui kadha wa kadha.

Kwanza ni maudhui ya taaluma na kazi. Mwanamke mjamzito anapofikishwa hospitalini anashughulikiwa haraka iwezekanavyo na kupelekwa katika chumba cha dharura kwa kuwa hali yake ilikuwa ya dharura. Vilevile, mpokezi anaingiza kitambulisho na kubainisha kuwa alikuwa akihudumiwa hapo na hivyo kumpigia daktari wake simu. Aidha, maudhui ya maendeleo ya

sayansi na teknolojia yanaendelezwa kupitia kwa wasifu wa msichana mjamzito uliopatikana kwenye ngamizi.

Matumizi ya simu yanachangia maudhui ya mawasiliano, uwajibikaji na utaaluma. Mpokezi anawasiliana na daktari na pia mwanamke msaidizi anawasiliana na Lulu kumfahamisha hali ya mwanamke mjamzito.

Sehemu ya *"accidents and emergency"* inachangia kuwasilisha maudhui ya hali ya dharura kwa mgonjwa. Vilevile, inazua hisia mseto za kuwa lolote mbaya au nzuri laweza kutokea. Kukosekana kwa Bob, mpenzi wa Isabela kunadhihirisha usaliti wa kimapenzi na mapuuza. Urafiki wa Lulu na Isabela umetumiwa na mwandishi kuwasilisha maudhui ya urafiki.

Vilevile, kuna maudhui ya matibabu. Daktari alipofika walipigia wazazi wa Isabela simu na kupata idhini ya kufanya upasuaji. Hili ndilo lililokuwa suluhu kwa sababu kutokana na rekodi za Isabela za kliniki na hali aliyokuwa baada ya kupigwa picha ya skena.

Mwandishi anasema kuwa;

> "Akalazwa kwenye kitanda cha upasuaji. Mtaalamu wa nusukaputi akamdunga sindano ya kumpoteza fahamu. Msichama mjamzito hakuchukua sekunde thelathini, fahamu zake zikapaa kwenye ulimwengu mwengine …" (uk. 19).

**2.4 Hitimisho**

Sura hii ilishughulikia usawiri wa aina ya mandhari katika vitabu vitatu tofauti teule za fasihi andishi ya watoto. Ilionyesha jinsi waandishi walivyosawiri mandhari yanayochangia kuwasilisha ujumbe (maudhui). Vitabu hivi teule ni; *Embe Tamu* (Njogu, 2003), *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005) na *Njiapanda* (Amana, 2005).

Mihimili mbalimbali ya nadharia ya finominolojia ilitumika kuchunguza aina mbalimbali za mandhari. Mandhari ambayo yalitambulishwa ni kama vile mandhari ya; nyumbani, hospitali,

sokoni, barabarani na shuleni. Mandhari haya yanadokeza maudhui ya; elimu, usafiri, sayansi na teknolojia, mapenzi, urafiki, biashara na kazi.

Sura inayofuata, ilichunguza jinsi mandhari yalichangia sifa za wahusika katika; *Embe Tamu* (Njogu, 2003), *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005) na *Njiapanda* (Amana, 2008).

## SURA YA TATU

## SIFA ZA WAHUSIKA KUTOKANA NA MANDHARI

### 3.0 Utangulizi

Sura hii ilichunguza jinsi mandhari yalivyochangia sifa za wahusika katika fasihi ya watoto. Nadharia ya finominolijia ya Husserl (1900) imesaidia kuchunguza sifa za wahusika kutokana na mandhari. Kwa mujibu wa Marleau (2012), binadamu hupata ufahamu wa mandhari yanayomzunguka yaani anavyojiona na kuona vitu katika mandhari kutokana na kutenda matendo mbalimbali pamoja na kuingiliana na wanajamii katika shughuli mbalimbali za kijamii. Naye Heidegger (1982) anadai kuwa, binadamu hupata maana ya vitu kwa kuangalia uhusiano uliopo baina ya binadamu na mandhari yanayowazunguka na jinsi vitu vilivyo katika mandhari hayo.

Smith (2013) anasisitiza kuwa, kila binadamu huwa na uzoefu na ufahamu wa dhana tofauti tofauti katika mandhari kupitia kuona, kufikiria, kuhisi na kutenda shughuli mbalimbali za kijamii. Uzoefu na ufahamu huu wa mandhari yanayomzunguka binadamu huwa na sifa za kipekee kwa binadamu kwa kuwa binadamu ataishi nazo na kuzitumia katika shughuli tofauti za kijamii.

Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (2008), wahusika ni viumbe wa sanaa wanaobuniwa kutokana na mazingira ya msanii yanayoweza kuwa ya; kubuni, kijiografia, kihistoria, kijamii, kitamaduni au ya kisiasa. Wahusika katika kazi ya sanaa hurejelea na huakisi sifa na tabia za binadamu katika jamii husika.

Wahusika ni sehemu muhimu ya fani (Msokile, 1999; Njogu na Chimerah, 2008). Bal (1997) anaeleza kuwa, wahusika hushabihiana na watu kwa kuwa fasihi huandikwa kwa ajili ya watu na kwa hivyo, huwahusu watu hao. Kimsingi, wahusika si watu halisi, bali ni matokeo ya ubunifu wa mwandishi ili kuakisi masuala kadhaa ya kijamii ambayo mwandishi ameyakusudia.

Sura hii, ilijihusisha na uchunguzi wa sifa za wahusika kutokana na mandhari yaliyosawiriwa na waandishi wa vitabu teule vya fasihi andishi ya watoto. Vitabu teule vilivyotumika katika uchunguzi ni pamoja na; *Embe Tamu* (Njogu, 2003), *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005) na *Njiapanda* (Amana, 2008). Aina za mandhari katika kila kitabu zilichunguzwa ili kubaini sifa za wahusika zinazotokana na mandhari hayo.

### 3.1 Sifa za wahusika kutokana na mandhari katika *Embe Tamu* (Njogu, 2003)

Kama ilivyotangulizwa katika sura ya pili, *Embe Tamu* ni kitabu cha ziada kinachonuiwa kuendeleza msingi wa kusoma na kukuza uwezo wa kusoma wa wanafunzi wa darasa la tano katika shule za msingi. Vilevile, aina mbalimbali za mandhari katika *Embe Tamu* zilibainishwa kama vile; mandhari ya ghala, mandhari ya sokoni miongoni mwa mandhari mengineyo.. Mwandishi ametumia wahusika wanaotenda shughuli mbalimbali za kijamii wakiingiliana katika mandhari mbalimbali. Mwandishi wa *Embe Tamu* amebuni wahusika ambao ni viumbe vinavyopatikana ulimwenguni kama vile; binadamu, Wanyama, mimea, mvua, mbegu na wengineo. Wahusika hawa wanapata sifa mbalimbali ambazo ni chanya na baadhi ya nyinginezo zikawa hasi katika mandhari mbalimbali.

#### 3.1.1 Sifa za Chandu na familia yake

Uzoefu na ufahamu wa binadamu kuhusu mandhari yanayomzunguka na shughuli zake za kijamii ni muhimu sana katika kuelewa mandhari na maana ya vitu na hali katika mandhari hayo (Merleau, 2012). Katika mandhari ya ghala, mwandishi amesawiri mhusika Chandu akiwa karibu na ghala lililokuwa nyumbani kwao. Haya ni mandhari ambayo Chandu ameyazoea na kuyafahamu vizuri. Chandu anajitayarisha kwa shughuli za siku hiyo. Mandhari haya ya ghala yanamsaidia msomaji kuelewa vizuri mandhari yanayomzunguka kwa kujinasibisha na mhusika Chandu. Mandhari ya ghala yanawapa wahusika sifa kadhaa.

**(i) Wenye ushirikiano na uwajibikaji**

Chandu na ndugu zake walishirikiana vilivyo kwani, walikuwa na ratiba ya kupeleka maembe sokoni. Hakuna aliyekosa kupeleka maembe sokoni wakati wa zamu yake. Ratiba hiyo iliwafanya waweze kuwajibika. Chandu anasema kuwa, siku hiyo ilikuwa zamu yake ya kupeleka maembe sokoni kwani ndugu zake watatu walikuwa wamemtangulia kwenda sokoni wiki tatu zilizopita (uk. 2).

**(ii) Wenye bidii**

Familia ya kina Chandu walikuwa wanatia bidii katika shughuli za ukulima. Jitihada zao zimewafanya wawe na mavuno ya kutosha kila msimu. Chandu alisimama karibu na ghala. Ghala yenyewe imejaa magunia yaliyojazwa maembe (uk. 1).

### 3.1.2 Sifa za wafanyibiashara na Chandu

Mwandishi amesawiri mandhari ya sokoni kuonyesha wahusika wafanyibiashara wakiwa sokoni wakiendeleza shughuli mbalimbali za kibiashara kama vile; kuuza maembe, kabeji, ndizi na bidhaa nyinginezo. Kwa kusoma mandhari ya sokoni, msomaji anaweza kuelewa mandhari hayo vizuri katika maisha halisi kwani atajinasibisha na wahusika katika mandhari aliyosawiriwa. Mandhari ya sokoni yamechangia sifa kadhaa za wahusika.

**(i) Ni wenye bidii kazini**

Siku ya gulio yaani siku maalum ya soko, wafanyibiashara tofauti walikuwa wanajishughulisha na uuzaji wa bidhaa zao kwa bidii. Mwandishi anasema kuwa, siku hiyo bidhaa huwa nyingi na tofauti. Bidhaa hizo huuzwa kwa bei nafuu na rahisi. Pia, kila mmoja ametia bidii na kuleta bidhaa sokoni na kuzipanga vizuri (uk. 3).

**(ii) Wenye amani**

Pale sokoni, kila mmoja anaonekana kuendeleza shughuli zake pasipo kuingiliwa na yeyote kwa kuwa wanauza bidhaa zao watakavyo mradi wameelewana na wateja. Hata mzee Chandu anapoenda sokoni miaka mingi baadaye, anabarizi pale mjini bila wasiwasi (uk. 22).

### 3.1.3 Sifa za Chandu na Bwaga

Kwa mujibu wa Heidegger (1982) binadamu na matendo yao huwa katika dunia kila wakati. Anasisitiza kuwa, kutenda shughuli mbalimbali za kijamii huweza kumsaidia binadamu kujielewa na kuyaelewa mandhari yanayomzunguka. Mwandishi amesawiri mandhari ya usafiri na kuweka wahusika Chandu na Bwaga katika safari kuelekea sokoni. Mandhari haya ya safari yanawapa wahusika hawa sifa kadha wa kadha.

**(i) Ni wenye bidii**

Chandu anabeba kikapu kilichojaa maembe kichwani akielekea sokoni. Chandu anajibidiisha kubeba kikapu kilichojaa maembe kichwani na tunaarifiwa kuwa mwendo wake ulikuwa wa kasi (uk. 2)

**(ii) Mwenye mapuuza**

Baada ya Chandu kujikwaa na kikapu chake kuegemea kidogo upande mmoja, hakuwajibika kuangalia kama kuna embe lililoanguka, anaendelea na safari tu. Hali hii inaonyesha kutowajibika (uk. 4).

**(iii) Wenye tamaa**

Bwaga anaokota embe lililoangushwa na Chandu. Uzuri wa embe lile ulimpa tamaa ambayo ilimfanya alile kwa pupa. Anasema,

> “Sasa nilifanye nini embe hili? Acha wee! Embe zuri lenye kupendeza!.......linafaa kwa kiamshakinywa” (uk. 6).

Bwaga alitamani sana kulila lile embe, msukumo huu ulimfanya kulila lile embe bila kujali hasara ambayo Chandu angepata.

### 3.1.4 Sifa za mchungaji na ng'ombe

Shughuli za kijamii ni muhimu sana katika uzoefu na ufahamu wa binadamu kuhusu mandhari yanayomzunguka (Heidegger, 1982). Mwandishi amesawiri mandhari ya ufugaji kuonyesha mchungaji akiwa katika shughuli ya uchungaji na kupitia shughuli hii mhusika anapata sifa mbalimbali.

**(i) Mtambuzi**

Kando na kuwachunga ng'ombe, mchungaji ana redio mkononi anayosikiliza kuonyesha kuwa anatambua njia za mawasiliano na umuhimu wa kupokea habari popote alipo.

**(ii) Mwenye kuwajibika**

Mchungaji anawajibika katika kazi yake kwani anawaongoza ng'ombe wake vizuri akiwapeleka malishoni. Mchungaji aliwaongoza ng'ombe kuwapeleka malishoni kuonyesha aliwajibikia kazi yake (uk. 7).

**(iii) Wenye utulivu**

Ng'ombe wanamfuata mchungaji bila kusumbua. Suala hili linaonyesha kuwa ng'ombe hawa ni watulivu kwani hawajaweza kukimbia huku na kule au kuingia mashambani mwa watu, wanamfuata mchungaji hadi malishoni tu.

### 3.1.5 Sifa za mvua na mbegu

Binadamu huwa na uzoefu na ufahamu wa dhana tofauti tofauti katika mandhari kupitia; kuona, kufikiria, kuhisi miongoni mwa mengine (Smith, 2013). Kitendo cha mvua kunyesha ni dhana muhimu katika maisha ya binadamu. Kupitia kunyesha kwa mvua msomaji anapata kuelewa umuhimu wa mvua katika mandhari na maisha kwa jumla. Mwandishi amesawiri mandhari ya

mvua kwa kuwahusisha wahusika wa kubuni kama vile; mvua, mbegu na wengine. Wahusika hawa wamepewa uhai na uwezo wa kuendeleza vitushi katika hadithi na kupata sifa zifuatazo;

**(i) Ni wenye matumaini**

Baada ya mbegu kujipenyeza ardhini, mvua ilinyesha mfululizo. Maji ya mvua yalipenya ndani ya udongo na kuupa uhai kwa kuwa ulikuwa mkavu. Dhana hii inaonyesha kuwa mhusika Mvua alimpa udongo matumaini. Vilevile, maji hayo ya mvua, udongo najua wanasaidia kupea mbegu la mwembe tumaini la kuweza kukua na kujiimarisha. Mwembe unasema,

> "Ewaa… Huu ndio wakati unaofaa. Nitakua hivi karibuni na nitajiimarisha!" (uk. 9).

**(ii) Wenye ushirikiano**

Mche wa mwembe ulitokea na kukaribishwa na mwangaza mzuri wa jua. Kuchipuka kwa mche kumesababishwa na ushirikiano usio wa kawaida kwa kuwa kati ya wahusika wote hakuna aliyejua kwamba ana manufaa kwa mwingine. Chandu anaangusha embe linaloliwa na Bwaga na kutupa mbegu mchangani (uk. 3). Baadaye, ng'ombe na mchungaji wanasukuma mbegu ile mchangani. Mvua inanyesha na kunywesha mbegu maji. Miale ya jua inapatia mbegu joto na kuifanya kuota mizizi (uk. 9). Mche mdogo unatokea na kuanza kuota majani na kuwa mwembe (uk. 10). Maelezo haya yanaonyesha kuwa miti humea bila kupandwa lakini kupitia ushirikiano usio wazi wa binadamu, wanyama, mvua, udongo, jua na vigezo vingine huchangia kukua kwa miti.

### 3.1.6 Sifa za wapita njia, beberu na mwembe

Finominolijia hujihusisha na kuchunguza vitu na hali katika mandhari halisia (Merleau, 2012). Mimea hupatikana katika mandhari na katika ukuaji wake huathiriwa na changamoto nyingi kama vile; kuliwa na beberu, pamoja na kukatwa kama kuni na kuchomwa. Mwandishi amesawiri mandhari ya ukuaji wa mimea ili kuwasilisha vitu na hali katika mandhari halisia

(Merleau, 2012). Msomaji anapata kujinasibisha na hali hii na kuweza kuelewa mandhari halisi yanayomzunguka. Katika mandhari haya wahusika wanapata sifa chanya na hasi kutegemea muktadha.

**(i) Ni waharibifu**

Wapita njia wanachoma nyuki bila kujali hali ya mwembe. Huu ni uharibifu mkubwa wa mandhari kwani walipochoma nyigu waliathiri matawi na majani ya mwembe na pia kuwaangamiza nyigu.Vilevile, mtema kuni anatema mwembe pasipokujali hatima ya mwembe.

**(ii) Ni katili**

Mche uliendelea kukua vizuri hadi pale beberu mmoja alipoyakata majani na kuyala bila huruma. Mche huo ukabaki kishina kilichokuwa na uchungu mwingi. Baada ya muda, mche ukashamiri tena na kuwakaribisha vipepeo waliotaga mayai na kuagua viwavi. Viwavi hawa wakala majani ya mwembe huo. Viwavi walipoulizwa na mwembe mbona hawakuwa na huruma hawakujali hisia za mwembe.

> "Mbona nyinyi hamna huruma? Hii ndiyo jaza yenu ya ihsani?" (uk. 12).

Hali hii inaonyesha ukatili kwa kuwa viwavi waliyala nusu ya majani yote ya mwembe hivyo, kupunguza nguvu zake.

**(iii) Ni wakarimu**

Mwembe unawakaribisha vipepeo bila tashwishi (uk. 11). Vilevile, mwembe unaruhusu nyigu kuishi hata baada ya kudhulumiwa na vipepeo (uk. 13). Kauli hizi zinadhihirisha ukarimu wa mwembe.

**(iv) Ni wenye matumaini**

Hata baada ya Mwembe kudhulumiwa na beberu anajipa moyo kwa kusema kuwa atakua polepole na kuwa mwembe imara.

"si hoja. Nitakua polepole halafu nitakuwa mwembe imara na wenye nguvu" (uk. 10).

Vilevile, baada ya viwavi kuliwa na nyuni na mvua kunyesha mwembe ulipata matumaini na kusema;

"Sasa naweza kukua bila kusumbuliwa" (uk. 13).

### 3.1.7 Sifa za mwembe, wapita njia na mtema kuni

Mwandishi amesawiri mandhari ya uharibifu wa mazingira kuwasilisha dhana nyingi katika uzoefu na ufahamu wa mandhari yanayomzunguka binadamu. Smith (2013), anasisitiza kuwa binadamu huwa na uzoefu na ufahamu wa mandhari kupitia kuona, kuhisi miongoni mwa njia nyinginezo. Kupitia mandhari ya uharibifu wa mazingira, mwandishi amewasilisha dhana yenyewe ya uharibifu wa mazingira kwa kusawiri wahusika wanaotekeleza vitendo vyenyewe vya uharibifu na kuweza kupata sifa mbalimbali kutokana na mandhari hayo.

**(i) Ni waharibifu**

Wapita njia wanachoma mzinga wa nyigu bila kujali hali ya mwembe. Wapita njia walichoma nyigu kwa vinga vya moto badala ya kutumia njia za kisayansi na kiteknolojia za kuwafukuza nyigu bila kuwaangamiza na kusababisha uharibifu wa mazingira.

**(ii) Hawana huruma**

Mtema kuni anakata matawi ya mwembe hadi shina la mwembe bila huruma.

"Aliendelea kukata matawi yote kisha shina la mwembe. Mwembe ukaanguka chini *pu*! Ukabaki kisiki tu. Ilikuwa hali ya kusikitisha mno!" (uk. 18).

Vilevile, wapita njia wanachoma nyigu kwa vinga vya moto vilivyosababisha nyigu kuangamia na kuchoma tawi la mwembe lililoangamia pia. Wapitanjia hao hawakuona wema ulioletwa na uwepo wa mwembe huo.

### 3.1.8 Sifa za mwembe na Chandu.

Mandhari haya yamesawiriwa na mwandishi kuwasilisha mandhari mapya ya soko. Mandhari haya yanampa msomaji uelewa mzuri wa mabadiliko ya soko na kuwa mji. Hata hivyo, wahusika waliosawiriwa wanapata sifa kadha wa kadha kutokana na mandhari haya.

**(i) Wenye shukrani**

Baada ya mtema kuni kukata mwembe ulibaki kisiki. Kisiki kile cha mwembe kilichipua vichipuzi vilivyoanza kuota majani. Miaka kadhaa baadaye, mwembe ukawa imara na kutoa maembe mengi matamu. Chandu alipokuwa katika pilka pilka pale mjini anachoka na kujipata ameketi chini ya mwembe ule ili apate kivuli na kubarizi. Mwembe unamtambua Chandu kisha kukatokea mchakato wa majani unaoangusha embe la kupendeza kama shukrani kwa Chandu:

> “Mwembe ulitazama chini na kumtambua Chandu papo hapo. *Hakika huyu ndiye Chandu! Chandu wa miaka na mikaka ingawa hana meno tisa sasa!* Embe la kupendeza likatoka mtini na kuanguka vizuri miguuni mwa Mzee Chandu (uk. 22).

**(ii) Ni wenye kumbukizi**

Wahusika Mwembe na Chandu ni wenye kumbukizi kwani wote wanakumbuka siku zao za zamani. Chandu alipokuwa amebarizi chini ya mwembe wa shani alihisi kama siku hiyo ilisadfiana na ya zamani alipokuwa ghulamu. Mwembe nao unatafakari kwamba Chandu angejua changamoto na mateso ulioyapitia.

**(iii) Wenye Maendeleo**

Wakati Chandu alikuwa kijana, soko ilikuwa mbali na kwao lakini kwa sasa akiwa mzee, maendeleo ya kiuchumi na kijamii yametokea:

> “Katika zama hizo soko lilikuwa mbali na Kijiji chao. Lakini sasa, licha ya soko kuwa karibu, masoko makuu kadhaa yalikuwa yamefunguliwa katika mji wao” (uk. 23).

**(iv) Wenye kutunza mandhari**

Mandhari ya pale kwenye mwembe wa shani yametunzwa vizuri na hata watu kuwekewa viti vya kukalia:

> "Mwembe huo ulisifika bara na baharini. Ulisifika kwa kuzaa maembe matamu sana. Isitoshe, matawi yake mengi na majani yake mapana yalitoa kivuli cha kuwakinga na jua watu zaidi ya mia moja kwa mara moja" (uk. 22).

Mwandishi wa *Embe Tamu* amebuni wahusika kama vile; Chandu, Bwaga, Mvua, Mchungaji, Wapita njia, Viwavi, Mwembe na wengineo. Wahusika hawa wamesawiriwa katika mandhari mbalimbali na kupata sifa chanya na hasi. Sifa chanya nikama vile; ushirikiano, uwajibikaji, wakarimu na wenye maendeleo nazo sifa hasi ni pamoja na; tamaa, uharibifu, katili miongoni mwa sifa nyinginezo.

## 3.2 Sifa za wahusika kutokana na mandhari katika *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005).

*Siku ya Wajinga* ni mojawapo wa vitabu teule vya kutumika katika utafiti. Mwandishi wa *Siku ya Wajinga* amesawiri aina kadhaa za mandhari kama vile; mandhari ya nyumbani, shuleni, darasani na mengine mengi. Amesawiri wahusika mbalimbali kama vile; Zito, Petro, Zena, Sadiki na wengine wanaoingiliana katika mandhari haya. Wahusika hawa wanapata sifa kutokana na mandhari katika kitabu cha *Siku ya Wajinga.*

### 3.2.1 Sifa za Zena, Sadiki, Zito na wazazi wao

Smith (2013) anasema kuwa, kila binadamu huwa na uzoefu na ufahamu wa dhana tofauti tofauti katika mandhari kupitia; kuona, kufikiria, kuhisia, kutenda shughuli za kijamii. Mwandishi amesawiri mandhari ya nyumbani ambapo panapatikana wahusika Zena na Sadiki wanaotekeleza shughuli mbalimbali za kinyumbani. Katika usawiri wa mandhari ya nyumbani, mwandishi pia amesawiri mhusika ambaye anatenda matendo mbalimbali yanayodhihirisha utundu na utovu wa

nidhamu jambo ambalo linatoa sifa mbalimbali kwa mhusika.Mandhari haya yanawapa wahusika sifa zifuatazo:

**(i) Ni wenye ushirikiano**

Sadiki na Zena walishirikiana katika shughuli tofauti tofauti. Sadiki na Zena wanashirikiana kufanya kazi kama vile; kusafisha vyombo, kufagia nyumba na shughuli nyinginezo za kinyumbani (uk. 1). Sadiki na Zena walitekeleza kazi nyumbani (uk. 8).

**(ii) Wenye bidii kazini**

Sadiki na Zena wanatia bidii katika kazi zote pale nyumbani. Wanapalilia mimea na kukama ng'ombe licha ya kuwa ni wanafunzi (uk. 8). Bidii yao pia iliwaongoza kufanya mazoezi ya masomo mbalimbali kama; Hesabu, Sayansi na mengine baada ya kumaliza shughuli za siku.

**(iii) Wenye kuwajibika**

Wazazi wa Sadiki na Zena wamewajibika kuwalea wana wao katika maadili mema kwani wamewafunza kuwa watoto waliowajibika na kuwafunza kujitendea shughuli zote pale nyumbani:

> "Wazazi wao daima waliwafundisha kushirikiana na kutochagua kazi. Walifunzwa kupalilia mimea mbalimbali na kuvuna. Walifunzwa kuwakama ng'ombe na kuwachunga wakiwa malishoni. Mama yao aliwafunza mapishi mbalimbali, usafi wa nyumba na ufuaji wa nguo pia. Kwa hivyo, hata wazazi wao walipokuwa safarini, hawakuwa na wasiwasi kwa sababu watoto wao walijua takriban kazi zote" (uk. 1-2).

**(iv) Ni wachokozi**

Zito anamkimbiza jogoo hadi anafikia kumchokoza mzee Lombo kwa kumwaga kitoweo chake. Jogoo aliingiza miguu ndani ya mchuzi wa mzee Lombo huku Zito akiwa mlangoni (uk. 27).

**(v) Wenye ujinga**

Zito alipokuwa anawaingiza mifugo zizini, fahali mmoja anasita kuingia na kuanza kutimua mbio huku Zito akimshika mkia. Kasi ya fahali inamzidi Zito na kuachilia mkia huku akianguka chini na kuumia. Huu ni ujinga kwa kuwa asingemshika ng'ombe mkia na kukimbizana na fahali huyo asingeumia.

**(vi) Wenye kuwajibika**

Babake Zito aliwajibika kwa kuwa alikuwa akirauka kila asubuhi kuwapeleka mifugo machungani. Vilevile, Zito na mamake wanawajibika kwani Zito aliwafungia mifugo hao zizini baada ya mamake kuwakama baadhi yao (uk. 35).

### 3.2.2 Sifa za Sadiki, Zena, Zito na walimu wao

Maana ya vitu na hali katika dunia hupatikana kupitia hali tofauti za uzoefu wa mtu kuhusu vitu hivyo na kutenda shughuli mbalimbali za kijamii (Mohanty, 2011). Mwandishi amesawiri wahusika Sadiki, Zena na Zito na kuwaweka katika mandhari ya shuleni wanapoonyesha uzoefu na ufahamu wa mandhari yenyewe kwa kutenda shughuli mbalimbali. Mandhari haya yanamsaidia msomaji kujinasibisha na wahusika katika mandhari ya shuleni na kupata sifa mbalimbali za wahusika.

**(i) Ni wasomaji**

Sadiki na Zena wanasomea shule ya Kambini na wako darasa la saba. Vilevile, walishirikiana katika masomo:

> "Baada ya shughuli za siku, ungewaona barazani mwao wakifanya mazoezi ya hesabu, kiingereza, sayansi na masomo mengine" (uk. 7).

**(ii) Wenye moyo wa kusaidiana**

Sadiki na Zena wanasaidiana masomoni na hata katika shughuli nyinginezo za kijamii. Sadiki na Zena walisoma na Zito ambaye alikuwa mzembe masomoni na kutenda mambo ya kijinga. Sadiki anamsaidia Zito kwa kumpa ushauri wa kuzingatia masomo na kuachana na matendo ya kijinga ili aweze kuwa mtu wa kutegemewa siku za usoni (uk. 10).

Mwandishi amesawiri mhusika Zito anayetekeleza kitendo cha wizi na ulaghai wa majibu ya maswali waliopewa na mwalimu wa hesabu shuleni. Kwa mujibu wa Smith (2013), kila binadamu huwa na uzoefu na ufahamu wa dhana tofauti tofauti katika mandhari kupitia kuona na kutenda shughuli za kijamii. Mwandishi amesawiri mandhari ya shuleni ili kumsaidia msomaji kujinasabisha na wahusika Zito, walimu na wengine. Kupitia kitendo hiki Zito anadhihirisha sifa zifuatazo;

**(iii) Ni mjanja**

Zito alitumia ujanja wa kijinga kupata majibu ya maswali. Zito alisubiri hadi walimu na wanafunzi wakaenda uwanjani kisha akanyapia ofisini na kuandika majibu ya maswali walioachiwa na mwalimu Petro. Mwalimu Petro alipokuwa anasahihisha kazi ya Zito aliishuku na kumwita Zito aeleze namna alivyopata majibu ya maswali hayo. Kwa hivyo, ujanja wake unatambulikana kwa kuwa alinyamaza tu.

**(iv) Ni mwizi na mwenye utovu wa nidhamu**

Zito anaiba majibu kwa mwalimu licha ya kuwa anapaswa kuwa uwanjani na wanafunzi wale wengine. Kitendo hiki kinadhihirisha utovu wa nidhamu.

**(v) Wenye kuwajibika na waelekezi**

Katika shule ya Hamio, walimu wanawajibika kazini kwa kuwaelekeza wanafunzi kubadilisha mtazamo wao wa maisha na kuwa watoto wazuri. Walimu wanawapa mafunzo ya dini na

mawaidha mbalimbali kwa mustakabali. Zito anasaidiwa kubadili tabia nakupata cheti cha kufuzu kwa nidhamu bora.

**(vi) Wasumbuvu**

Zito anawasubua walimu katika shule ya Hamio. Alifanya kazi kwa ulegevu bila kujali ndiposa akaamua kutowalisha ng'ombe wakati zamu yake ilipofika. Vilevile, alipanga kutoroka shuleni humo. Hata hivyo, anakabiliwa vilivyo na walimu na anabadili nia na kuwa mwema.

**(vii) Wenye majuto**

Wahenga walisema kuwa, majuto ni mjukuu. Zito anajutia ukaidi wake katika shule ya Kambini. Baada ya kubadilika na kurejelea katika shule hii anahuzunishwa na maandishi ("werevu ukikusumbua, jaribu ujinga") aliyoandika dawatini na kuwa wenzake walikuwa wamepiga hatua. Sadiki alikuwa katika kidato cha kwanza katika shule ya upili ya Juhudi (uk. 61).

### 3.2.3 Sifa za mwalimu Petro, Rukia pamoja na Sadiki, Zena na Zito

Mwandishi amesawiri mandhari ya darasani kuonyesha wahusika kadha wa kadha wakitenda shughuli mbalimbali za kielimu. Mwandishi amesawiri mandhari ya darasani ambapo wahusika wameweza kutekeleza mambo mengi kama vile; kuimba nyimbo na shughuli nyinginezo za ukuzaji talanta ambapo wameweza kupata sifa nyingi.

**(i) Ni mcheshi**

Mwalimu wa hesabu, Petro alikuwa mcheshi kutokana na mtindo wake wa kufundisha:

> "Kwa sababu somo lake lilikuwa na ucheshi mwingi, wanafunzi walimpenda sana. Aliweza kurahisisha kuelewa kwao kutokana na jinsi alivyowachekesha mara kwa mara" (uk. 12).

Vilevile, Zito ni mcheshi kwa kuwa alizunguka darasani akiwaonyesha wenzake sufuri aliyopata na kusema kuwa ni yai kubwa na atapelekea mamake akamkaangie. Jambo hili liliwafanya wenzake kuangua kicheko.

**(ii) Ni mwenye taasubi ya kiume**

Sadiki na Zena hawakutatizwa na somo la hesabu. Zito ana taasubi ya kiume kwa kuwa Zena au msichana mwingine pale darasani alipojitolea kumuonyesha Zito hesabu aliona kama madharau makubwa japo Sadiki alikuwa amemweleza kwamba somo la hesabu sio la wavulana kwa hivyo hapaswi kuona haya anapoelekezwa na msichana:

> "Kwake kuelekezwa na wasichana kulikuwa madharau makubwa" (uk. 13).

**(iii) Ni waelekezi**

Sadiki anamwelekeza Zito kubadili tabia zake za kijinga. Sadiki alimweleza kuwa asione haya kuelekezwa na wasichana kwa kuwa somo la hesabu si la wavulana peke yao (uk. 13). Katika (uk. 18) Sadiki na Zito walipokuwa wanaelekea nyumbani, Sadiki anamwelekeza aache ujinga kwa kuwa una madhara mengi.

**(iv) Wenye huruma na masikitiko**

Sadiki anamhurumia Zito kwa kufurahia ujinga wake anapozunguka darasani akiwaonyesha wanafunzi sufuri aliyopata (uk. 14). Vilevile, Sadiki anasikitikia rafikiye Zito wanafunzi wengine wanapomchekelea kwa kuonyesha ujinga wake (uk. 15).

**(v) Wenye kujitolea kazini**

Mwalimu Rukia amejitolea kazini kwani anawaongoza wanafunzi kuimba nyimbo na hata wanapoenda kucheza kandanda anaandamana nao (uk. 22). Vilevile, katika shule maalum walimu walijitolea kuwapa wanafunzi wao mawaidha. Mawaidha na mafunzo ya dini yanamfaa

Zito na kuibadili tabia yake. Mwandishi anatueleza kuwa mwishoni mwa mwaka wa pili Zito alipewa cheti cha kufuzu kwa nidhamu bora (uk. 61).

**(vi) Wenye bidii**

Wanafunzi wanatia bidii kuiga mapigo ya mwalimu Rukia ndipo waibuke waimbaji wazuri. Zito alipobadilisha tabia, alitia bidii katika yale walifundishwa hadi akawa hodari katika kazi ya useremala.

### 3.2.4 Sifa za wachezaji na wanafunzi

Michezo ni dhana muhimu katika maisha ya binadamu. Binadamu huwa na uzoefu wa dhana tofauti tofauti katika mandhari kupitia kuona, kutenda na kadhalika (Smith, 2013). Katika mandhari haya ya michezo mwandishi amesawiri wahusika ambao wanapata sifa kutokana na mandhari yenyewe. Sifa wanazopata kutokana na mandhari ya michezo ni pamoja na;

**(i) Washindi**

Wachezaji wa shule ya Kambini ni washindi kwani wameshinda michezo hadi kiwango cha wilaya:

> "Shule ya Kambini ilisifika sana kwa sababu ya timu yake bora ya kandanda. Iliweza kushinda shule nyingi na kunyakua kikombe cha wilaya mara kadha" (uk. 30).

**(ii) Wenye ujirani mwema**

Shule zote mbili; shule ya Kambini na shule jirani wana ujirani mwema kwani wanaleta wanafunzi wao pamoja kucheza kandanda:

> "Timu ya shule yao ilihitajika kufanya mazoezi na timu jirani siku hiyo" (uk. 16).

**(iii) Wenye umoja na ushirikiano**

Baada ya kucheza wilayani wanaungana pamoja na mwalimu Rukia. Wanapita njia ya mkato wote kuelekea nyumbani. Msafara wa wanafunzi huku wakishangilia unaonyesha ushirikiano.

### 3.2.5 Sifa za mwalimu Rukia na wanafunzi

Kwa mujibu wa Heidegger (1982), binadamu haelewi maana ya vitu na hali pamoja na dhana mbalimabali katika mandhari yanayomzunguka kwa kuangazia sehemu fulani ya mandhari bali hupata maana ya vitu kwa kuangalia uhusiano uliopo baina ya binadamu na mandhari yanayomzunguka, na jinsi vitu vilivyo katika mandhari hayo. Mandhari ya makaburini yanamsaidia msomaji kuelewa uhusiano wa maisha ya binadamu na kifo kwa kuwa binadamu huishi na mwishowe anafariki ambapo huzikwa makaburini. Kutokana na mandhari haya ya makaburini wahusika wanapata sifa kama vile;

**(i) Wenye kufuata utamaduni wao**

Mandhari ya makaburini yanaonyesha kuwa wahusika walikuwa na imani na desturi za jamii husika ambapo wao huzika wafu makaburini. Kitendo hiki cha kuzika wafu kinabainisha kuwa ni watamaduni.

**(ii) Wachokozi**

Msafara wa wanafunzi na mwalimu Rukia walipofika mtoni kila mmoja alikata kiu na wengine kunawa uso. Zito anamshawishi Sadiki kuangua matunda, mabungo. Walipokuwa kule juu ya miti ya mabungo Zito anamshtua mwalimu Rukia kwa kutupa tunda majini ambapo mwalimu Rukia anaingiwa na woga akidhani ni mizimu:

> "……Zito alichuma bungo moja bichi na kulirusha katikati ya mto likalia "Chubwi!" Kitendo hiki kilimshtua Sadiki na ……Rukia vilivyo" (uk. 32).

### 3.2.6 Sifa za mwalimu Petro na wanafunzi

Baada ya Zito kuanguka bondeni alipokuwa akikimbiza fahali, anapelekwa hospitali anapolazwa. Mwandishi amesawiri mandhari haya ya hospitali kuwapa wahusika sifa zifuatazo;

**(i) Wenye utu**

Wanafunzi na mwalimu Petro wanaungana kumtembelea Zito hospitali. Kitendo hiki kinaonyesha utu. Mwalimu Petro na wanafunzi walimtembelea Zito hospitalini alipokuwa amelazwa (uk. 39).

**(ii) Wenye upendo na ushirikiano**

Licha ya vituko vya Zito vya kijinga, wanakijiji wanaonyesha upendo na umoja wanapoungana pamoja kumshughulikia anapoumia. Mtu mmoja anararua shati lake na kumfunga Zito kichwani ili kuzuia michirizi ya damu (uk. 37). Vilevile, watu wanashirikiana kumpeleka Zito hospitalini. Wazazi wa Zito walisaidiwa na wanakijiji kumpeleka Zito hospitalini:

> "Walisaidiwa na watu wengine kumbeba Zito mzegamzega hadi hospitalini ambako alilazwa" (uk. 37).

Mwandishi wa *Siku ya Wajinga*, amesawiri mandhari kama vile mandhari ya; nyumbani, shuleni, makaburini miongoni mwa mengineyo. Mandhari haya yamekuzwa na kuwepo kwa wahusika tofauti. Wahusika hawa wamepata sifa kama vile; wenye bidii, waelekezi, watamaduni, wenye utu miongoni mwa sifa nyinginezo.

### 3.3 Sifa za wahusika kutokana na mandhari katika *Njiapanda*

*Njiapanda* kama ilivyotangulizwa katika sura ya pili ni kitabu kinacholenga wanafunzi wa darasa la nane katika shule za msingi ili kuendeleza na kukuza uwezo woa wa kusoma. Mwandishi wa kitabu hiki amesawiri aina mbalimbali za mandhari kama vile; mandhari ya barabarani, mandhari ya kidhahania, mandhari ya michafuko na migomo shuleni miongoni mwa mandhari mengineyo. Mwandishi amesawiri wahusika mbalimbali wanaoingiliana katika mandhari haya kutekeleza shughuli mbalimbali za kijamii. Wahusika hawa wanapata sifa mbalimbali kutokana na mandhari haya.

### 3.3.1 Sifa za Waislamu,Wakristo, mama msaidizi na dereva

Uzoefu na ufahamu wa dhana mbalimbali katika mandhari hutokana na kuona kwa binadamu, kufikiria, kuhisi pamoja na kutenda shughuli za kijamii (Smith, 2013). Dhana ya usafiri barabarani imewasilishwa na mwandishi kupitia usawiri wa mandhari ya barabarani. Matukio yanatokea katika barabara ya *Grand Coalition*, yanawapatia wahusika sifa kadhaa.

**(i) Wenye kufuata utamaduni wao**

Katika barabara ya *Grand coalition* mwandishi amesawiri wahusika katika maombolezi. Wahusika hawa ni watamaduni kwa kuwa maombolezi yao yanafuata mila na desturi kulingana na utamaduni wao. Waislamu wamebeba jeneza kwa mikono ilhali Wakristo wanatumia gari refu jeusi lililobeba jeneza (uk. 2).

**(ii) Ni wacha Mungu**

Waombolezaji ni wacha Mungu kwani wanashiriki kuimba nyimbo za kumsifu Mungu:

> "Nyuso za Wakristo waliofikwa na msiba zilikuwa zimegubikwa huzuni. Walikuwa wakiomboleza na kuimba nyimbo za kumsifu Bwana" (uk. 2).

**(iii) Wenye ushirikikano**

Waombolezaji wameungana pamoja kama jamii kuwazindikisha waliofariki. Vijana Waislamu walibeba jeneza huku wazee wakiwafuata nyuma (uk. 1).

**(iv) Ni watiifu**

Katika barabara hii ya *Grand coalition*, ambayo ni njiapanda kulikuwa na taa za trafiki. Wapitanjia na madereva wa magari wanaonyesha utiifu na kutokiuka sheria za barabarani kwani wanapofika kwenye gurufu wanakita hapo hadi taa zilipoashiria nyekundu ndipo wakaondoka (uk. 4).

**(v) Wenye utu**

Mama msaidizi na dereva wa gari dogo lililobeba mwanamke mjamzito ni wenye utu. Mwanamke mjamzito anapoanguka katikati ya barabara, alisaidiwa na wasamaria waliompakia kwenye gari ndogo na kupelekwa hospitalini.

### 3.3.2 Sifa za Bikizee na Kijana

Kwa mujibu wa Mohanty (2011), finominolojia hujihusisha na uchunguzi wa kuwepo kwa vitu katika mandhari na ufahamu wa vitu hivyo pamoja na uzuri na ubaya wa matendo ya binadamu katika mandhari. Mwandishi amesawiri mandhari ya kidhahania kwa kuweka wahusika katika mazungumzo ya kidhahania ambapo ushauri nasaha unatolewa kwa wahusika kupitia mazungumzo hayo. Mandhari haya ya kidhahania yanachangia sifa kadhaa za wahusika.

**(i) Ni watambuzi**

Katika mazungumzo ya Bikizee na Kijana, inadokezwa kuwa Kijana ni mtambuzi kwani ameishi duniani na hata kama amefariki ameweza kutambua kuwa maisha duniani si matamu (uk. 6).

**(ii) Wenye hekima**

Bikizee anaonyesha hekima na busara kwa nasaha anayotoa kwa Kijana na Kiumbe. Anasema,

> *"usimpotoshe mwenzako!"* (uk. 6)
>
> *"Usss! Acha kumwambia maneno ya kukosa adabu... Mfahamishe tu kwa njia nzuri. Huna njia nyingine isiyokuwa hiyo ya utovu wa adabu?"* (uk. 7).

Kauli hizi zinaonyesha mtu mwenye hekima na busara kwa kuwa anataka Kijana atumie maneno yenye adabu bila kumpotosha Kiumbe.

**(iii) Wenye majuto**

Kijana anajutia kukata roho akiwa wa umri mdogo. Anasema kuwa, yeye ni wa umri wa miaka kumi na saba lakini ametangulia ahera. Anasema,

“Tusiwasikize wale walevi wanaosema, ‘ponda raha, sijui mali, kufa kwaja’, La!” (uk. 7).

**(iv) Wapenda raha na anasa**

Kijana anakiri kuwa vijana wa siku hizi wanapenda raha na anasa kwa kuwa; wanakunywa pombe, wanatumia mihadarati, wanaenda densi na kutembea na vimanzi (uk. 7).

### 3.3.3 Sifa za vijana, walimu na Kiumbe

Mwandishi amesawiri wahusika wanafunzi katika mandhari ya shuleni, wanafunzi hawa wanasababisha michafuko shuleni kwa; kuchoma mabweni, madarasa, nyumba ya mwalimu mkuu na gari lake. Mandhari haya yanamsaidia msomaji kujinasabisha na wahusika ili kupata sifa za wahusika hao.

**(i) Wenye ukatili**

Vijana wa shule waliogoma walichoma mabweni na baadhi ya wanafunzi wakafa. Kitendo hiki kinaonyesha ukosefu wa huruma kwa wenzao watakao athirika kwa kupata majeraha au kupoteza uhai.

**(ii) Ni wenye utundu**

Wanafunzi wanashiriki maandamano na hata kuchoma gari la mwalimu na maktaba ya shule (uk. 8).

**(iii) Ni wahuni**

Bikizee anakiri kuwa uhuni miongoni mwa wanafunzi wa St. Kizito, Bombolulu na Kyanguli uliwafanya kuchoma shule zao bali si uchochezi wa siasa. Bikizee anasema,

> *“Jinai ni jinai, hata ifanywe na mtu mzima au kijana! Huo ni uhaini tu! Kwani mabweni ya St. Kizito, Bombolulu Girls na Kyanguli yalipochomwa, ulikuwa wakati wa uchanguzi?”* (uk. 8).

**(iv) Wenye mapuuza**

Mwandishi katika mandhari ya kidhahania amechora wahusika walimu wenye mapuuza kwani mhusika kijana anaelezea kuwa wamenyimwa fursa ya kufanya majadiliano na viongozi wa shule bila vikwazo jambo ambalo linachangia michafuko shuleni (uk. 9).

**(v) Wenye kutetea haki zao**

Vijana wamejitokeza kama wenye kutetea haki zao. Kijana anadai kuwa wanahaki ya kujieleza, haki ya kuwa na uhuru wa kutoa maoni miongoni mwa haki nyinginezo na ndio maana michafuko inatokea shuleni wakitetea haki zao:

> *"Uhuru kamili, kweli, si mzuri. Lakini mfumo wa shule lazima uzingatie demokrasia, ambapo wanafunzi wanaruhusiwa kujadiliana. Kufanya mijadala bila vikwazo. Wote wenye kuhusika wawe wanazungumza kila mara kutatua matatizo yao!"* (uk. 10).

**(vi) Wenye hekima na uwajibikaji**

Bikizee anamwelezea Kijana kuwa heshima si utumwa na vijana wanapaswa kuwaheshimu watu wazima na wajiheshimu wenyewe ndipo wapate kuheshimika (uk. 9).

**(vii) Wenye kudadisi**

Kiumbe ni mdadisi. Kiumbe ameuliza maswali ili apate kujua:

> *"Huko ndioo wapi?*
>
> *Mbona mnapelekwa mkiwa mmebebwa? Kwani hamuwezi kujipeleka wenyewe?*
>
> *Mbona hamuelewani? Kuna tatizo?"* (uk. 6).

### 3.3.4 Sifa za mama msaidizi, mpokezi, Lulu, madaktari na Bob

Finominolojia huunda mkusanyiko mpana wa ufahamu na uzoefu wa mandhari na husaidia binadamu kupata maana ya vitu na hali katika mandhari kwa kuwa uzoefu wa binadamu humpa ufahamu wa mambo mengi katika akili yake zaidi ya anachoona na kusikia (Merleau, 2012).

Mwandishi amesawiri mandhari ya hospitali ambapo amesawiri wahusika kadhaa katika mandhari haya na ambao wana uzoefu na ufahamu wa mandhari ya hospitali kwani wanatekeleza majukumu yao ya kimatibabu kwa ustadi. Mandhari haya yamechangia sifa za wahusika kama vile;

**(i) Wenye kuwajibika**

Mwanamke mjamzito anapofikishwa hospitali, machela ya magurudumu inaletwa haraka na kupelekwa chumba cha dharura bila kusubiria usajili. Huu ni uwajibikaji wa wafanyakazi wa hospitali hii. Mpokezi anawajibika vilivyo baada ya kugudua kuwa mwanamke mjamzito alikuwa amesajiliwa katika hospitali hiyo. Mpokezi anampigia simu daktari. Vilevile, mama msaidizi anawajibika kwa kushughulika kutafuta jamaa wa mwanamke mjamzito hadi akampata Lulu (*Beste*), rafikiye mwanamke mjamzito.

**(ii) Waaminifu**

Msaidizi wa mwanamke mjamzito anamkabidhi rafiki wa mwanamke mjamzito (Lulu) stakabadhi za mwanamke mjamzito, Isabela anapofika hospitali.

**(iii) Wenye utu na nia njema**

Mpokezi katika hospitali anamwelekeza mama msaidizi kufanya kila anachotakiwa ndipo mwanamke mjamzito apate usaidizi pale hospitalini kwa haraka. Mama msaidizi anampa mpokezi kitambulisho na kadi ya bima ya mwanamke mjamzito kama alivyoangizwa. Mpokezi anamwelekeza mama msaidizi kumuona mwanamke mjamzito alipopata nafuu huku akisubiri daktari wake binafsi afike amshughulikie. Lulu anapofika hospitali, mpokezi anampa fomu za bima na za kulazwa hospitalini amjazie mwanamke mjamzito. Vilevile, baadaye anamfahamisha kuwa mamlaka ya hospitali iliwapigia wazazi wa mwanamke mjamzito na kupata kibali cha kumfanyia upasuaji kwa kuwa yeye alikuwa na umri wa chini ya miaka kumi na minane.

**(iv) Wenye urafiki wa dhati**

Lulu anaonyesha urafiki wa dhati kwani anapopigiwa simu kuhusu Isabela; hakusita kwenda kumshughulikia (uk. 14).

**(v) Wenye ushirikiano**

Madaktari wanashirikiana na kuungana pamoja kutekeleza operesheni ya mwanamke mjamzito (uk. 19).

**(vi) Ni wataalamu**

Madaktari wanaofanya operesheni ni wataalamu kwani wamevaa sare za taaluma ya umatibabu na wanatekeleza kazi yao kiutaaluma (uk. 19).

**(vii) Ni wasaliti**

Bob, mpenziwe mwanamke mjamzito anamsaliti mpenzi wake baada ya kumpachika mimba na kumwacha. Mwanamke mjamzito alipoelezwa na mama msaidizi kuwa Bob, mpenziwe alikuwa mteja alibaki na maswali mengi kichwani:

> *"Bob yuko wapi? Alienda wapi usiku wa jana alipokuja kuniona dakika mbili na kutoweka ghafla? Mbona hakuja kunichukua kunipeleka hospitali? Amepatikanana nini? Kwa nini nilipompigia simu aliikata? Ana nini..."* (uk. 16).

Mwandishi wa *Njiapanda* amesawiri mandhari mbalimbali ambayo yanakuzwa na wahusika kama vile; Wakristo, Waislamu, Mwanamke mjamzito, mpokezi, madaktari, Lulu, Bob miongoni mwa wengine. Wahusika hawa wamepata sifa kadha wa kadha kutokana na utendaji wao. Baadhi ya sifa hizi ni; watamanduni, wenye ushiriakano, wenye utu, wataalamu, wasaliti miongoni mwa sifa nyinginezo.

### 3.4 Hitimisho

Sura hii ilishughulikia jinsi wahusika wanavyopata sifa kutokana na aina mbalimbali ya mandhari yaliyosawiriwa na waandishi wa vitabu teule vya fasihi andishi ya watoto. Vitabu hivi teule ni; *Embe Tamu* (Njogu, 2003), *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005) na *Njiapanda* (Amana, 2008).

Mihimili ya nadharia ya finominolojia ilitumika kuchunguza jinsi mandhari yalichangia sifa za wahusika. Wahusika walidhihirisha kuwa na sifa kama vile wahusika; watiifu, waliowajibika, wataalamu, wenye hekima na busara miongoni mwa sifa nyinginezo zinazotokana na aina mbalimbali za mandhari yaliyosawiriwa na waandishi wa vitabu teule.

Sura ambayo inafuata ilifafanua matumizi ya lugha katika usawiri wa mandhari katika; *Embe Tamu* (Njogu, 2003), *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005) na *Njiapanda* (Amana, 2008).

# SURA YA NNE

# MATUMIZI YA LUGHA KATIKA USAWIRI WA MANDHARI

## 4.0 Utangulizi

Sura hii ilibainisha matumizi ya lugha katika usawiri wa mandhari katika vitabu teule.

Nadharia ya kimtindo ambayo iliasisiwa na Leech (1969), miongoni mwa waasisi wengine, imetumika kusaidia uchanganuzi. Leech (1969) anasema kuwa, athari ya kazi yoyote ya fasihi kwa msomaji hutegemea mtindo wa mwandishi ambaye hutumia lugha kwa njia mbalimbali pamoja na vipengele tofauti vya kimtindo ili kumwadhiri msomaji kihisia na kimawazo. Ngara (1982) anadai kwamba, vipengele mbalimbali vya fasihi; mandhari, maudhui na wahusika haviwezi kuwasilishwa bila kutumia lugha. Wamitilia (2003) anadai kuwa, umtindo humwezesha mchanganuzi kuchunguza jinsi lugha ilivyotumiwa katika uchanganuzi wa kazi ya fasihi. Anaongezea kuwa, fasihi ni sanaa ya lugha ambayo inamhusu binadamu na huwa katika umbo ambalo hutambuliwa na wanajamii. Anasisitiza kwamba, lugha ndio nyenzo kuu katika kazi yoyote ya fasihi. Hii ina maana kuwa, hatuwezi kuwasilisha fasihi pasipo kuwa na lugha.

Kulingana na Khasiani na Indindi (2018), matumizi ya lugha hujikita katika mbinu za kimuundo, mbinu za kimtindo na tamathali za usemi. Mbinu za kimuundo hutumiwa na msanii kuwasilisha ujumbe katika kazi ya fasihi. Mbinu za kimtindo humsaidia msanii kuumba kazi yenyewe na mwishowe tamathali za usemi hutumika kupamba kazi ya msanii.

Sura hii ilionyesha jinsi ambavyo waandishi wa vitabu teule vya fasihi ya watoto walivyotumia lugha kusawiri mandhari. Vitabu teule vilivyotumika katika uchunguzi ni pamoja na; *Embe Tamu* (Njogu, 2003), *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005) na *Njiapanda* (Amana, 2008). Aina za mandhari katika kila kitabu zilichunguzwa ili kubaini matumizi ya lugha katika usawiri wa mandhari hayo.

### 4.1 Matumizi ya lugha katika usawiri wa mandhari katika *Embe Tamu* (Njogu, 2003), *Siku za Wajinga* (Momanyi, 2005) na *Njiapanda* (Amana, 2008).

*Embe Tamu* ni kitabu cha ziada kinachonuiwa kuendeleza msingi wa kusoma na kukuza uwezo wa kusoma wa wanafunzi wa darasa la tano katika shule za msingi. Mwandishi wa *Embe Tamu* alisawiri aina mbalimbali za mandhari kama vile mandhari ya; ghala, sokoni, hospitali miongoni mwa mandhari mengineyo. Mandhari haya yalisawiriwa kwa matumizi mbalimbali ya lugha.

Kama ilivyotangulizwa katika sura ya pili na ya tatu, *Siku ya Wajinga* ni mojawapo wa vitabu teule vya kutumika katika utafiti. Mwandishi wa *Siku ya Wajinga* alisawiri mandhari ya aina mbalimbali kama vile; mandhari ya nyumbani, mandhari ya shuleni, mandhari ya hospitali miongoni mwa mengineyo. Mandhari haya yalisawiriwa na mwandishi kwa kutumia lugha ili kuwasilisha ujumbe aliokusudia.

*Njiapanda* kama ilivyotangulizwa katika sura ya pili na ya tatu ni kitabu kinacholenga wanafunzi wa darasa la nane katika shule za msingi ili kuendeleza na kukuza uwezo wao wa kusoma. Mwandishi amesawiri mandhari ya aina mbalimbali kama vile; mandhari ya barabarani, mandhari ya kidhahania, mandhari ya michafuko na migomo shuleni miogoni mwa mandhari mengineyo. Mwandishi ametumia mbinu mbalimbali za kifasihi na matumizi ya lugha katika usawiri wa mandhari haya.

#### 4.1.1 Usimulizi

Ngara (1982) anasema kuwa, vipengele muhimu vya fasihi kama vile maudhui, mandhari na wahusika, haviwezi kuwasilishwa bila kutumia lugha. Wamitila (2003) anaeleza kuwa, usimulizi ni uelezi wa matukio katika hadithi. Mawazo ya Wamitila ni kwamba, kazi zote za fasihi lazima ziwe na matukio na hayo matukio yanaweza kuwasilisha kwa hadhira kwa njia nyingi za usimulizi.

Mwandishi anasawiri mandhari ya ghala katika *Embe Tamu* kwa kusimulia Chandu akiwa karibu na ghala (uk. 1). Ilikuwa zamu yake kwa kuwa ndugu zake watatu walikuwa wamemtangulia (uk. 2). Aidha, mwandishi ametoa maelezo ya Chandu akibeba kile kikapu kilichojaa maembe.

> "Chandu alikiangalia kikapu kile akatikisa kichwa chake. *Nitawezaje kukibeba kikapu hiki kilichojaa maembe? Lisilokuwa na budi hutendwa*. Chandu alikichukua kikapu chake na kujitwika nacho kichwani" (uk. 2).

Haya ni masimulizi ambayo yanasaidia kusawiri mandhari ya ghala kuwasilisha maudhui ya ukulima.

Mandhari ya sokoni katika *Embe Tamu* yanaelezewa kupitia masimulizi. Msimulizi anasema;

> "Ilikuwa ni siku ya gulio. Hii ni siku maalum ya soko. Soko lenyewe hufanywa nje ya vijiji. Hufanywa kwenye kiwanja ambacho ni wazi. Hufanywa nje ya majengo ya soko la kawaida. Wanavijiji waliipanga siku hiyo ili watu wajumuike pamoja kufanya biashara" (uk. 2).

Mwandishi amesimulia safari ya Chandu na Bwaga wakielekea sokoni. Chandu na Bwaga walianza safari yao mapema kwa kuwa walisafiri kwa miguu. Chandu alikuwa mbele ya Bwaga. Kasi ya Chandu ilimfanya ajikwae na kuangusha embe moja linalookotwa na Bwaga na kushawishika na hatimaye kulila. Masimulizi haya yanasaidia kusawiri mandhari ya usafiri.

Mwandishi amesimulia safari ya asili ya mwembe. Baada ya Bwaga kula lile embe anatupa mbegu ardhini. Katika mandhari ya ufugaji, mwandishi anatueleza kuwa mchungaji na ng'ombe wake waliikanyanga mbegu ya embe na kuizika ardhini hata bila fahamu na kuendeleza safari ya chanzo cha mwembe. Masimulizi haya yanasawiri mandhari ya ufugaji na kuonyesha jinsi mimea na wanyama wanafaana na kutegemeana bila hata fahamu.

Mwandishi anasimulia ukuaji na changamoto za mwembe. Mbegu ilianza kutokeza mizizi na kuzama udongoni. Mche wa mwembe ulichipuka na kuota majani. Baada ya muda, beberu anafahamia Mwembe ule na kula matawi yake yote. Baadaye, kisiki kikaanza kuchipua majani na hatimaye vipepeo wakatua na kutaga mayai yalioangua viwavi. Viwavi wale wakala majani ya mwembe (uk. 12). Masimulizi haya yanasaidia kusawiri mandhari ya ukuaji wa mimea.

Mwandishi amesawiri mandhari ya uharibifu wa mazingira kwa kusimulia jinsi mwembe ulivyoathiriwa na shughuli za kibinadamu na hali ya anga. Binadamu aliamua kuchoma mzinga wa nyingu na kuchoma matawi ya mwembe. Binadamu pia anakata mwembe ili apate kuni za kupikia. Vilevile, wakati wa msimu wa masika umeme ulipiga sehemu kubwa ya mwembe ikaungua (uk. 17).

Mwandishi ametumia masimulizi kueleza pacha wawili, Zena na Sadiki. Pacha hawa wawili walishirikiana katika shughuli za nyumbani na masomoni. Mwandishi ameeleza kuwa wazazi wa pacha hawa walikuwa wamewafundisha kuwajibika katika kazi zote pale nyumbani ndio maana hawakuwa na wasiwasi wowote walipokuwa safarini (uk. 8). Masimulizi haya yanatumiwa na mwandishi kusawiri mandhari ya nyumbani katika *Siku ya Wajinga*.

Mwandishi ametumia masimulizi kusawiri mandhari ya shuleni. Zena, Sadiki na Zito wanasoma katika shule ya msingi ya Kambini na walikuwa darasa la saba. Haya yanafahamika kupitia masimulizi. Vilevile, mwandishi amesimulia kuhusu mandhari ya shule maalum, shule ya Hamio ambayo Zito alipelekwa ili kubadilisha tabia yake. Shughuli ambazo zilitekelezwa ili kuwapa wanafunzi mafunzo mema ya kiutu chini ya ulinzi mkali yanafahamika kupitia masimulizi. Bali na mafunzo wanafunzi walitakiwa kufanya kazi zingine kama walivyoratibiwa (uk. 51). Aidha, anatueleza vile Zito alivyojiendeleza katika shule hiyo ya Hamio hadi akabadilisha mienendo yake ya kijinga.

Mandhari ya shuleni yamesawiriwa kwa kutumia masimulizi. Mwandishi anaeleza kuwa Zito alikuwa amedhihirisha mabadiliko yasio ya kweli kumbe alikuwa na mpango wa kutoroka shuleni. Anafanikiwa kutoroka kwa kuruka ua wa shule lakini anasikika na mlinzi ambaye anamkimbiza na hatimaye kumkamata na kumpeleka kwa mwalimu mkuu ambapo Zito alijua ataadhibiwa kwa viboko. Mwalimu mkuu aliwaita walimu wale wengine na kumpa Zito mawaidha.

> "Walimkumbusha kuwa akiyataka maisha bora, hakuwa na jingine ila kuvumilia na kuwatii wakuu wake" (uk. 59).

Mafundisho ya dini na mawaidha aliyopewa na walimu yalimfanya abadilishe tabia yake na kuwafurahisha wazazi wake pamoja na sadiki. Zito alijiunga na shule ya Kambini tena katika darasa la saba. Anajutia maandishi aliyokuwa ameyaandika dawatini. Anayafuta na kuandika haya kwenye karatasi "ukitaka cha uvunguni sharti uiname" (uk. 62 – 63). Maelezo haya yanasawiri mandhari ya shuleni katika *Siku ya Wajinga*.

Walimu na wanafunzi wa shule ya Kambini wanasawiri mandhari ya darasani. Mwandishi anasimulia jinsi mwalimu Rukia alivyowafunza wanafunzi kuimba wakifuatilia mapingo ya wimbo. Mwalimu Rukia alipokuwa anawafundisha wanafunzi wa darasa la saba wimbo mpya ulioitwa *safari ya Bamba* alibaini kuwa kuna sauti ambayo ilisikika kutokubaliana na zingine (uk. 22). Mwalimu Rukia anabaini kuwa Zito ndiye aliyekoroma kama chura na kufukuzwa nje, sauti za wanafunzi zilifuatana vizuri (uk. 23). Mwandishi anaendeleza mandhari ya ukuzaji wa talanta kwa kusimulia kuhusu mwalimu Mfaki, mwalimu mkuu ambaye aliwapa wanafunzi kazi ya kutunga hadithi zao. Wakati wa kusimuliana darasani ikawa ni zamu yake Zito. Zito alikuwa ametunga kisa ambacho hakina mantiki kwa kuwa;

> "Alianza kuvipa uhai vitu kama sahani, vikombe, majani, nahata kuwafanya wanyama kama paka kuongea! Aliitia chumvi hadithi hiyo ikawa haiaminiki tena" (uk. 25).

Mwandishi anasimulia kuhusu timu ya kandanda ya shule ya Kambini. Anaeleza kuwa timu hii ilikuwa stadi kwa kuwa ilikuwa imenyakua kikombe cha kandanda wilayani mara kadha (uk. 30). Siku hiyo timu hii ilikuwa imefuzu kuingia mkondo wa mwisho wa mashindano ya kandanda wilayani, baada ya kuishinda timu ya shule ya Mkomani mabao mawili bila jibu. Vilevile, ameeleza safari ya wanafunzi ya kurejea nyumbani kwa kutumia njia ya mkato huku wakishangilia mabingwa wa mchezo huo. Masimulizi haya yanasawiri mandhari ya kimichezo kwa msomaji.

Kuna maelezo yanayodokeza mandhari ya hospitali. Mwandishi anasimulia vile wazazi wa Zito walivyosaidiwa na watu wengine kumbeba hadi hospitalini. Zito alilazwa kwa kuwa alikuwa amepoteza fahamu. Zito akiwa katika ulimwengu wa ndoto, aliota mwalimu Hodari akiwa amewapa swali gumu la hesabu ambalo baadaye wanabaini kuwa lilitungwa na mmoja wao na walipokuwa wanamkimbiza Zito anaanguka chini. Masimulizi haya yanasaidia katika usawiri wa mandhari ya hospitali katika *Siku ya Wajinga*.

### 4.1.2 Taswira

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), fasihi ni sanaa ya lugha ambayo inamhusu binadamu na huwa katika umbo ambalo hutambuliwa na wanajamii. Msokile (1999), anafafanua taswira kama mkusanyiko wa picha ambazo msanii anaziunda kutokana na maelezo yake katika kazi ya fasihi. Msomaji hujenga picha akilini mwake kutokana na maneno ya mwandishi au msimulizi. Kwa kurejelea maelezo ya Khasiani na Indindi (2018), taswira ni mbinu ambapo mwandishi hutumia maelezo yanayojenga picha fulani katika akili ya msomaji. Picha hizo hutokana na matumizi ya sitiari.

Picha ya akilini inatokea wakati ambapo msimulizi anatueleza kuhusu soko. Soko hili hufanywa nje ya vijiji katika kiwanja wazi. Anasema kuwa;

> "Ukienda katika gulio utakuta watu aina mbalimbali na bidhaa nyingi tofauti tofauti" (uk. 2).

Katika mandhari ya mvua mwandishi ametumia taswira kuonyesha vile maji yalivyokuwa mengi. Anasema;

> "Maji hayo yalisomba mchanga, changarawe,vijiti, majani, karatasi na kila aina ya uchafu na kuusafirisha sehemu nyingine. Maji mengine yalipenya ndani ya mchanga" (uk. 8).

Kuna taswira ya jinsi wapita njia walivyouchoma mzinga wa nyingu. Mwandishi anasema kuwa, kupitia kuchoma kwa mzinga wa nyingu, majani mengi ya mwembe yalianguka chini na kuwa meusi. Taswira hii inasawiri uharibifu wa mazingira. Vilevile, wakati wa msimu wa masika umeme uliupiga mwembe huo na kuunguzwa (uk. 17).

Mwandishi amejenga picha ya akilini kwa kutoa maelezo kuhusu bustani la mji. Hapa ndipo mwembe wa shani ulipokuwa. Taswira inaendelea kudhihirika kupitia maelezo ya mwembe ule ukimwangushia mzee Chandu embe pale miguuni pake.

> "Embe la kupendeza likatoka mtini na kuanguka vizuri miguuni mwa Mzee Chandu" (uk. 22).

Kuna picha ya akilini inayotokana na maelezo kuhusu Zito akimfukuzu jogoo. Mbio za Zito na jogoo yule ziliwashangaza majirani kwa kuwa alimfukuza kwenye viambaza vya nyumba zao. Hatimaye, jogoo yule alijitoma kwa vishindo na kuingia ndani ya nyumba ya mzee Lombo aliyekuwa akila mchuzi kwa sima. Mwandishi ameeleza kwa kusema kuwa;

> "Jogoo aliruka juu na kuingiza miguu yake ndani ya bakuli la mchuzi" (uk. 27).

Mwandishi ametumia taswira ya Zito akitimua mbio na fahali mmoja huku akiwa amemkamata mkia kusawiri mandhari ya utundu na utovu wa nidhamu. Watu wanastaajabishwa na jambo hili walililoliona kama sinema. Kasi ya fahali huyu inamzidi Zito na kuanguka chini. Alipata majeraha usoni na kuzirahi. Mtu mmoja alirarua shati la Zito na kumfunga kichwani ili kuzuia michirizi ya damu (uk. 37).

Maelezo ya mwandishi kuhusu namna Zito alivyoiba majibu ya zoezi waliopewa na mwalimu Petro yanasaidia kusawiri mandhari ya wizi na ulaghai. Mwandishi anasema;

> "Zito alinyapianyapia hadi afisini kwa mwalimu Petro. Alipekuapekua nyaraka na makaratasi yake mpaka akaona ile zoezi walilopewa. Majibu ya zoezi hilo yaliandikwa kwa kalamu ya wino mwekundu. Alichukua karatasi na kunakili majibu yote, kisha akipiga mbio hadi darasani na kuyaandika yote katika daftari lake" (uk. 16).

Kuna picha ya akilini inayotokana na maelezo kuhusu mwalimu wa hesabu, mwalimu Petro. Mwalimu Petro alipokuwa akifundisha hesabu alikuwa hatulii mahali pamoja. Alirusha mikono na kuruka kutoka upande mmoja wa darasa hadi mwingine (uk. 12). Aidha, katika (uk. 53) mwandishi anachora picha nyingine ya akilini anapoeleza jinsi nguruwe na ng'ombe walivyohangaika na kutoa milio iliyotatiza masomo katika madarasa. Mwandishi ametumia taswira kusawiri mandhari pana ya darasani na shughuli mbalimbali katika mandhari hayo.

Mwandishi ametumia taswira ya njia ya mkato ambayo wanafunzi walipita wakitoka kushabikia timu yao ya kandanda kusawiri mandhari ya makaburini. Anasema kuwa;

> "……….njia ya mkato iliyopitia kwenye mto huu kulikuwa na makaburi yaliyojengewa ua. Yalikuwa na misalaba nyeupe iliyong'aa wakati wa jua la kuchwa. Kwa mbali, misalaba hiyo ilionekana kama watu walionyoosha mikono yao wakisali" (uk. 30 -31).

Kauli hii inatupa picha ya akilini kuhusu mandhari hayo ya makaburini.

Maelezo kuhusu vituko vilivyotokea katika barabara ya *Grand Coalition* yanazua picha ya akilini. Kulitokea Waislamu vijana waliobeba jeneza huku wakifuatwa na wazee nyuma (uk. 1).

Upande wa pili wa barabara kulikuwa na msafara wa magari yalioangikwa tepe nyekundu. Kati ya msafara huo kulikuwa na gari moja refu jeusi lililokuwa limebeba jeneza. Nyuso za Wakristo zilikuwa zimegubikwa huzuni huku wakiomboleza na kuimba nyimbo za kumsifu Bwana. Waislamu na Wakristo walipofika kwenye gurufu walisimama papo hapo.

Aidha, wapita njia walikuwa wamesongamana wakisubiri wakati taa zitakapoashiria wekundu ndipo itakapokuwa zamu yao ya kupita. Walipoanza kupita, mwanamke mjamzito alianguka chini katikati ya barabara na kuzirai (uk. 3).

Kuna picha ya akilini inayotokana na maelezo kuhusu jinsi mwanamke mjamzito alivyopokelewa alipofikishwa hospitali. Mwanamke mjamzito aliwekelewa kwenya machela ya magurudumu na kupelekwa katika chumba cha dharura. Picha ya akilini inajitokeza kupitia maelezo ya mwanamke mjamzito akipelekwa katika chumba cha dharura kwa kubebwa na machela ya magurudumu manne huku mwanamke msaidizi na mpokezi wakiendelea kutambulisha stakabadhi za mwanamke mjamzito (uk. 13).

Mwandishi anaendeleza mbinu ya taswira kwa kueleza hali ilivyokuwa katika chumba cha dharura. Mwanamke mjamzito amewekewa mipira ya oksijeni puani na kuwekewa dripu mkono mmoja. Aidha, mwandishi ameeleza na kuchora picha ya akilini ya chumba cha upasuaji. Mwandishi anasema kuwa;

> "Akalazwa kwenye kitanda cha upasuaji. Mtaalamu wa nusukaputi akamdunga sindano ya kumpoteza fahamu. Msichana mjamzito hakuchukua sekunde thelathini, fahamu zake zikapaa kwenye ulimwengu mwengine …" (uk. 19).

### 4.1.3 Chuku

Njogu na Chimerah (2008), wanaifafanua tamathali ya chuku kama mbinu ya kutia chumvi ili kueleza jambo fulani kwa msisitizo. Mwandishi ametumia chuku kuonyesha kasi ya Chandu katika mandhari ya usafiri. Anasema;

> "Miguu yake ikashika kasi mpaka akawa anapeperuka juu na chini angani" (uk.

### 4.1.4 Tashbihi

Wamitila (2003), anafafanua tashbihi kama ulinganishaji unaodhamiria kulinganisha sifa fulani na nyingine na kujenga picha ya aina fulani akilini kwa kutumia viungo kama vile; mithili ya, kama, mfano wa, sawa na, ja, na kama vile. Mwandishi ametumia tashbihi kulinganisha kasi ya Chandu na ile ya gari. Mwandishi anasema kuwa;

> "Miguu ya Chandu ilikuwa kama injini ya gari la *audi* kwa kasi" (uk. 5).

Katika mandhari haya ya shuleni katika *Siku ya Wajinga* mwandishi ametumia tashbihi kulinganisha vile Zito alikuwa ameingiwa na hofu. Zito alifahamu kuwa mwalimu Petro alikuwa amebaini kwamba alikuwa ameiba majibu ya zoezi lile. Mwandishi anasema kuwa;

> "Zito sasa alianza kutetemeka kama unyasi kwenye upepo" (uk 16).

Tashbihi zinazohusu kufananisha matendo huweza kudokeza mandhari husika. Katika mandhari ya ukuzaji talanta, sauti ya mwalimu Rukia inalinganishwa na ya kinanda. Mwandishi anasema;

> "Mwalimu Rukia alikuwa na sauti nzuri kama kinanda" (uk. 20).

Wanafunzi walifurahia sauti ya mwalimu Rukia kiasi cha kuiga sauti hiyo bila mafanikio. Aidha, mwalimu Rukia alisikia sauti moja ambayo haikukubaliana na zingine. Sauti ile ilikuwa ya Zito. Mwalimu Rukia anamwamrisha aseme kwa sauti kuwa yeye anaimba kama chura (uk. 23). Mwandishi ametumia tashbihi kulinganisha kicheko cha Zito na kile cha sokwe au mwenye kichaa na kusaidia kusawiri mandhari ya makaburini.

"Alitoka pale mbio huku Zito akicheka mithili ya sokwe" (uk. 33).

"Zito alianza kucheka tena kama mwenye kichaa" (uk. 34).

### 4.1.5 Tashihisi

Tashihisi ni mbinu ya kuvipa uhai vitu visivyokuwa na sifa za uhai (Khasiani na Indindi, 2018). Wamitila (2003) anasema kuwa tashihisi husawiri vitu visivyokuwa na uhai kupewa sifa za binadamu za kufikirika na kuhisi. Mwandishi ameeleza kuwa sauti hafifu ya mbegu ilisikika hapo mchangani.

"Nitakua polepole mpaka siku moja niwe mwembe mkubwa" (uk. 7).

Mbinu ya tashihisi imetumiwa kusawiri mandhari ya mvua. Mwandishi anayapa maji sifa ya kibinadamu kwa kusema kuwa, maji yalipenya ndani ya mchanga na kukutana na mbegu ya embe (uk. 8). Vilevile, mbegu inasema;

"Ewaa… Huu ndio wakati unaofaa. Nitakuwa hivi karibuni na nitajiimarisha!" (uk. 9).

Mbinu ya tashihisi imetumika kusawiri mandhari ya ukuaji wa mimea na changamoto zake. Baadhi ya mifano hiyo ni;

"Mvua, hewa na joto walijitahidi kuufurahisha mche huo."

"Mche ukageuka kishina. Kishina hicho japo kilikuwa na uchungu mwingi kwa sababu ya majani yake kukatwa na beberu, kilijihimiza na kujituliza. Kikajipa moyo, si hoja. Nitakua polepole halafu nitakuwa mwembe imara na wenye nguvu" (uk. 10).

Mazungumzo kati ya mwembe na vipepeo pia yanadhihirisha tashihisi.

"Tunaweza kuketi hapa kwa muda mfupi? Wakauliza.

"Kwani kuna kosa gani?" Mwembe ukawajibu. Mwembe ulikubali bila tashwishi. Mwembe huo ulikuwa karimu sana" (uk. 11).

Vilevile, tashihisi inajitokeza katika kauli hii ya mwembe;

> "Mwembe mchanga ukalia kwa uchungu na huzuni. Ukawauliza, Mbona nyinyi hamna huruma?"(uk.12).

Mwandishi ametumia mbinu ya tashihisi kusawiri mandhari ya mabadiliko ya miji wakati anaupa mwembe uwezo wa kuzungumza.

> "Mwembe ulitazama chini na kumtambua Chandu papo hapo. *Hakika huyu ndiye Chandu! Chandu wa miaka na mikaka ingawa hana meno tisa sasa!"*(uk. 22).
>
> "Mwembe ukamtazama tena Chandu ukamnong'onezea, Lau ungejua mateso niliyoyashuhudia!" (uk. 22)

**4.1.6 Mbinu rejeshi**

Wamitila (2003) anasema kuwa, fasihi ni sanaa ya lugha ambayo inamhusu binadamu na huwa katika umbo ambalo hutambuliwa na wanajamii. Ni mbinu ambapo mwandishi humrudisha msomaji katika tukio au kisa kilichotokea mbeleni (Khasiani na Indindi, 2018). Mbinu rejeshi huonyesha tukio ilivyokuwa wakati fulani uliopita. Mwandishi ametumia mhusika Chandu kusawiri mandhari mji. Wakati huu Chandu ni mzee na anakumbuka zama zile alipokuwa kijana.

> "Alhamisi ya miaka mingi kupita………… Mzee Chandu alihisi siku hiyo ilikuwa inalingana na ya zamani alipokuwa ghulamu. Lakini hakujua vipi aliifananisha siku hiyo iliyopo na iliyopita. Katika zama hizo soko lilikuwa mbali na kijiji chao. Lakini sasa, licha ya soko kuwa karibu, masoko makuu kadhaa yalikuwa yamefunguliwakatika mji wao" (uk. 23).

**4.1.7 Mazungumzo baina ya wahusika**

Msokile (1999) anasema kuwa, sifa za mhusika hujulikana taratibu katika kazi ya fasihi haswa pale anapozungumza. Katika usawiri wa mandhari ya darasani, mwandishi ameweka wahusika Zito na Sadiki katika mazungumzo:

“Nitakutumikia vipi nawe unataka kushikilia ujinga kuliko werevu?” Sadiki alimuuliza siku moja.

“Eh! Huelewi nawe unajidai u mwerevu?”

“Naelewa maana ya kauli hiyo, lakini sielewi kile unachokusudia,” alitamka Sadiki.

“Sikiliza haya basi. Ukiwa daktari, utanihudumia nikiwa mgonjwa. Ukiwa mwalimu, utafundisha wanangu na ukiwa wakili, utanisimamia katika kesi zangu. Umeelewa sasa? Kwa ujumla, katika kazi yoyote ile utakayoajiriwa kufanya, utakuwa ukitutumikia sisi wajinga. Kwa ufupi, utakuwa mtumishi wetu,” alieleza Zito huku akikenua meno ambayo kawaida hayakukumbana na mswaki.

“Nawe utakuwa ukila nini, ukivaa nini, na ukikaa wapi?” Sadiki alimuuliza.

“Ala! Mahitaji yote nitatimiziwa na nyie werevu. Yangu itakuwa kuketi kitako na kuishi raha mustarehe.”

Sadiki alikuna kichwa huku akifikiri.

“Mbona unakuna kichwa? Ama unataka kujiunga nasi wajinga? Fuata nyuki ule asali, bwana,” alisema Zito huku akicheka.

“Kama unadhani ujinga ni chakula, kapike ule mwenyewe!” sadiki alisema ghafla na kumwacha rafikiye akipasua vicheko kama sokwe (uk. 10 – 11).

Vilevile, kuna mazungumzo kati ya Zito na Zena kama yafuatayo.

“Jamani Zito, hata leo umepata sufuri! Ngoja nikuonyeshe njia ya mkato ya kufanya hesabu hizi,” Zena alimwambia Zito siku moja darasani baada ya mwalimu kutoka.

Zito alitazama huku na huko, kisha akamwambia kwa sauti ya chini, “Hapana, sio sasa. Nionyeshe wakati wa breki” (uk. 13).

Aidha, katika shule ya Hamio kuna mazungumzo baina ya mwalimu Timami na Zito.

"Usipokoma utajikuta mashakani tena. Hatuwezi kuruhusu ukamea pembe mpya hapa."

Zito alipangusa michirizi ya jasho lililomtiririka kwa wingi sasa, kisha akamwambia mwalimu, "Mwalimu, nataka kurudi nyumbani kwetu."

Mwalimu Timami alicheka kwa muda kisha akatamka, "Ati umesema unataka kurudi nyumbani? La hasha! Nyumbani hurudi ng'o! tutahakikisha kwamba huo ujeuri, uvivu na ujinga wako vimekuhama kabisa kabla ya kukurudisha kwenu" (uk. 55).

Mazungumzo haya yanatumiwa na mwandishi kusawiri mandhari ya darasani.

Katika mandhari ya nyumbani, mwandishi amesawiri Zito akizungumza na mamake kutokana na kitendo cha kumfukuza jogoo na kusababisha hamaki kwa mzee Lombo.

"Ulimfanyia nini mzee Lombo?" mama alisaili.

"Ah! Mwache mzee yule mlafi. Jua bado halijatua, yeye anabugia sima kwa mchuzi. Jogoo huyu kamharibia starehe yake leo," Zito alitamka huku akicheka.

"Zito, huu si utani hata. Yaani ulimfukuza kuku hadi nyumbani mwa mzee Lombo? Lahaula! Mwana wewe! Ujinga wako utaisha lini we?" Mama alinena kwa hasira.

"Lakini mama, ujinga huo haufikii ule wa kumtupia kuku mchele ilhali yeye ni chakula pia. Huku ni kuharibu chakula", Zito alimjibu huku akicheka kwa sauti kubwa ambayo ilimkasirisha mamake zaidi.

"Unataka kuniambia mjinga ni mimi niliyekupa mchele?"

"La, mimi ningekuwa mjinga kama ningemtupia jogoo mchele kula, kisha tukamchinja. Hii ingekuwa hasara tu."

"Mwangalie! Zuzu we! Umeenda kuzuzuka mitaani na kuwapa watu vicheko. Wewe huenda shuleni kufanya nini?" mama yake alikuja juu kwa hasira.

"Kusindikiza walio werevu," Zito alitamka. Kwa hasira, mama alimrukia ili amkamate. Kuona hayo, Zito alimtupia jogoo na kuchomoka mbio (uk. 28 – 29).

Mazungumzo haya yanaonyesha jinsi Zito alivyokosa heshima kwa watu wengine na kusaidia katika usawiri wa mandhari ya nyumbani.

**4.1.8 Methali**

Methali ni usemi mfupi wenye maana pana na busara au hekima ilio na mizizi katika jamii fulani na unaoelimisha, kuasa au kukejeli watu au vitendo fulani katika jamii lakini kwa njia iliyofumbwa na kuwekwa tafsida (Wamitila, 2003). Mandhari ya shuleni yamesawiriwa kwa kutumia methali kutimiza malengo tofauti tofauti lakini imedhamiria kutoa ujumbe.

Zito alipokuwa anakimbizwa na mlinzi alifika mahali ambapo palikuwa na ua mrefu wa mawe uliozingirwa na nyaya za stima juu. Mwandishi anatumia methali kuonyesha kuwa mbio za Zito zilifika kikomo.

"Lakini mbio za sakafuni huishia ukingoni" (uk. 58).

Aidha, walimu wa shule ya Hamio waliamua kumpa mawaidha Zito na hivyo kila alipokosa kutimiza wajibu wake alielekezwa kwa kuambiwa methali hii, "ukitaka cha uvunguni sharti uiname" (uk. 60). Zito alipoelewa methali hii alianza kuyabadilisha mawazo yake na kuwa mtu mwema. Aliporudi katika shule ya Kambini aliyafuta yale maandishi yaliyokuwa kwenye dawati lake na kuandika methali aliyokuwa akiambiwa na walimu katika shule ya Hamio, "ukitaka cha uvunguni sharti uiname" (uk. 62 – 63).

**4.1.9 Sadfa**

Sadfa ni utokeaji aghalau wa mambo mawili kwa wakati mmoja bila kupanga au kutarajiwa (Kamusi ya karne ya 21, 2011). Wamitila (2003) anaeleza, sadfa kama mambo mawili au zaidi yanayotokea kwa wakati mmoja bila kutarajiwa lakini yanahusiana kwa kiasi fulani. Mandhari

ya barabarani yamesawiriwa kupitia sadfa. Waislamu na Wakristo wanakutana pale kwenye gurufu bila kutarajiwa lakini matukio wanayoenda kutenda yanahusiana kwa kuwa walikuwa wanaenda kumzika mmoja wao. Mwandishi anasema kuwa, walipofika kwenye gurufu walikita papo hapo – Waislamu hawakuweza kunyanyua unyayo (uk. 1) na magari yaliokuwa na Wakristo hayakuondoka (uk. 2).

**4.1.10 Ritifaa**

Ritifaa ni mbinu ambapo mhusika katika kazi ya kifasihi hufanywa kuzungumza na mhusika mwingine aliyekufa au kitu kisichokuwa na uhai kama kwamba mtu huyo yupo au kitu hicho ki hai (Khasiani na Indindi, 2018). Mazungumzo ya kijusi na mwanamke mjamzito yanawasilishwa kupitia ritifaa.

> *“Mama, una nini? Una nini mama?”* Sauti ndani kwa ndani iliita.
>
> *“Mwanangu, mbona umenitia wasiwasi?”* Sauti ndani kwa ndani ya mjamzito ilimsaili kiumbe aliyekuwa ndani ya kizazi chake …(uk. 3).
>
> *“Mwanangu, kwa nini ulitufanya tusimame saa nzima pale njiapanda?”* Msichana mjamzito akazungumza tena ndani kwa ndani na kiumbe aliyomo kizazini mwake.
>
> *“Nilikuwa naongea …”* Kiumbe akamjibu ndani kwa ndani.
>
> *“Ulikuwa unaongea na nani?”*
>
> *“Na wale watu wawili.”*
>
> *“Watu gani?”*
>
> *“Wale waliobebwa kwenye vitanda.”*
>
> *“Uliongea na nani? … Eti wale watu, eh Maiti?”*
>
> *“Ndiyo! Kwani wewe hukuwasikia?”*
>
> *“La!”*

*"Basi waliongea nami!" …*

*"Alaa! Uliongea nao?"* Msichana mjamzito alimuuliza tena kiumbe aliyekuwa kizazini mwake.

*"Eh! Waliniambia mambo mengi; mengi sana."* Kiumbe akamjibu ndani kwa ndani.

*"Hao maiti?"*

*"Sadakta!"*

*"Ehe! Walikwambia nini?"*

*"Pulika basi, mama …"* (uk. 5).

Mwandishi ametumia wahusika ambao wamefariki (Bikizee na Kijana) na Kiumbe (mhusika ambaye bado hajazaliwa) kuendeleza mazungumzo ni kana kwamba wako pamoja. Kupitia mazungumzo yao, Kijana anaeleza sababu zinazosababisha michafuko na migomo shuleni. Bikizee anatoa ushauri nasaha kuonyesha hekima aliyonayo. Kiumbe anaonekana kuwa mdadisi sana. Mazungumzo kati ya wahusika hawa yanatumiwa na mwandishi kujenga uhalisia ajabu ili kusawiri mandhari ya michafuko na migomo shuleni.

*Kijana:* *Kama vile sisi vijana wanafunzi tulivyofanya. Tulisababisha machafuko shuleni. Tulichoma mabweni yetu sisi maboda pamoja na baadhi ya wanafunzi. Katika hali ya kuchoma, mlipuko wa bomu la petroli ya chupa ukanifikia na kuniunguza vibaya sana mwili mzima mpaka nikafia humo mimi pia. Aidha, tukateketeza maktaba ya shule yetu. Tukayatia moto baadhi ya madarasa, nyumba ya mwalimu mkuu wetu pamoja na gari lake; nusura afie humo. Tulisababisha uharibifu mkubwa sana wa mali! Baadaye tukafanya maandamano!*

*Kiumbe:* *Kisa na maana?*

*Kijana:* *Watatupatiaje mtihani mwingo mgumu ambapo hatujakamilisha silabasi?*

*Bikizee:* *Hiyo ndiyo sababu au kuna nyingine?*

*Kijana:* *Bila shaka! Wenzetu wanasema migomo hiyo imechochewa na uchaguzi wa Desemba 2007 na matokeo ya Januari 2008 yaliyozusha ghasia. Halafu mbona mnatulaumu sisi peke yetu?*

*Bikizee:* *Jinai ni jinai, hata ifanywe na mtu mzima au kijana! Huo ni uhaini tu! Kwani mabweni ya St. Kizito, Bombolulu Girls na Kyanguli yalipochomwa, ulikuwa wakati wa uchaguzi?*

*Kijana:* *Uongozi wa shule zetu pia umechangia. Unafikiri walimu wakuu, manaibu wao na walimu wanapotumia uongozi wa kiimla kuendesha shughuli za shule, wanafunzi watapata uhuru wa kueleza maoni yao?*

*Bikizee:* *Aghlabu wanafunzi wakiachiwa uhuru usio na mipaka, wa kufanya watakavyo, huoni hilo pia ni hatari?* (uk. 7 – 8).

Mazungumzo haya yanatumika kusawiri mandhari ya michafuko na migomo shuleni.

Mwanamke mjamzito anajikita tena katika mazungumzo na Kiumbe katika chumba cha upasuaji. Mazungumzo hayo ni kama yafuatayo.

> *"Mama, mama, uko salama?"* Sauti ndani kwa ndani ikaitana tena. Ilimchukua muda wa kupesa macho kuweza kumjibu.
>
> *"Mwanangu, na wewe uko salama?"* Sauti ndani kwa ndani ya msichana mjamzito ikajibu swali la kiumbe aliyekuwa ndani ya kizazi chake.
>
> *"Mama, wanafanya nini sasa? Wanatufanyia nini?"*
>
> *"Sijui, mwanangu, kwa hakika. Ninachoelewa mimi ni kuwa ninafanyiwa operesheni. Operesheni ya kukutoa kwa utaalamu toka kizazini mwangu kukukaribisha dunia*

*nyingine ngeni usiyoitambua. Dunia ambayo unastahiki zaidi kuishi. Sio humu kizazini mwangu. Utolewe ili kiungamwana changu na chako kikatwe na tutenganishwe."*

*"Mama, eti nisikutegemee wewe tena! Ni haki kweli? Tafadhali mama, wazuie! Naomba unisikize mara ya mwisho!"* (uk. 19 – 20).

Mazungumzo haya japo ni ya kidhahania yanatumiwa na mwandishi kuendeleza usawiri wa mandhari ya hospitali.

### 4.1.11 Majazi

Kulingana na Khasiani na Indindi (2018), majazi ni mbinu ya kisanaa ya kuwapa wahusika au mahali majina kulingana na sifa za mhusika huyo au mahali hapo. Jina hilo hutoa picha ya mhusika au mahali panapozungumziwa. Mwandishi amebuni wahusika kimajazi katika mandhari ya michafuko na migomo shuleni. Mwandishi ametumia jina la Kiumbe kuonyesha kuwa hajazaliwa na hakika kutokana na maelezo yupo ndani ya kizazi cha mamake. Vilevile, mwandishi ametumia jina Kijana kuashiria kuwa maiti wa kwanza ni kijana na jina Bikizee kuonyesha maiti wa pili katika mazungumzo alikuwa mwanamke mzee.

## 4.2 Hitimisho

Sura hii ilibainisha matumizi ya lugha katika usawiri wa mandhari mbalimbali katika vitabu teule vya fasihi andishi ya watoto. Vitabu hivi ni; *Embe Tamu* (Njogu, 2003), *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005) na *Njiapanda* (Amana, 2008).

Mihimili ya nadharia ya kimtindo ilitumika kuchunguza jinsi waandishi wa vitabu teule walivyotumia mbinu mbalimbali za kifasihi pamoja na tamathali za lugha kusawiri mandhari. Mbinu za kifasihi na tamathali za lugha zilizobainika ni pamoja na; taswira, ritifaa, mazungumzo baina ya wahusika miongoni mwa mbinu nyinginezo.

Sura ambayo inafuata ni ya mwisho katika utafiti huu. Sura hii huwa ni hitimisho ya utafiti.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO, MUHTASARI NAMAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi.

Sura hii ya tano ilishughulikia hitimisho ambapo muhtasari wa utafiti ulitolewa. Maelezo kuhusu malengo ya utafiti pamoja na upeo na mipaka yametolewa. Changamoto za utafiti zilielezwa.

Aidha, matokeo ya utafiti yalijadiliwa kubainisha kufanikiwa kwa utafiti katika kutimiza malengo ya utafiti. Manufaa ya matokeo ya utafiti yalielezewa. Isitoshe, mapendekezo yalitolewa kuendeleza utafiti zaidi kuhusu fasihi andishi ya watoto.

## 5.1 Muhtasari

Malengo matatu yaliongoza utafiti huu. Kwanza kabisa, utafiti ulidhamiria kubainisha aina ya mandhari yaliyosawiriwa na waandishi wa vitabu teule vya fasihi andishi ya watoto. Vilevile, ulilenga kuchunguza jinsi mandhari yalivyochangia sifa za wahusika katika hivyo vitabu teule vya fasihi andishi ya watoto na mwisho utafiti ulidhamiria kubainisha matumizi ya lugha katika kusawiri mandhari hayo.

Ili kutimiza malengo ya utafiti, vitabu vitatu vya fasihi andishi ya watoto viliteuliwa kimaksudi. Vitabu hivi ni pamoja na: *Embe Tamu* (Njogu, 2003), *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005) na *Njiapanda* (Amana, 2008). Tasnifu imegawanywa katika sura tano.

Sura ya kwanza ilishughulikia masuala ya uandishi wa tasnifu katika idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. Baadhi ya masuala haya ni: suala la utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada na misingi ya nadharia ambapo nadharia mbili ziliongoza utafiti huu yaani; nadharia ya finominolojia na nadharia ya kimtindo. Aidha, mbinu za utafiti zilishughulikiwa. Katika mbinu za utafiti, mambo yaliyoshughulikiwa ni

pamoja na; mtindo wa utafiti, mahali pa utafiti, uteuzi wa sampuli, njia za ukusanyaji data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo.

Sura ya pili ilishughulikia usawiri wa aina za mandhari kuwasilisha maudhui katika fasihi andishi ya watoto. Utafiti uliangazia usawiri wa aina za mandhari katika vitabu teule yaani, usawiri wa mandhari katika: *Embe Tamu* (Njogu, 2003), *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005) na *Njiapanda* (Amana, 2008).

Sura ya tatu ilichunguza sifa za wahusika kutokana na mandhari. Vitabu teule vya fasihi andishi ya watoto yaani; *Embe Tamu* (Njogu, 2003), *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005) na *Njiapanda* (Amana, 2008) vilitumiwa kuchunguza sifa za wahusika kutokana na mandhari.

Sura ya nne ilibainisha matumizi ya lugha katika usawiri wa mandhari. Matumizi ya lugha katika usawiri wa mandhari katika vitabu teule yaani; *Embe Tamu* (Njogu, 2003) *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005) na *Njiapanda* (Amana, 2008) yalichunguzwa.

**5.2 Matokeo ya Utafiti**

Utafiti huu ulidhamira kutimiza malengo matatu. Lengo la kwanza lilikuwa kubainisha aina za mandhari kuwasilisha maudhui katika vitabu teule vya fasihi andishi ya watoto. Utafiti huu ulibaini kuwa, waandishi mbalimbali husawiri aina mbalimbali za mandhari kutegemea mwandishi mwenyewe na mandhari yanayomzunguka pamoja na misukumo ya kuandika kazi yenyewe ya fasihi.

Katika *Embe Tamu* (Njogu, 2003) utafiti ulibainisha aina mbalimbali za mandhari yaliyosawiriwa kuwasilisha maudhui na mwandishi. Mandhari haya ni pamoja na; Mandhari ya ghala ambayo yalisawiriwa kuwasilisha maudhui ya ukulima. Isitoshe, mwandishi amesawiri mandhari ya sokoni kuweka wazi maudhui ya biashara. Mandhari ya usafiri, ufugaji na ya mvua vilevile yamesawiriwa. Aidha, mwandishi amesawiri mandhari ya ukuaji wa mimea. Mandhari

haya yamesawiriwa kusisitiza maudhui ya ukulima na changamoto zake. Zaidi ya hayo, mwandishi amesawiri mandhari ya uharibifu wa mazingira na kuonyesha athari za shughuli za jamii kwa mazingira na mwisho amesawiri mandhari ya mjini kuweka wazi maudhui ya maendeleo na mabadiliko.

Utafiti vilevile uliangazia usawiri wa aina mbalimbali za mandhari katika *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005), ambapo mandhari ya nyumbani yalisawiriwa kuwasilisha maudhui ya kilimo na ufugaji. Mandhari ya shuleni yamesawiriwa na mwandishi kuwasilisha maudhui pana kama vile maudhui ya; kielimu ushauri nasaha, majuto, mabadiliko na utaaluma. Mandhari ya darasani yamesawiriwa kuendeleza maudhui ya elimu na vilevile, kubainisha taasubi ya kiume katika jamii. Maudhui ya ubaguzi na ukuzaji talanta yamewasilishwa kupitia usawiri wa mandhari ya darasani. Mwandishi amesawiri mandhari ya michezo kubainisha umuhimu wa michezo kwa wanafunzi. Mandhari ya makaburini ambayo yamesaidia kuendeleza maudhui ya vifo na utamaduni. Mandhari ya hospitalini yamesawiriwa kuonyesha maudhui ya ushirikiano katika jamii.

Katika *Njiapanda* (Amana, 2008), mwandishi amesawiri mandhari ya barabarani kuonyesha itikadi na imani za jamii. Isitoshe, mwandishi ameangazia mandhari ya kidhahania ambapo amewasilisha maudhui ya ushauri nasaha. Vilevile, mwandishi amesawiri mandhari ya shuleni kuweka wazi maudhui ya migomo shuleni na madhara ya migomo hiyo. Mandhari ya hospitali yamesawiriwa pia kuonyesha maudhui ya; taaluma na kazi, mawasiliano, usaliti wa kimapenzi miongoni mwa maudhui mengineyo.

Lengo la pili la utafiti lilikuwa kuchunguza jinsi mandhari yaliyosawiriwa na waandishi wa vitabu teule yalivyochangia sifa za wahusika. Ilibainika kuwa, waandishi wamesawiri aina mbalimbali za mandhari ili kusaidia kukuza na kulenga wahusika katika kazi zao. Aina ya

mandhari inayomzunguka mhusika huchangia sifa za mhusika huyo katika kazi ya fasihi. Kila aina ya mandhari iliyosawiriwa na mwandishi ilichangia sifa kadha wa kadha za mhusika katika mandhari hayo.

Katika *Embe Tamu* (Njogu, 2003), utafiti ulibainisha kuwa mandhari mbalimbali yalichangia sifa za wahusika. Kutokana na mandhari ya ghala wahusika walipata sifa kama vile; ushirikiano, uwajibikaji na bidii. Mandhari ya sokoni yaliwapatia wahusika sifa kama vile; amani na wenye bidii. Mandhari ya usafiri yalionyesha wahusika wenye kuwajibika na wenye tamaa.

Mandhari ya ufugaji yalidhihirisha wahusika wenye utulivu na watambuzi. Isitoshe, mandhari ya mvua yameonyesha wahusika wenye matumaini na ushirikiano.

Zaidi ya hayo, ilibainika kuwa, mandhari ya ukuaji wa mimea yalichangia wahusika ambao ni; katili, waharibifu, wakarimu na wenye matumaini.

Mandhari ya uharibifu wa mazingira yameonyesha wahusika ambao ni waharibifu na wasio na huruma.Mwisho, katika mandhari ya mjini, wahusika wameonyesha sifa kama vile; wenye shukrani na wenye kumbukizi.

Utafiti ulibainisha kuwa mwandishi katika *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005) amesawiri mandhari ambayo yamechangia sifa mbalimbali za wahusika. Katika mandhari ya nyumbani, wahusika wameonyesha ushirikiano, bidii kazini, wenye ujinga na uchokozi. Mandhari ya shuleni yamebainisha wahusika ambao ni wasomaji, wenye moyo wa kusaidia, wanjanja, wasumbufu na wenye majuto.

Kutokana na mandhari ya darasani, utafiti umebainisha kuwa, wahusika ni; wacheshi, wenye taasubi ya kiume na ni waelekezi. Kwenye mandhari ya michezo wahusika wamedhihirisha ujirani mwema na wenye ushirikiano.  Zaidi ya hayo, mandhari ya makaburini imebainika kuwa,

yamewapatia wahusika sifa ya kuwa watamaduni na wachokozi. Kutokana na mandhari ya hospitali wahusika ni wenye utu na upendo.

Katika *Njiapanda* (Amana, 2008) imebainika kuwa, mwandishi amesawiri aina mbalimbali za mandhari ambayo yamechangia sifa kadha wa kadha za wahusika. Mandhari ya barabarani yamechangia sifa zifuatazo za wahusika. Wenye kufuata utamaduni wao, ni wacha Mungu na wenye ushirikiano.

Katika mandhari ya kidhahania wahusika wameonyesha kuwa ni; watambuzi, wenye hekima na wenye majuto. Isitoshe, wameonyesha kuwa ni wenye mapuuza na wenye kutetea haki zao pamoja na kuwa wadadisi. Mandhari ya hospitali yamechangia sifa za wahusika kama vile; wahusika wenye kuwajibika, waaminifu, wenye utu na nia njema pamoja na kuwa wenye urafiki wa dhati na ushirikiano.

Lengo la tatu la utafiti lilikuwa kubainisha matumizi ya lugha katika usawiri wa mandhari. Ilibainika kuwa kila mwandishi alitumia mbinu za lugha na tamathali za usemi kusawiri mandhari.

Utafiti ulibainisha kuwa, katika *Embe Tamu* (Njogu, 2003) mwandishi alitumia mbinu mbalimbali za lugha kusawiri aina mbalimbali za mandhari. Katika usawiri wa mandhari ya ghala, mwandishi alitumia usimulizi kusawiri mandhari. Aidha, usimulizi na taswira ni mbinu zilizotumika kusawiri mandhari ya sokoni na usafiri.

Mandhari ya ufugaji na mvua yalisawiriwa kupitia usimulizi na tashihisi. Isitoshe, mandhari ya ukuaji wa mimea pamoja na mandhari ya uharibifu wa mazingira yalisawiriwa kwa kutumia taswira, tashihisi na usimulizi. Zaidi ya hayo, mandhari ya mjini yalisawiriwa kupitia mbinurejeshi, taswira na tashihisi.

Katika *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005), mwandishi amesawiri mandhari ya shuleni na mandhari ya nyumbani kupitia usimulizi, mazungumzo baina ya wahusika, taswira na tashibihi. Isitoshe, mandhari ya darasani yalisawiriwa kwa matumizi ya mazungumzo baina ya wahusika, usimulizi, tashbihi pamoja na taswira. Mandhari ya michezo yamesawiriwa kwa kutumia usimulizi. Mandhari ya makaburini yalisawiriwa kupitia taswira na tashbihi lakini mandhari ya hospitali yakasawiriwa kupitia usimulizi. Mandhari ya mjini yalisawiriwa kupitia masimulizi na matumizi ya methali.

Kwenye *Njiapanda* (Amana, 2008), ilibainika kuwa mwandishi amesawiri mandhari ya barabarani kupitia taswira na sadfa. Mandhari ya kidhahania yamesawiriwa kwa matumizi ya ritifaa. Aidha, mandhari ya shuleni yamesawiriwa kwa matumizi ya ritifaa na majazi. Matumizi ya taswira na ritifaa yamebainika katika usawiri wa mandhari ya hospitali.

Malengo ya utafiti yaliweza kutimizwa na pengo lililokuwa wazi katika usawiri wa mandhari katika fasihi andishi ya watoto kuzibwa.

**5.3 Umuhimu wa Matokeo ya Utafiti**

Matokeo ya utafiti huu yalikuwa muhimu kwa wakuza mtaala kwani watasaidika katika uteuzi wa vitabu vya kusoma vya wanafunzi kwani watatumia usawiri wa mandhari kama kigezo cha uteuzi. Vilevile, waandishi wa vitabu vya fasihi andishi ya watoto watanufaika kwani wataweza kujisaka zaidi na kubuni mandhari mwafaka yanayoafiki hadhira lengwa.

Wasomi wa fasihi andishi ya watoto na fasihi kwa jumla watanufaika na utafiti huu kwani wataweza kulinganisha na kulinganua usawiri wa mandhari wa waandishi mbalimbali. Walimu na wanafunzi watanufaika na ufafiti huu kwani wataweza kuchambua vitabu kwa kuangalia umuhimu wa mandhari katika kuwasilisha maudhui na umuhimu wa mandhari hayo katika kukuza na kuendeleza sifa za wahusika.

## 5.4 Changamoto za Utafiti

Utafiti ulikumbwa na changamoto kadha; muda wa kushughulikia masomo ulipungua na ulipopatikana haukua wa kutosha kwani mtafiti ni mwalimu na shughuli za kazi zililemeza utafiti. Zaidi ya hayo, uhaba wa pesa za kulipia karo na ada nyinginezo zinazoambatana na utafiti ziliutatiza utafiti.

Vilevile, mtandao ulitumika sana katika utafiti na mara nyingi shida za umeme kupotea zilitatiza utafiti. Ugonjwa wa korona umeathiri kila nyanja ya elimu kwa hivyo utafiti huu uliadhirika pakubwa kwani mwendo ulidhibitiwa na ikawa vigumu kufika maktabani.

Hata hivyo, mbinu badala kama kutumia siku za likizo kupata muda wa utafiti. Vilevile, idhini ya kutumia baruapepe kuwasiliana na wasimamizi ilisaidia sana,

## 5.5 Mapendekezo

Utafiti huu ulishughulikia usawiri wa mandhari katika fasihi andishi ya watoto. Aina mbalimbali za mandhari zilibainishwa kusawiriwa na waandishi wa vitabu teule vilivyotumika katika utafiti. Malengo ya utafiti yalikuwa kubainisha aina za mandhari kuwasilisha maudhui katika vitabu teule, pili kuchunguza jinsi mandhari hayo yalichangia sifa za wahusika na tatu kubainisha matumizi ya lugha katika kusawiri mandhari katika fasihi andishi ya watoto.Utafiti zaidi unaweza kufanywa kuhusu usawiri wa mandhari katika tanzu za fasihi simulizi ya watoto kama vile; nyimbo za watoto, hadithi za watoto, ushairi na kadhalika. Aidha, utafiti zaidi unaweza kufanywa kwa kutumia nadharia nyingine bali na ya finominolojia na kimtindo zile zilizoongoza utafiti huu. Vilevile, utafiti unaweza kufanywa kuhusu usawiri wa mandhari wa waandishi bali na *Embe Tamu* (Njogu, 2003), *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005) na *Njiapanda* (Amana, 2008).

**MAREJELEO**


Akoliet, J. (1990). Response and Critism in Children's Literature in Kenya: The Case of Barbara Kimenye. M.A Thesis Kenyatta University. (Haijachapishwa)

Amana, B. (2008). *Njiapanda*. Nairobi: Oxford University Press, East Africa Limited.

Bal, M. (1997). *Narratology: Introduction to the Theory of Narrative* (2nd edition). Toronto: University of Toronto Press.

Bakize, L.H. (2014). *Utangulizi wa Fasihi ya Watoto*. Dar es Salaam. Moccony Printing Press.

Elmeel, S. na Elmeel, D. (1996). *Educator's Companion to Children's Literature. Folklore Contemporary Realistic Fiction, Fantacy, Biographies and Tales from here and there, Volume 2*. London: Greenwood Publishing Group.

Erickson, N. L. (2018). The Importance of Setting in Your Story. Retrieved from https://blog.bookbaby.com/2018/02/Importance-of-Setting-in-Your-Story/.27/4/2021.

Fang, Z. (1996). "Illustrations, Text, and the Child Reader: What are Pictures in Children's Story books for?". In, *Reading Horizons: A Journal of Literacy and Language Arts*. Pp. 2 – 3.

Gatere, L.N. (2019). Usawiri wa Familia ya Kisasa katika Fasihi ya Watoto Nchini Kenya. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Heidegger, M. (1982). *The Basic Problems of Phenomenology*. Trans. Albert Hofstadter. Bloomington: Indiana University Press.

Hunt, P (2006). *Introduction: The expanding World of Children's Literature Studies. In understanding Children's Literature* (PP. 11- 24). Routledge.

Husserl, E. (1989). *Ideas Pertaining to a Pure Phenomenology and a Phenomenological Philosophy, Second Book*. Trans. Richard Rojcewicz and Andre Schuwer. Dordrecht and Boston: Kluwer Academic Publishers.

Kahenya, P. W. (1992). Children's Literature: An analytical study of the content value of the Tintin Comics. M.A Thesis. The University of Nairobi. (Unpublished).

Kairu, W. (2005). Uhalisia na Mtindo wa Ken Walibora katika Fasihi ya Watoto. Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Karanja, D. W. (2008). Usawiri wa Masuala Ibuka katika Hadithi za Watoto Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Karuga, M. N. (2005). Uhakiki na Upokezi wa Fasihi ya Kiswahili ya Watoto katika Shule za Msingi Nchini Kenya. Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Khaisani, D. na Indindi, H. (2018). *Mwongozo wa K.C.S.E Fasihi*. Nairobi, Kenya: Vide Muwa Publishers Limited.

Leech, G. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry*. London: Longman Group Ltd.

Longhorn Publishers, (2011). *Kamusi ya Karne ya 21*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks Graphics na Publishing.

Merleau, P. M. (2012), *Phenomenology of Perception*, Trans. Donald A. Landes. London and New York: Routledge.

Ministry of Education Science and Technology (2015). *Approved List of School Textbooks and Other Instructional Materials for ECDE, Primary Schools and Teacher Training Colleges.* (14th ed.). Vol. 1, 2015.

Mligo, E.S. (2012). *Jifunze Utafiti: Mwongozo kuhusu Utafiti na Uandishi wa Ripoti yenye Mantiki.* Dar es Salaam: Ecumrnical Gathering (EGYS).

Mohanty, J. (2011), *Edmund Husserl's Freiburg Years: 1916-1938*. New Haven and London:Yale University Press.

Momanyi, C. (2005). *Siku ya Wajinga*. Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

Moran, D. (2000). *Introduction to Phenomenology*. London and New York: Routledge.

Msokile, M. (1999). *Misingi ya Hadithi Fupi*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mugenda, O.M. na Mugenda, A. G. (1999). *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches*. Nairobi: Acts Press.

Muthubi, F. (2005). Usimilishwaji katika Fasihi ya Watoto. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Muusya, J. (2012). Mandhari katika Hadithi Fupi: Ulinganishaji wa Diwani za Pendo la Heba na Hadithi Nyingine na Mizungu ya Manabii na Hadithi Nyingine. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Mwanzi, H. (1982). *Children's Literature in Kenya. An Analysis of Children's Prose Fiction*. M.A. Thesis University of Nairobi: (Haijachapishwa).

Mwendwa, S.M. (2020). Usimilisho wa Vielelezo katika Hadithi za Watoto na Namna Vinavyochangia katika Uwasilishaji Ujumbe. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Ngara, E. (1982). *Stylistic Criticism of the African Novel*. London: Heinemann.

Ngari, G. A. (1990). Maigizo ya Kienyeji ya Watoto Nchini Kenya: Nafasi ya Kuyatumia katika Ufundishaji. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Ngiti, M.A. (2019). Dhima za Hurafa katika Fasihi ya Watoto. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Ngugi, E. (2018). Maudhui na Mtindo katika Ushairi wa Watoto: Uchanganuzi wa *Utenzi wa Haki za Watoto* na *Mashairi Bulbul*. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Njogu, K. (2003) *Embe tamu.* Nairobi: Oxford University Press East Africa Limited.

Njogu, K. na Chimerah, R. (2008). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. (Chapa ya Pili). Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njue, J. G. (2015). Tathmini ya Hadithi za Watoto katika Mitandao. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Odhiambo, D.A. (2018). Ufasiri wa Ngano za Kifantasia Miongoni mwa Watoto wa Shule za Msingi. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Omuya, R. (2017). Usimilishwaji wa Biblia kama Fasihi ya Watoto Hadithi teule. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Oyoo, M. (2003). *Theory of Children's Literature: A Module*. The Catholic University of Eastern Africa – Literature Department.

Ruthiiri, M. (2012). Tathmini ya ufaafu wa vitabu vya kusoma kwa madarasa ya tano na sita katika shule za msingi. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Santora, L. (2005). *Assessing Children's literature*. New York. ADL.

Smith, D. na Thomasson, A. (eds), (2005). *Phenomenology and Philosophy of Mind*. Oxford and New York: Oxford university press.

Smith, D. W. (2013). *Phenomenology" The Stanford Encyclopedia of Philosophy. The Metaphysics Research lab, center for the study of language and information*. New York: Stanford university press.

Sweetlands, R. (2017). *Elements of Story or Fiction - character, setting, plot, point of view, style, tone, theme.*www.homeofbob.com/literature/genre/fiction/ficElements.html. Downloaded 24/4/2017.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi. Focus Publication Limited.